# Nipashe

Jumanne Julai 23, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579977

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US







## Mhandisi MV Mapinduzi adaiwa kujinyonga melini

UKURASA 3

UKURASA 13

# Mazungumzo ya Nape, Makamba yazua jambo

• **Mbunge** ataka walioyadukua washughulikiwe, TCRA, Polisi watoa neno...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**MAJALIWA AKATA MZIZI WA FITINA NGORONGORO**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wananchi wanaoishi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro...

UKURASA WA 3

**AJALI YA HIACE YAUA SITA, YAWAJERUHI 24**

WATU sita wakiwamo watoto wadogo watatu, wamefariki dunia papo hapo, baada ya magari mawili kugongana...

UKURASA WA 4

**MPINA ASHUKIA WANAOTAKA KUMKWAMISHA MAGUFULI**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amewashukia baadhi ya watu waliowahi kupewa nyadhifa za juu...

## Mwinyi adai January kamkwaza

UKURASA 26



UKURASA 2

Rais John Magufuli akisisitiza jambo kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene (kulia) na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, baada ya kuwaapisha Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Maagizo 6 ya JPM kwa Bashe, Simbachawene


TAIFA STARS vs KENYA

JULAI 28, 2019 • UWANJA WA TAIFA




HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18, TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

## KESI YA MAUAJI:

# Mahakama yaelezwa mshtakiwa alikiri kumpiga mjukuu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imeambiwa kwamba mshtakiwa Ester Lyimo, alipotoa maelezo ya onyo wakati akihojiwa na Inspekta wa Polisi Salma Sechonge (43), alikiri kumpiga mjukuu wake Naomi John (7) (wakati wa uhai wake) mara kwa mara pamoja kumfinya sehemu mbalimbali za mwili wake.

Kadhalika amedai kuwa alipomhoji mshtakiwa alikiri kurudia kumpiga na kumfinya sehemu zenye majeraha katika mwili wa Naomi.

Inspekta Sechonge alitoa ushahidi katika kesi ya mauaji ya Naomi mbele ya Naibu Msajili Pamela Mazengo, anayesikiliza kesi za mauaji baada ya mahakama hiyo kupewa mamlaka ya kusikiliza kesi hizo.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Cecilia Mkonongo, akisaidiana na Wakili wa Serikali, Joyce Nyumayo.

Akiongozwa na Nyumayo, shahidi alidai kuwa Machi 25, 2017 akiwa ofisini kwake Kituo cha Polisi Mbagala, Mkoa wa Kipolisi Temeke, aliitwa na bosi wake akapewa amri ya kwenda kumhoji mtuhumiwa wa mauaji.

Alidai kuwa saa moja usiku alikwenda Kituo cha Polisi Charambe, alikohifadhiwa mtuhumiwa kwa ajili ya kumhoji na kuandika maelezo.

"Nilimkuta mtuhumiwa na nilijitambulisha kwake kwamba namwandikia maelezo ya onyo ana haki ya kuita wakili wake, ndugu au akiwa mwenyewe, nilimfahamisha maelezo hayo yatatumika mahakamani kama kielelezo, alikubali kuyatoa bila uwakilishi," alidai shahidi na kuongeza.

"Mshtakiwa alianza kutoa maelezo yake kwa kukiri kuwa alimchapa Naomi (wakati wa uhai wake) mara kwa mara na alikuwa anarudia sehemu zenye makovu na majeraha kwenye mwili wake," alidai Inspekta Sechonge.

Alidai kuwa baada ya kumaliza kumhoji alimpa akayasoma, alithibitisha na kuyasaini.

Shahidi mwingine, mtaalamu wa kupiga picha na kuchora ramani wa Jeshi la Polisi, Sajenti Mgeni (52), alidai kuwa alipewa kazi ya kupeleleza tukio la mauaji.

Alidai kuwa Machi 26, 2017, alipofika ofisini bosi wake alimkabidhi jalada la kupeleleza likiwa na watuhumiwa watatu wote wanawake, Ester Lyimo, Victoria John na Jacqline.

Alidai kuwa kabla ya kuwahoji alimfahamisha bosi wake Mkuu wa Upelelezi Mbagala, Afande Walelo, kwamba anataka kwenda eneo la tukio.

Shahidi huyo, akiongozwa na Mkonongo alidai kuwa aliongozana na askari mwenzake Aloyce na mtoto wa mshtakiwa Victoria kwenda nyumbani kwake kwa sababu hawakupafahamu.

"Tulipofika tulipokelewa na watoto wawili wa kiume akiwamo Andrew ambaye alikuwa na mikwaruzo usoni, shingoni na mkononi nilianza kumhoji akanieleza majeraha hayo yametokana na kupigwa na mama mdogo, nilipomfunua alikuwa anatisha zaidi ngozi ilikiwa ina majeraha kama kenge," alidai shahidi na kuongeza:

"Nilipomwona Andrew katika hali ile nikabaini

INAENDELEA UK. 8

# Mazungumzo kina Nape, Makamba yaibua jambo

**Na Mary Geofrey**

MBUNGE wa Ubungo, Saed Kubenea (Chadema), ameitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) na vyombo vya dola nchini kuchukulia hatua dhidi ya waliohusika kudukua mawasiliano yanayodaiwa ya viongozi wastaafu na watu mashuhuri.

Wiki iliyopita, mazungumzo yaliyokuwa na sauti zinazodaiwa za Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye (CCM) na makatibu wakuu wa zamani wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba, yalikuwa yanasambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu changamoto hiyo, Kubenea alisema vyombo vya dola vinapaswa kuwachukulia hatua waliodukua mazungumzo ya viongozi hao.

Alisema kuwapo kwa vitendo hivyo vinavyoendelea kushika kasi nchini ni kinyume cha katiba ya nchi ibara ya 16 na ili kudhibiti suala hilo, anafikiri ipo haja wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Kuvuja kwa mawasiliano ya watu ni kinyume cha sheria ya mawasiliano nchini. TCRA inayosimamia sheria hii na vyombo vya ulinzi na usalama waeleze nani anafanya kazi hii kwa sababu haiwezekani wakawa wamerekodi vipande vifupi tu, lazima wamerekodi mazungumzo marefu," Kubenea alisema.

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza wakati alipotembelea mnara wa fuvu la binadamu wa kale (Zinjanthropus Boisei), uliopo katika Bonde la Olduvai-Ngorongoro, mkoani Arusha jana. Kutoka (kushoto) ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Khamis Kigwangala. **PICHA: OWM**

# Maagizo 6 ya JPM kwa Bashe, Simbachawene

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amewaapisha George Simbachawene na Hussein Bashe kushika nyadhifa alizowateua juzi, huku akiwataka kutekeleza mambo sita katika wizara zao.

Simbachawene ameteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), akichukua nafasi ya January Makamba ambaye uteuzi wake umetenguliwa wakati Bashe ameteuliwa kuwa Naibu wa Kilimo.

Akizungumza wakati wa kuwaapisha mawaziri hao Ikulu jijini Dar es Salaam jana, Rais Magufuli alitoa maagizo manne kwa Simbachawene ikiwa ni pamoja na kwenda kusimamia vizuri Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

"(Suala la) Muungano ukalisimamie vizuri, ukawe chachu ya kuuimarisha, usiwe chachu ya kuuharibu," Rais Magufuli aliagiza.

Kiongozi huyo wa nchi pia alimtaka Simbachawene akahakikishe fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya wizara yake zinatoa matokeo chanya na yanayoonekana.

Alimtaka waziri huyo wa zamani wa Nishati na Madini na Ofisi ya Rais-Tamisemi kwenda kushughulikia miradi hewa, akiutolea mfano mradi wa Rufiji ambao wahusika walidai wamepanda mikoko, lakini haipo.

Katika agizo lake la tatu kwa Simbachawene, Rais Magufuli alimtaka waziri huyo kuhakikisha anakwenda kutatua changamoto ya ucheleweshaji wa vibali kwa wawekezaji inayolikabili Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc).

"Vibali kwa mfano vya Nemc, pasiwe na ucheleweshaji utoaji vibali kwa viwanda vyetu, tunataka kuwa na viwanda vya kutosha na wawekezaji wasiwekewe vipingamizi kwa visingizio vya Nemc, vibali hivi vitoke kwa wakati," Rais Magufuli alionya.

Alisema haoni sababu wawekezaji kucheleweshwa kuwekeza kwa sababu ya vibali, akishauri ikiwezekana wawekeze kwanza ndipo vitolewe baadaye.

"Nimekuwa nikipata matatizo sana kwenye suala hili mpaka uzungumze, ukishazungumza utasikia kibali kimetolewa baada ya siku tano, unajiuliza kwanini hakikutolewa mwaka mzima uliopita? Nenda kalisimamie hili, ukakae na wataalamu wako," aliagiza.

Rais Magufuli pia alimtaka Simbachawene kwenda kuyasimamia vyema masuala ya mazingira na changamoto zake.

"Nakumbuka suala la mifuko ya plastiki lilichukua miaka minne, licha ya kutia saini, lakini halikutekelezwa. Makamu wa Rais (Samia Suluhu Hassan) akazungumza, haikutekelezwa, Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) akaenda kuzungumza bungeni halikutekelezwa, mpaka mwishoni nilipotoa amri ya lazima ndipo likaanza kutekelezwa," alisema.

"Usiende ukafanye hivyo wewe, kayatekeleze haya kwa sababu ni yale uliyoyaapa leo (jana), bahati nzuri utajifunza mengi kutoka kwa Makamu wa Rais ambaye ni msimamizi mzuri, kashirikiane naye katika kutekeleza

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Idara ya Mazingira wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Modester Mushi, akitoa maelezo kuhusu eneo la Mtoni Mashine ya Maji ambalo linapata maji kupitia mtambo wa maji wa Mtoni, kwa kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2019, Mzee Mkongea Ali, baada ya kutembelea chanzo hicho jijini Dar es Salaam jana na kupanda miti pembezoni mwa mto huo kwa lengo la kutunza na kuhifadhi mazingira. **PICHA: FRANK MONYO**

# Majaliwa akata mzizi wa fitina Ngorongoro

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wananchi wanaoishi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kuwa watulivu wakati serikali inaandaa utaratibu shirikishi wa matumizi ya eneo hilo.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya miaka 60 na makumbusho mpya ya kambi ya Dk. Lous Leakey na mkewe Dk. Mary Leakey, waliogundua fuvu la binadamu wa kale Zinjathropus, katika eneo la Olduvai Gorge lililoko ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro mkoani Arusha.

Majaliwa alisema wananchi wa eneo hilo wanapaswa kutambua kuwa hakuna atakayewatupa, kwa kuwa serkali ni yao, inawapenda, inawatunza na kulinda haki zao, na kuwataka kutokuwa na wasiwasi kwa kuwa maslahi yao yatalindwa.

Hivi karibuni, serikali iliunda tume ya kuja na matokeo ya kisayansi juu ya matumizi sahihi ya eneo la Ngorongoro kutokana na ongezeko la changamoto za migogoro baina ya wananchi wanaoishi ndani ya hifadhi na wanyama.

NCAA inasema mwaka 1959 wakati hifadhi hiyo inaanzishwa, idadi ya watu ilikuwa 8,000 lakini kwa sasa kuna zaidi ya watu 95,000, huku kukiwa na uhitaji wa kubadili muundo wa maisha kwa kula vyakula vingine na siyo mazao ya mifuko na nyama, kujenga kisasa na mabadiliko ya utamaduni.

Waziri Mkuu aliahidi wananchi hao kuwa watafanya kikao cha pamoja ili watoe yaliyomo vifuani mwao juu ya mgogoro uliopo kwa

INAENDELEA UK.26

# Mhandisi wa MV Mapinduzi akutwa amejinyonga melini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MHANDISI wa Umeme wa meli ya MV Mapinduzi, Haji Abdallah Khatib (50), amedaiwa kujinyonga wakati meli hiyo ikiwa katika safari yake ya kutoka Unguja kwenda Pemba.

Kutokana na tukio hilo, Meli hiyo MV Mapinduzi 2 imelazimika kukatisha safari yake na kurejea kutia nanga ili kutoa mwili huo na kisha kuendelea na safari.

Meli hiyo ambayo iliondoka jana katika Bandari ya Unguja majira ya saa 2:00 asubuhi ikiwa na abiria 448, ilikaribia katika kisiwa cha Pemba, lakini ilishindwa kuendelea na safari baada ya kubaini kuwa mhandisi huyo amejinyonga na kufariki dunia. Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Mustafa Aboud Jume, alisema tukio hilo limetokea majira ya saa 3:30 asubuhi wakati meli hiyo ikiwa katika eneo la bahari ya kisiwa cha Tumbatu ikiwa safarini kwenda Pemba.

Alisema baada ya kukuta mhandisi huyo ameshajinyonga na kufariki dunia, nahodha wa meli hiyo, Abubakar Zuberi Mzee, alitoa taarifa na kutakiwa meli hiyo irudi Unguja.

"Tayari meli imeshafika katika Bandari ya Unguja na maiti imeshashushwa kwa ajili ya kupelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa uchunguzi," alisema.

Alisema baada ya mwili wa marehemu kuteremshwa, meli hiyo iliendelea na safari kuwapeleka abiri Pemba.

Katibu Mkuu huyo alisema baada ya kutokea kwa tukio hilo, abiria walipewa taarifa na hali ilikuwa shwari na hakukuwa na taharuki yoyote. Meli hiyo ambayo ilikuwa ifike majira ya saa sita kisiwani Pemba, baada ya kutokea kwa tukio hilo ilitarajiwa kufika saa 10:00 jioni. Mmoja wa waliokuwamo katika meli hiyo, ambaye hakutaka kutajwa jina lake, alisema baada ya kupewa taarifa ya tukio hilo, walipata taharuki kubwa lakini walitulizwa baada ya kuelezwa hali halisi ya tukio hilo na kukawa na utulivu hadi meli hiyo ilipotia nanga katika Bandari ya Malindi, Unguja na maiti kutolewa.

"Tunashukuru meli imefika salama katika Bandari ya Malindi na hivi sasa tupo safarini tunakwenda Pemba baada ya maiti kutolewa," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Thobias Sedeyoka, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema uchunguzi unaendelea ili kubaini chanzo cha kifo hicho. Hilo ni tukio la nne kutokea kwa watu wanaodaiwa kujinyonga katika Mkoa wa Mjini Magharibi kwa mwaka huu ikiwamo tukio la Kamishna Msaidizi wa Polisi Azizi Ali kukutwa nyumbani kwake akiwa ameshafariki dunia. Pia msichana mmoja huko Kisauni alikutwa akiwa amejinyonga nyumbani.

# Ajali ya Hiace yaua sita, yawajeruhi 24

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU sita wakiwamo watoto wadogo watatu, wamefariki dunia papo hapo, baada ya magari mawili kugongana wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga.

Tukio hilo lilitokea juzi usiku katika Kijiji na Kata ya Nyambula barabara ya Kahama-Kakola Tarafa ya Kahama Mjini, na kuhusisha gari aina Toyota Land Cruiser namba T.477 ATC, mali ya Thomas Evarist Katoto (47), mkazi wa Kahama na gari aina ya Toyota Hiace namba T.710 AZZ, ambayo mmiliki wake hajafahamika.

INAENDELEA UK.26


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **JAGA AUCTION MART COMPANY LIMITED and TINCOM COMPANY LTD** ,kwa niaba ya Access Bank Tanzania Limited watauza kwa njia am nada wa hadhara, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kua utakapopita muda wa siku kumi am na(14) kwa dhamana ya nyumba au kiwanja; . Dhamana husika zitauzwa kwa njia am nada kwa siku husika iliyopangwa. Mnada utafanyika sehemu nyumba husika ilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| Na | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | TAREHE | MAHALI ILIPO DHAMANA NA KAMPUNI INAYOUZA | MUDA WA MNADA | AUCTION COMPANY. |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KIGODA/ABBASS, KIGODA | KIGODA/ABBASS, KIGODA | HOUSE | 03/08/2019 | VIGWAZA | KUANZIA SAA 2:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JAGA AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| **2.** | BISWALO/JEREMIAH,CHARLES | BISWALO/JEREMIAH,CHARLES | **IST T657 DDF** | **29/07/2019** | TABATA BIMA | KUANZIA SAA 2:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JAGA AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| **3.** | MWAKIMBWALA/ANTONY,LUSEKELO | MWAKIMBWALA/ANTONY,LUSEKELO | **HOUSE** | **04/08/2019** | TABATA | KUANZIA SAA 2:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JAGA AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| **4.** | HAULE/D,DESDELIUS | KELVIN,STEPHEN ,MGADALA | **HOUSE** | **06/08/2019** | MBAGALA | KUANZIA SAA 2:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JAGA AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 5. | SENYAGWA/B,JESSEY | SENYAGWA/B,JESSEY | MOTOVEHICLE T450 CYG & T495 ADM | 29/07/2019 | ITETEMIA | KUANZIA SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | TINCOM COMPANY LTD |
| **6** | NJIU/WILLIAM,ESTHER | NJIU/WILLIAM,ESTHER | COASTER T810ASW | 30/7/2019 | TABATA | KUANZIA SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | WAUNGWANA AUCTION MART |

**MASHARTI YA MNADA**
**Dhamana zitauzwa mahali zilipo**

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (on fall of the hammer), na salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya kipindi cha siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada. Malipo yote yanayohusu nyumba ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.
ii. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.
iii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

**Kwa maelezo na ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na**
**Mratibu wa MIKOPO,**
**AccessBank Tanzania Limited-Makao Makuu**
**S.L.P. 95068,**
**Dar Es Salaam.**
**Simu: 022 2774355, Nukushi: 022 2774340**
**Barua pepe: info@accessbank.co.tz**
**Simu: JAGA AUCTION MART COMPANY LIMITED**
**• 0713123427**

215335902

# Wanafunzi wenye ufadhili nje watahadharishwa

**Na Mary Geofrey**

WANAFUNZI wanaopata ufadhili wa kwenda kusoma nje ya nchi wametakiwa kujiepusha na shughuli za kufanya vibarua katika nchi za watu kwa lengo la kujipatia kipato na badala yake wazingatie kile kilichowapeleka.

Wito huo umetolewa na Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph (SJUIT), Prof. Innocent Ngalinda, wakati akiwaaga wanafunzi watano kati ya 80 wa Stashahada ya Uhandisi wa Sayansi ya Kompyuta, wanaoenda nchini India kwa ajili ya kumalizia mwaka wa mwisho wa masomo yao kwa lengo la kuwaongezea ufanisi katika taaluma hiyo.

Alisema kila mwaka chuo hicho kimekuwa kikiwapeleka wanafunzi wote wa mwaka wa mwisho ngazi ya Stadhahada na Shahada wa Uhandisi wa Sanyasi ya Kompyuta nchini India kwa ajili ya kumalizia masomo yao ili wapate uzoefu wa kuendana na teknolojia ya masomo hayo.

"Nina waasa, chuo kinawapeleka India kwa ajili ya kupata elimu, kuongeza taaluma ili kuwa wahitimu mnaoendana na teknolojia ya Sayansi ya Kompyuta, acheni kwenda kufanya kazi za vibarua, acheni kwenda kufanya uhuni na mambo ambayo hayaendani na kilichowapeleka kazi yenu iwe kusoma na mrejee nchini mkiwa mmepata elimu na si vinginevyo," alisema Prof. Ngalinda.

Alisema kumekuwapo na tabia za vijana wanaokwenda katika nchi mbalimbali duniani kwa ajili ya masomo kujihusisha na vitendo visivyo na maadili na matokeo yake kuharibu mipango yao na malengo tarajiwa.

Vile vile, alisema chuo hicho kinazingatia ubora wa elimu wanayotoa na ndio sababu wamekuwa wakipeleka wanafunzi nje ya nchi ili kuwapatia elimu inayoendana na ukuaji wa teknolojia na kukidhi matakwa ya soko la ajira nchini.

"Gharama za masomo wanayolipia ndizo zinazotumika kuwapeleka India kwa ajili ya kumalizia masomo yao na si kwamba tunawatoza fedha nyingine. Huu ni mkakati wa chuo kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu iliyo bora na wala hakuna haja ya kusafiri kuifata mataifa mengine kwa sababu tunakidhi mahitaji yote," alisema.

Kwa upande wa wanafunzi wanaokwenda nchini India, Sky Karoli, mbali na kuushukuru uongozi wa chuo hicho kwa kuwawezesha kupata uzoefu kutoka chuo cha nchini India alisema ni fursa nzuri kwao.

Alisema wanaamini watapata elimu iliyo bora itakayo wawezesha kuwa wahitimu wanaoweza kutatua changamoto zilizopo ndani ya jamii.

Naye George Temu, alisema wanaenda kujifunza namna nchi nyingine zilivyopiga hatua katika ukuaji wa teknolojia ili kupata elimu itakayowawezesha kuifanyia kazi wakirudi nchini.

Pia, alivitaka vyuo vingine kuiga mfano huo wa kupeleka wanafunzi wake nje ya nchi kwa lengo la kuboresha sekta ya elimu nchini.

# Mpina awashukia anaodai wanataka kumhamisha JPM

**Na Mwandishi Maalum,** SIMIYU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amewashukia baadhi ya watu waliowahi kupewa nyadhifa za juu serikalini na kwenye Chama cha Mapinduzi (CCM) kuendesha mikakati na njama za kutaka kumkwamisha Rais John Magufuli kwenye ajenda kuu ya kuwahudumia wananchi na kutaka taifa lijadili mambo ya watu binafsi.

Mpina ambaye pia ni Mbunge wa Kisesa (CCM) Wilaya ya Meatu Mkoa wa Simiyu, alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wananchi wa jimbo hilo katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Malwilo Kata ya Tindabuligi.

Mpina alisema Watanzania wana imani kubwa na Serikali ya awamu ya tano, na kwamba mikakati na njama hizo kamwe hazitafanikiwa.

Mpina alisema viongozi hao waliwahi kupewa nafasi za juu ndani ya CCM na Serikali, lakini Watanzania walishuhudia usimamizi dhaifu wa shughuli za chama na kusababisha makundi makubwa ya viongozi na wanachama kuhamia vyama vya upinzani na kuisababishia CCM na Serikali kuchukiwa na wananchi.

Mpina alisema baada ya Rais Magufuli kufanikiwa kusuka upya mifumo, kufumua mikataba na sheria mbalimbali na kuongeza udhibiti na usimamizi wa rasilimali za nchi pamoja na kupambana na rushwa kwa vitendo na kukomesha mambo machafu yaliyokuwa yanaumiza wananchi, ndipo wanaibuka watu wachache kutoa waraka na kutaka kuwahamisha wananchi kwenye ajenda kuu ya maendeleo ili wajadili mambo binafsi kwa maslahi yao.

"Walanguzi na wala rushwa waliokuwa wanaiba fedha za taifa hili wamedhibitiwa, mishahara hewa ililipwa miaka nenda rudi viongozi wakawa wanaiba mishahara hewa kana kwamba hakuna mtu

INAENDELEA UK. 8



Mkurugenzi wa Maendeleo wa Kampuni ya TICTS, Donald Talawa, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilela, baada ya kukabidhi msaada wa mifuko ya saruji 1,200 na mabati 1,200, shuleni hapo, wilayani Mlele Mkoa wa Katavi wikiendi, kwa ajili ya ujenzi wa hosteli ya wasichana ambayo itatoa malazi kwa takriban wasichana 200. Wengine ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Rachel Kasanda (wa pili kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mlele, Alexius Kagunze (kulia) na (kushoto) ni Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Deus Bundala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashe akaribishwa na ujumbe mzito

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amemkaribisha Naibu Waziri mpya wa wizara hiyo, Hussein Bashe, kwa kumweleza kwamba jambo la muhimu katika kutekeleza majukumu yake ni kufanya kazi kwa bidii na weledi.

Hasunga alisema hayo jijini Dar es Salaam alipoongoza kikao kazi cha uongozi wa juu wa Wizara ya Kilimo ili kutoa taswira ya mwelekeo wa wizara hiyo.

Kikao hicho kilichofanyika kwa saa kadhaa, kilihudhuriwa na Naibu Mawaziri Omary Mgumba na Hussein Bashe pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara, Mhandisi Mathew Mtigumwe.

Hasunga aliwataka Mgumba na Bashe kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii na ushirikiano ili kutimiza azma ya serikali ya kuimarisha uchumi wa wananchi kadhalika maendeleo kwa ujumla wake.

Alitoa taswira ya mwelekeo wa wizara hiyo katika mipango ya muda mfupi na muda mrefu ili kuwa na weledi na utendaji uliotukuka katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015/2020. Rais John Magufuli alimteua Bashe kuwa Naibu Waziri wa Kilimo kuchukua nafasi ya Innocent Bashungwa ambaye sasa ni Waziri wa Viwanda na Biashara.

Moja ya mambo aliyoyabainisha Hasunga ni pamoja na haja ya kuanzishwa kwa Sheria ya Kilimo itakayotoa suluhisho la changamoto zinazomkabili mkulima na sekta hiyo kwa ujumla.

"Kuna kila sababu ya kuanzishwa haraka sheria ya kilimo na tayari tuko katika hatua za mwisho kwa sababu hatuna sheria na inayotumika sasa ni Sera ya Kilimo iliyotungwa mwaka 2013 ambayo pia inahitaji kupitiwa upya," alisema

Pia alisema sheria zinazotumika kwa sasa ni za bodi za mazao mbalimbali, ambazo pia zina changamoto zake na kuna mazao ambayo hayana bodi kiasi kwamba kuwatetea wakulima wa mazao hayo inakuwa vigumu.

Mazao yaliyo katika utaratibu wa bodi ni pamoja na pamba, kahawa, chai, korosho, pareto na tumbaku kwa upande wa mazao ya biashara, mazao ambayo hayana bodi ni yale ya chakula ambayo nayo yana mchango mkubwa katika uchumi wa taifa.

Kadhalika ameeleza kuhusu usajili wa wakulima wa mazao yote na bodi hizo ziliagizwa kuwapatia vitambulisho kwa ajili ya kuwatambua wakulima hao na wanapofanyika kazi zao ili iwe rahisi kuwahuduma.

Pamoja na mambo mengine, Hasunga alielezea umuhimu wa Wizara ya Kilimo kuanzisha bima ya kilimo kwa wakulima nchini ambao kwa muda mrefu wamekosa utetezi pindi wanapopatwa na majanga kutokana na uchache wa mvua au vinginevyo, jambo linalosababisha kukosekana kwa mazao ya kutosha.

## HABARI KITAIFA



Wafanyakazi wa Kampuni ya Azam Paper Craft International jijini Dar es Salaam, wakiendelea na shughuli za kutengeneza mifuko mbadala ya karatasi kiwandani hapo, katika Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji nchini (EPZA), jijini Dar es Salaam wikiendi, ili kukabiliana na upungufu wa mifuko hiyo, baada ya serikali kupiga marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Hapi awashambulia Makamba, Kinana

**Na Silvanus Kigomba,**
IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, amewashukia viongozi hao wastaafu akihoji uhalali wa waraka wao uliosambazwa hivi karibuni kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Hapi alieleza hayo jana mjini Iringa wakati akizungumza na vyombo vya habari na kueleza kuwa hatua hiyo ya viongozi wastaafu wakiwamo makatibu wakuu wa chama hicho kwa nyakati tofauti Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana, inalenga kukigawa chama hicho.

Aliongeza kuwa kitendo hicho kina lengo mahsusi la kukigawa chama hicho na taifa kwa ujumla, jambo ambalo halipaswi kufumbiwa macho na wana-CCM na Watanzania wanaolitakia mema taifa.

Alisema viongozi hao wastaafu walikuwa na fursa ya kukutana na Rais John Magufuli kueleza duku duku lao, lakini njia waliyoitumia inaonesha lipo jambo ambalo linapikwa ili kumwondoa kwenye mstari Rais kwa kumtisha kwamba chama kimegawanyika na nchi imepasuka.

"Ndugu zangu kustaafu ni heshima, na ukistaafu lazima usemwe. Kama hujasemwa ina maana hukufanya vitu, maana kama usiposemwa wewe uliyewahi kupewa dhamana wakati fulani unataka nani asemwe?" alihoji Hapi.

"Mimi niseme kama kiongozi kijana. Hawa wastaafu wetu wametuangusha sana, tumefedheheka sana wamepoteza heshima yao waliyoijenga kwa miaka mingi."

Aliongeza kuwa Watanzania wanatakiwa kusimama na Rais Magufuli kwani ameonesha kushughulikia madhaifu yaliyoonekana hasa katika kusimamia rasilimali za taifa.

# Reli Tanga- Moshi kuongeza pato kwa mikoa kaskazini

**Na Mwandishi Wetu**

UZINDUZI wa huduma za reli kati ya Tanga na Moshi utaongeza kipato kwa mikoa miwili hiyo, kuchagiza kukua kwa sekta ya ujenzi majumbani na kuifanya Tanga ijitwalie hadhi yake ya zamani enzi zao la katani katika soko la dunia.

"Wakati ule Tanga ulikuwa ni mji maarufu," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Tanga Cement , Reinhardt Swart akizungumzia kuhusu uzuduzi huo uliofanywa na Waziri Mkuu, Kassim Mjaliwa, Jumamosi.

Alisema Kampuni ya Tanga Cement ilikuwa ni mteja wa kwanza wa huduma hizo mpya ambazo zilisita miaka 12 iliyopita, ambapo treni hiyo ilipowasili katika stesheni ya treni ya moshi mjini ikikokota mabehewa yaliyosheheni jumla ya tani 800 kwa mpigo, mzigo ambao ni sawa na ule ambao ungesafirishwa na malori 30.

" Ninaamini usafirishaji kwa urahisi wa bidhaa kati ya vituo hivyo viwili utaongeza kiwango cha watu kuzalisha kipato kwa mikoa yote miwili. Sisi tunahitaji watu wengi zaidi wajipatie pesa mifukoni mwao ambayo itawasaidia kujenga nyumba bora ambazo bila shaka zinahitaji saruji, hivyo tutaongeza mauzo yetu, kuongeza kipato cha wanahisa wetu kupitia gawio, serikali ya Tanzania itavuna kodi ambayo itasaidia katika maendeleo ya nchi," alisema mkurugenzi huyo.

Aliongeza kuwa Tanga ni eneo muhimu la kiuchumi na ina miundombinu yote muhimu ambayo ni bandari, barabara na reli.

Alisema wahusika wakiisimamia miundombinu hiyo vyema na kuitumia ipasavyo, ana uhakika kuwa baada ya

INAENDELEA UK.26

# Bosi wa Benki ya Standard Chartered atunukiwa tuzo

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Global Brand Awards, limemtunuku Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, tuzo ya kiongozi bora katika masuala ya kibenki Tanzania kwa mwaka 2019.

Taarifa iliyotolewa jana na Benki ya Standard Chartered, ilieleza kuwa Rughani ni miongoni mwa washindi wa tuzo hiyo ambayo imekuwa ikiwapatia tuzo kampuni, watu kutoka taasisi mbalimbali ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika taasisi zao.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Rughani alisema: "Ninajisikia furaha kupokea tuzo hii na ninaiwasilisha kwa wafanyakazi wenzangu wa Standard Chartered Tanzania, pia ninaiwasilisha kwa wafanyakazi wenzangu wa sekta ya benki tulio chini ya taasisi za benki, huu ni ushindi wetu na ninawashukuru wote."

Taarifa hiyo ilieleza tuzo hizo ni za saba tangu zilipoanza kutolewa, ambapo kampuni na washindi watakabidhiwa zawadi zao kwenye sherehe maalumu zitakazofanyika mwezi ujao.

Rughani alichaguliwa kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Standard Charteres Tanzania Januari 2016, alianza kufanya kazi katika benki hiyo tangu mwaka 1999 na amewahi kushika nafasi mbalimbali kama vile Mkuu wa Idara ya fedha, Mkurugenzi Mtendaji wa Fedha nchini Ghana.

Pia amewahi kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Fedha Afrika Magharibi katika nchi za Ghana, Gambia, Sierra Leone na Ivory Coast, Mkurugenzi Mtendaji wa Fedha Standard Chartered Tanzania.

Rughani pia amewahi kuwa Mwenyekiti wa Maofisa Watendaji Wakuu Tanzania, Makamu Mwenyekiti wa Taasisi za Benki Tanzania, Mkurugenzi wa Bodi ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Halmashauri zote zifuatiliwe kwa karibu kodi pango ardhi

**KATIKA** toleo letu la jana, tulichapisha habari iliyoeleza kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, ameagiza kupelekwa timu maalum kuchunguza idara ya ardhi katika Manispaa ya Shinyanga mkoani Shinyanga kutokana na idara hiyo kubainika kupunguza kiasi cha fedha kwa baadhi ya wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi katika madeni wanayodaiwa.

Mabula alitoa maagizo hayo wakati akifunga mkutano wa siku tatu wa wataalamu wa sekta ya ardhi jijini Dodoma, na kusema sekta ya ardhi katika Manispaa ya Shinyanga kumekuwapo na mchezo mchafu wa kuwapunguzia wadaiwa sugu kodi ya pango la ardhi kwa kucheza na mfumo, hivyo kuikosesha serikali mapato kupitia sekta hiyo.

Alisema katika Manispaa ya Shinyanga kuna mchezo wa kupunguza madeni kwa mfano, mtu anadaiwa Sh. milioni 20 halafu anapunguziwa deni lake.

Mabula pia alifichua kuwa Manispaa hiyo imekuwa ikiandaa hati nyingi kwa udanganyifu na kusisitiza kuwa timu maalum ya uchunguzi lazima ipelekwe ili kubaini udanganyifu huo kwa kuwa manispaa hiyo imetia aibu na kuondoa uaminifu kwa serikali.

Kadhalika, Mabula alishangazwa na idara ya ardhi katika manispaa hiyo kushindwa kufuatilia hati za madai ilizowapelekea wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi na kusubiri Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya kuwakumbusha, jambo alilolieleza kuwa ni kinyume cha taratibu za utendaji kazi.

Mchezo alioufichua Mabula katika Manispaa ya Shinyanga inawezekana kinafanyika katika manispaa zingine nchini, na ni mchezo unaofanywa na mtandao wa watumishi zaidi ya mmoja, kwa lengo la kujipatia fedha ambazo wanaziweka kwenye mifuko yao binafsi.

Hilo linapaswa kuchukuliwa na serikali kuwa ni funzo na namna ambavyo kila uchao baadhi ya watumishi wanaendelea kubuni njia ya kuiibia serikali, na mwisho wa siku inakosa mapato ya kujiendesha na kutoa huduma kwa jamii.

Kwamba licha ya kuanzishwa kwa mifumo kadhaa ya kudhibiti mapato ya serikali, bado kuna wajanja wanatumia upungufu wa mifumo hiyo kuihujumu serikali kupitia wizi wa fedha za umma.

Kimsingi kodi ya pango la ardhi ni miongoni mwa vyanzo vya mapato mapya ya serikali iliyobuniwa na kusimamiwa kwa karibu na serikali ya sasa, lakini bado ufuatiliaji wa karibu na makini bado unahitajika.

Tunaona kuwa ukiwapo usimamizi makini na wa karibu wa makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kwa halmashauri zetu zote, kwa muda mfupi serikali inaweza kukusanya mapato ya kuridhisha, ambayo yataiwezesha serikali kutekeleza miradi mingine mikubwa inayowagusa sana wananchi.

Ifike mahali sasa wakurugenzi wa halmashauri zetu kila mmoja apangiwe malengo ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi, na hicho kiwe moja ya vigezo vya kupima utendaji wao.

Tusidanganyike kamwe kuwa rasilimali zinazipaswa kuwa tegemeo la serikali kukusanya mapato makubwa kuwa ni mafuta, gesi na madini, bila kuhusisha ardhi.

Taarifa kuwa tangu kuanza kwa operesheni maalum ya kufuatilia wadaiwa sugu wa kodi hiyo, shilingi bilioni 20 zimekusanywa ndani ya mwezi mmoja, ni uthibitisho kuwa upo umuhimu wa kuekeleza nguvu katika makusanyo ya kodi hiyo.

Pamoja na changamoto zilizopo, serikali hainabudi kuhakikisha kuwa mifumo ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi inafuatiliwa kwa karibu na pale inapoonekana ina upungufu, basi ibadilishwe ili taifa lisiendelee kupoteza mapato kwenda katika mifuko ya watu binafsi wachache.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ma-RC, DC, simamieni agizo la serikali ununuzi wa pamba

Na Raphael Kibiriti

**KWA** zaidi ya wiki nne zilizopita, safu hii imekuwa ikibainisha kwa mapana kilio cha wakulima wa pamba, kinachotokana na kusuasua kwa ununuzi wake katika mikoa inayolima zao hilo.

Hali hiyo imesababisha pamba nyingi kuendelea kubaki mikononi mwa wakulima lakini pia katika maghala ya Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS), baada ya baadhi ya wakulima kuipeleka kwa minajili ya kuiuza, lakini wakaishia kukopwa.

Kwamba wakaishia kukopwa baada ya kampuni za ununuzi kutopeleka fedha zikidai bei ya kununulia zao hilo ya Sh. 1,200 kwa kilo iliyowekwa na Serikali, haina faida kwao kutokana na kuporomoka bei katika soko la dunia.

Ni vyema kwamba Serikali hii sikivu ya Dk. John Magufuli iliyojinasibu kwa maneno na vitendo kuwa iko kwa ajili ya Watanzania wote na hasa wanyonge ambao kwa sehemu kubwa ni wakulima imeingilia kati suala hili.

Suala ambalo lilikuwa linaelekea kukatisha tamaa juhudi za wakulima wa pamba za kuongeza uzalishaji, hivyo kipato na hatimaye kuboresha maisha yao na ya taifa kwa ujumla, wakati taifa likielekea kwenye uchumi wa viwanda.

Si kwenye uchumi wa viwanda tu, lakini katika dhima nzima ya kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025, takribani miaka sita ijayo.

Usikivu na utetezi wa serikali kwa wakulima wa zao hili, wengi wakiwa wadogo wadogo umeonekana katika msimamo wake ambapo bila kumumunya maneno imeendelea kusisitiza kwa wanunuzi kwamba bei ya kilo moja ya pamba ni kuanzia Sh.1,200 na si vinginevyo.

Kuna taarifa kwamba wanunuzi wamesuasua kununua zao hili kwa bei hiyo elekezi ya Serikali wakitaka walinunue kwa chini ya Sh. 1,000 ambayo kimsingi haimlipi mkulima ukilinganisha na gharama na nguvu anazoweka kwenye uzalishaji wa zao hilo.

Lakini eneo jingine ambalo Serikali imeonyesha inatembea katika maneno yake linapokuja suala la kupigania maslahi ya wanyonge ni baada ya kulipatia ufumbuzi tatizo la kusuasua kwa masoko ya zao hilo.

Ni baada ya kuwa imefanya mazungumzo na wadau muhimu wa zao hilo na kufikia muafaka katika dhima nzima ya kuhakikisha pamba yote ya wakulima inanunuliwa ifikapo mwishoni mwa mwezi huu na wakulima wanalipwa fedha zao zote.

Hakikisho hili la Serikali lilibainishwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika ziara yake ya kukagua mwenendo wa ununuzi wa zao hilo, aliyoifanya katika kijiji cha Mwabakima wilayani Igunga, mkoani Tabora Julai 15.

Akasema kuwa baada ya mazungumzo, walikubaliana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kuanza kutoa dhamana kwa benki nchini ili zitoe mikopo kwa wanunuzi wa zao hilo na hivyo kuwawezesha kuinunua pamba yote kwa pesa taslimu.

Aidha, akawaonya wanunuzi kutumia pesa watazopata kwa madhumuni lengwa.

Vilevile akawaagiza wakuu wa mikoa na wilaya katika maeneo yote yanayolima zao hilo wasimamie ipasavyo wanunuzi wote ili fedha zinazotolewa zitumike kwa manunuzi ya pamba na si vinginevyo.

Hata hivyo, taarifa ambazo Muungwana amezipata kutoka katika maeneo mbalimbali ni kwamba fedha zimeanza kupelekwa katika baadhi ya maeneo lakini si kwa kiwango cha kutosha.

Kwa hali hiyo bado kuna wakulima wengi waliokuwa tayari wamepeleka pamba yao kwenye maghala ya AMCOS hawajalipwa mpaka sasa, pia bado kuna wakulima wengi walio na pamba yao majumbani, wakisubiri fedha zipelekwe ili waiuze.

Muungwana anatoa rai kwa wakuu wa mikoa na wilaya kuwasimamia wanunuzi wa pamba ambao tayari wamepata mikopo ili kuhakikisha fedha hizo zinafanya kazi iliyokusudiwa ya kununua pamba ya wakulima.

Ni muhimu wafanye hivyo ili kuhakikisha ahadi ya Serikali inatimia kwamba ifikapo Julai 30 pamba yote ya wakulima iwe imenunuliwa kwa ustawi wa wakulima wa zao hilo na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

## MJADALA/BARUA

### Wenzetu hawa wanaikwaza jamii

**Mhariri,**

*UKISOMA vitabu vya dini na hata kusikiliza mahubiri na mawaidha ya viongozi wetu wa dini ni dhahiri utafahamu jinsi ambavyo misahafu na maelekezo ya viongozi hao inavyosisitiza juu ya umuhimu wa kulinda uhai wa binadamu.*

*Inafafanuliwa kwamba uhai wa binadamu ni lazima ulindwe kwa kuwa ndivyo yalivyo maagizo ya Muumba na kwamba hata sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika jamii na makabila zinasisitiza juu ya hilo.*

*Ninaandika katika ukurasa huu kuelezea namna ninavyochukizwa na watu ambao hutupa watoto ovyo jalalani ama kwenye vyoo wakati mwingine na hivyo kukatisha maisha ya watoto wasio na hatia. Tatizo hili kimsingi liko sana kwa wasichana ambao matukio mengi yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara juu yao katika vyombo vya habari.*

*Ninawatahadharisha watu wanaofanya unyama huo wakumbuke kwamba Mwenyezi Mungu anawaona.*

*Ninaomba Serikali yetu tukufu iwachukulie hatua kali watu wa aina hii wasiothamini kabisa uhai wa binadamu.*

**Pawa Nkanda- Majimoto**

### Wavuta sigara hadharani wananikwaza

**Mhariri**

*NAOMBA unipatie nafasi kwenye gazeti letu linalotupatia fursa sisi wasomaji wake ya kueleza dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika jitihada za kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa za kimaendeleo kama watu binafsi na taifa kwa ujumla.*

*Kero niliyonayo kwa leo ni ile ya watu wanaovuta sigara kila mahali hata kwenye sehemu za wazi au za umma ambazo kimsingi haziruhusiwi kwa wavutaji kufanya starehe yao hiyo. Tabia hii inakera katika mazingira yoyote kwa sababu inasumbua wengine wasio wavutaji wa sigara, hali inayowasababishia adha isiyokuwa na sababu, eti tu kwa baadhi ya watu kuendeleza starehe zao.*

*Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa utafiti toka vyanzo mbalimbali vya kiafya, inabainishwa kwamba moshi wa sigara unapomfikia mtu asiyevuta, humuathiri zaidi kiafya kuliko hata huyo mtumiaji mwenyewe.*

**Joseph Baltazari- Shy**

### WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Taasisi zitoe elimu sahihi ya mpigakura, si vinginevyo




**Na Sabato Kasika**

**WAZIRI** Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, amezionya asasi za kiraia zilizopewa jukumu la kutoa elimu ya mpigakura kutokisemea chama chochote cha kisiasa.

Badala yake zinatakiwa kuelekeza wananchi umuhimu wa kujiandikisha, kupiga kura na kuwachagua viongozi wanaowataka na si kuwashawishi ili wampigie kiongozi, ambaye asasi hizo zinamtaka.

Anazitaka asasi hizo kuwaelekeza Watanzania kujua umuhimu wa kujiandikisha, kupigakura na kuwachagua viongozi wanaowataka wenyewe bila kuwapo kwa ushawishi wa aina yoyote.

Hivyo ndivyo alivyoagiza Waziri Mkuu wakati akizindua rasmi uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura akiwa mkoani Kilimanjaro.

Uboreshaji huo unakwenda sambamba na utoaji wa elimu hiyo, ambayo inatolewa na asasi 28 zilizopewa vibali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kutangazwa Juni mwaka huu.

"Tume imetoa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura kwa baadhi ya asasi za kiraia, rai yangu kwa asasi zilizopata vibali hivyo, kuendelea kutoa elimu hiyo kwa wananchi kwa kuzingatia mwongozo," anasema Majaliwa.

Anafafanua kuwa mwongozo umetolewa na NEC, hivyo asasi hizo zisikisemee chama chochote cha kisiasa, bali zielekeze wananchi umuhimu wa kujiandikisha, kupigakura na kuwachagua viongozi wanaowataka wenyewe na siyo kuwashawishi ili wampigie kiongozi ambaye asasi hizo zinamtaka.

Anasema zikifanya hivyo zinakuwa zimejiepusha na ushabiki wa kisiasa na kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa na mwisho wa siku Watanzania watajitokeza kwa wingi kuchagua viongozi wanaowataka.

Anaamini kwamba wananchi wakipata elimu kuhusu uboreshaji wa daftari hilo, watahamasika kutumia haki yao ya kikatiba ya kujiandikisha na hatimaye kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Nikumbushe tu kwamba, siku ambayo asasi hizo zikikabidhiwa jukumu la kutoa elimu ya mpigakura, ziliagizwa kuzingatia mambo muhimu ili kufanikisha kazi hiyo, ikiwamo kufuata sheria, kanuni na taratibu na kutojihusisha na itikadi za kisiasa, udini, ukanda na ukabila.

Hadi sasa zinaendelea kuonywa kutojiingiza katika mijadala ya kisiasa na ushabiki na kutakiwa kufuata miongozo, ambayo zimepewa na NEC, lengo likiwa ni utoaji wa elimu kufanyika kwa ufanisi.

Hivyo kwa kauli ya Waziri Mkuu ambayo inaendelea kusisitiza kile ambacho NEC imekisema, wahusika wasikie na kuzingatia ili uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura ufanyike kama inavyotakiwa.

Asasi hizo zikienda kinyume na hayo, basi zijue kwamba zitakuwa zimechangia kuvuruga maana halisi ya elimu hiyo ya mpigakura inayokusudiwa kuwafikia wananchi.

Kushabikia vyama vya siasa katika utoaji wa elimu ya uraia ni sawa na kufanya kampeni, hivyo asasi zifanye kazi zake na kuwaachia wanasiasa kampeni zao wakati muafaka kufanya hivyo utakapotimia.

Watanzania na hasa vijana waliotimiza umri wa miaka 18 au wale ambao watatimiza umri huo ifikapo Oktoba, 2020 wahamasishwe kujitokeza kwa wingi na kujiandikisha katika daftari hilo.

Hayo ni miongoni mwa yale ambayo Waziri Mkuu amesisitiza na kusema vijana ndio walengwa wakuu kwa vile wanaingia kwa mara ya kwanza katika uchaguzi, hivyo ni muhimu kuyazingatia ili elimu hiyo iwe na matokeo mazuri.

Kama anavyosema Waziri Mkuu, bila kujiandikisha hawataweza kutumia haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wanaowataka, na kwamba kujiandikisha kwao kutawahakikishia ushiriki wao katika uchaguzi wa viongozi.

Walengwa pia wasiwe tayari kusikiliza mambo ambayo yataelezwa yakiwa kinyume na malengo la elimu ya mpigakura, vinginevyo wanaweza kuingizwa katika mtego bila wao kujua.

Watoaji wa elimu ya mpigakura watakaoweka pembeni, sheria, kanuni na taratibu na kujihusisha na itikadi za kisiasa, udini, ukanda na ukabila, waogopwe kama ukoma ili wasilipeleke taifa kubaya.

Ikumbukwe kuwa Watanzania wanaunganishwa na Utanzania wao, siyo kwa itikadi za kisiasa, udini, ukanda na ukabila, hivyo jambo la muhimu ni kuendelea kuwaunganisha kama walivyo.

Vilevile wapo baadhi ya Watanzania ambao hawana dini wala hawako kwenye vyama vya siasa, lakini wote wanaunganishwa na Utanzania wao na siyo ukanda, ukabila, udini wala itikadi za vyama vya siasa.

Kwa maana hiyo watoaji wa elimu, ambao hawatazingatia mwongozo kama wanavyotakiwa, basi waogopwe kama ukoma ili wasilipeleke taifa kubaya, kwani watakuwa wanalenga kuwagawa Watanzania.

Niseme tu kuwa hata wanasiasa nao wanatakiwa kuhakikisha kwamba mambo yote ya kisiasa wanayosimamia, kuyatetea na kuyasifia yanatakiwa kuwakilisha maslahi ya Watanzania wote kwa ujumla.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Maagizo 6 ya JPM kwa Bashe, Simbachawene

INATOKA UK. 2

yanayotakiwa kutekelezwa."

Katika hafla ya kuwaapisha viongozi hao jana, Rais Magufuli alimwagiza Bashe kwenda kutekeleza mambo mawili ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto ya masoko ya mazao ya biashara.

Rais alisema amekuwa akifuatilia michango ya Mbunge huyo wa Nzega Mjini anayoitoa bungeni kuhusu sekta ya kilimo, hivyo kumtaka sasa akaitekeleze wizarani kwa vitendo.

"Nimekuwa nakusikiliza sana bungeni, michango yako ni mizuri, umekuwa ukitoa uchambuzi wa namna ya kuleta mafanikio ya kilimo, ndiyo maana nimekuweka Wizara ya Kilimo," alisema.

"Sekta ya kilimo ina wizi mwingi, ninafahamu changamoto inayoipata Bodi ya Sukari, inapigwa vita sana, nilikuwa nasubiri waziri aivunje na yeye angekipata cha mtema kuni, lakini hajaivunja.

"Nataka nieleze ukweli kwa sababu ile bodi inafanya kazi nzuri lakini inapigwa vita na wafanyabiashara wa sukari waliozoea kutumia sukari kama 'white gold', tumesema hapana kwa sababu 'gape' (pengo) kubwa la sukari tuliyonayo katika nchi ni ndogo, haiwezi ikawa 'exaggerated' (lisikuzwe) tunaletewa sukari ambayo ni ya ovyo, imeshaisha muda wanawaletea wananchi."

Rais Magufuli alimtaka Bashe na watendaji wengine wa Wizara ya Kilimo kuhakikisha wanasimamia mazao ya kilimo ili wananchi wapate soko.

"Kilimo ni biashara, mkulima akilima korosho, mahindi, wapate faida ili kusudi wapate utajiri, kaendeleze kilimo cha kisasa.

"Nina uhakika mkishirikiana na wizara nyingine kama Wizara ya Viwanda na Jeshi la Magereza ambao bado kilimo hakijaleta matokeo, mnaweza kuleta matumaini makubwa kwa wananchi," alisema. "Sasa hivi kuna changamoto kule Kagera, tuliwaambia wauze kahawa, wawekezaji wanaotaka kununua waje, lakini ni lazima wanunue kwa Sh. 1,500 na kuendelea kwa sababu ipo michango inatakiwa kulipwa kwenye halmashauri na serikali.

"Wafanyabiashara wachache wameanza kuwadanganya wananchi. Fedha zimeshapelekwa za kulipia kahawa. Wafanyabiashara wa namna hii ambao wanawadanganya wananchi wasiziuze kuwa hao watazinunua, lazima washughulikiwe kwa mkono mkubwa bila kuwaonea huruma." Alisema changamoto za aina hiyo zipo pia kwenye zao la pamba ambalo serikali imeagiza kilo moja inatakiwa iuzwe kuanzia Sh. 1,200.

"Nitoe wito ingawa nilishazungumza, wafanyabiashara wakinunua pamba na kuwakopesha, mkampata mtu mwingine anayetaka kuwalipa, iuzeni hiyo pamba ili mpate fedha zenu ili wananchi msibaki kukopesha kwa wafanyabiashara.

"Ninawapongeza, nawatakia kazi njema, mkamtangulize Mungu, mtapigwa vita, mtazungumzwa, mengine myavumilie, mmwachie Mungu kwa sababu ndiye aliyetaka muwe katika nafasi zenu, kashirikianeni na wanyonge, nina uhakika mtafanya makubwa," alisema.

Awali, Simbachawene alisema amekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa muda na ameona fedha nyingi zinatengwa, lakini hazitatui matatizo kwenye mazingira.

"Nitashirikiana na kumshauri Makamu wa Rais na wenzangu watanisaidia ili Muungano wetu uweze kudumu kwa sababu hatuna chaguo lingine la nchi nyingine mpya itakayotokea zaidi ya Muungano wa Zanzibar na Tanganyika," alisema.

Naye Bashe alimwahidi Rais Magufuli kuwa atatimiza yale ambayo yako ndani ya mamlaka aliyopewa ili kusukuma gurudumu la maendeleo.

"Ninaifahamu sekta ya kilimo, ninamshukuru Spika (Job Ndugai) alinipa nafasi ya kukaa kwenye Kamati ya Bajeti, namshukuru Simbachawene, kaka yangu amekuwa mwenyekiti wangu katika kamati hiyo, imenipa elimu ya kufahamu changamoto zinazoikabili nchi hii," alisema.

**WAFUGAJI**

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli alitangaza jana kuwa amepanga kukutana na wafugaji wa Tanzania ili kuzungumza nao kama alivyofanya kwenye makundi mengine yakiwamo ya wadau wa sekta ya madini na wafanyabiashara.

"Hatuwezi kuzidharau changamoto zao hasa katika kushughulikia maeneo ya kuchungia mifugo yao kwa sababu ng'ombe wapo wengi, mpaka sasa takwimu zinaonyesha wapo milioni 5.5," alisema.

# Mahakama yaelezwa mshtakiwa alikiri kumpiga mjukuu

INATOKA UK. 2

kwamba walifanyiwa ukatili wa hali ya juu tofauti ni kwamba huyu mzima na yule amefariki, nilimpigia simu afande Walelo akaniamuru nirudi kituoni na huyo mtoto," alidai Sajenti Mgeni huku akitokwa na machozi kuonyesha uchungu wa ukatili wa mshtakiwa.

Alidai kuwa alimhoji jirani yake mshtakiwa Mwanahamisi kuhusu mahusiano yake na mshtakiwa, alidai kuwa alimweleza jinsi alivyokuwa akiwapiga Andrew na marehemu mara kwa mara.

Alidai kuwa alishuhudia jinsi Naomi (marehemu kwa sasa) alivyotumikishwa kazi za watu wakubwa tofauti na umri wake.

Vile vile, alidai kuwa Mwanahamisi alijaribu kumsihi asiwapige, lakini aliambulia kununiwa, alipomsalimia hakuitikia na ikawa hawana uhusiano wa ujirani tena.

Pia alidai alipomfikisha Andrew kituoni bosi wake alipomwona, aliagiza apelekwe hospitali na alilazwa.

"Machi 28, 2017 niliungana na jopo la madaktari kufanya uchunguzi kwa kweli hali ya mwili wa marehemu ilisikitisha, alikuwa na uvimbe mkubwa kichwani walipomfunua walibaini damu ilivilia kwenye ubongo, vidonda mwili mzima vilivyokosa matibabu na mkono wa kulia ulikuwa umevunjika," alidai shahidi huku akitokwa machozi.

Kadhalika alidai kuwa alipiga picha kama ilivyo taratibu na kuziwasilisha kwa wakuu wake.

Mahakama hiyo ilipokea ramani ya eneo la tukio na picha tisa za marehemu kama vielelezo katika kesi hiyo.

Shahidi mwingine kutoka Dawati la Jinsia Polisi, Chang'ombe Koplo Joyce, alidai kuwa siku ya tukio alipigiwa simu na Dk. Ruth anayehusika na ustawi wa jamii Hospitali ya Temeke niende kuna tukio.

Alidai kuwa alikwenda kitengo cha dharura akafahamishwa kwamba wamepokea mtoto, lakini mshtakiwa na wenzake wanadai ni mgonjwa wakati tayari ameshafariki.

"Nilivyomuona mtoto alionekana amepata mateso na ukatili mkubwa kabla ya kufa kwake, niliwachukua watuhumiwa, mshtakiwa na wanawe nikawapeleka kituoni na baadaye nilikwenda kuwakabidhi polisi Mbagala eneo lilikofanyika tukio," alidai Koplo Joyce.

Kesi hiyo inaendelea leo ushahidi wa Jamhuri.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Machi 25, 2017 Tuangoma Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam mshtakiwa alimuua mjukuu wake kwa kumpiga.

# Mpina awashukia anaodai wanataka kumhamisha JPM

INATOKA UK. 4

aliyetakiwa kuchukua hatua... leo Mheshimiwa John Magufuli amekuja, mishahara hewa yote imekuwa historia," alisema Mpina.

Pia alisema Rais Magufuli amerekebisha mifumo kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo sekta ya madini, hali iliyowezesha Serikali kuwa na hisa kwenye migodi hiyo, ambapo sasa Serikali inapata mabilioni ya fedha kutoka kwenye madini, rasilimali zetu zilikuwa zinaibwa kana kwamba hakuwapo mtu wa kuchukua hatua.

"Uvuvi haramu kila kona, samaki walikuwa hakuna Taifa lenye maziwa makubwa kuliko nchi yoyote Afrika na Dunia, Taifa lenye bahari samaki tunanunua za kutoka nje," alisema na kuongeza:

"Mheshimiwa Magufuli akasema uvuvi haramu hapana, Mpina nenda pale kakomeshe uvuvi haramu, uvuvi haramu umekoma nchi hii, wananchi wanakula samaki wengi na wakubwa kila sehemu na mauzo ya nje yameongeka."

Mpina alisema mambo mengine makubwa yaliyosimamiwa na Rais Magufuli kudhibiti utoroshaji fedha nje ya nchi, biashara ya dawa za kulevya, matumizi ya pombe za viroba, utoroshaji magogo nje ya nchi, uingizaji holela wa bidhaa toka nje na kuua viwanda vya ndani. Pia mikopo ya serikali, matumizi holela ya fedha za umma yote yameshughulikiwa na Serikali ya awamu ya tano.

"Sasa wengine wanaanza kujitokeza na mawaraka yao wataendelea kuyasoma wenyewe, Watanzania wako bize na maendeleo hawahitaji waraka hatuhitaji waraka sisi, tunahitaji umeme wa uhakika, sisi tunahitaji elimu bora na maji, sisi tunahitaji soko na bei nzuri ya pamba, sisi tunahitaji malisho ya mifugo, sisi tunahitaji usafirishaji wa uhakika treni, ndege, barabara, madaraja na viwanda.

Sisi tunahitaji hospitali nzuri, tunahitaji dhuluma zote dhidi ya wananchi zikomeshwe, mambo hayo Magufuli amekuwa akishughulikia nayo kufa na kupona.. sisi hatuhitaji waraka...waraka wakasome wao na familia zao."

Alisema mageuzi makubwa aliyoyafanya Rais Magufuli katika kipindi kifupi cha uongozi wake Tanzania haitamsahau na wanaCCM hawatamsahau kwa juhudi kubwa alizofanya za kuweka mifumo imara ndani ya Serikali na CCM.

"Kama ni kwenye chama nani katika historia ya nchi yetu aliyeweza kufanya kama Mheshimiwa Magufuli, nani katika utawala ambaye ameweza kurudisha wabunge 10, madiwani 200 na halmashauri nne kutoka upinzani na kujiunga na CCM?" alihoji.

# Mazungumzo kina Nape, Makamba yaibua jambo

INATOKA UK. 2

Alitahadharisha kuwa kuwapo kwa vitendo hivyo kunahatarisha usalama wa raia na uhusiano na mataifa mengine, akidai kuwa kama viongozi wanaweza kudukuliwa mawasiliano yao binafsi, inawezekana hata mabalozi na watu binafsi wakafanyiwa vitendo hivyo.

"TCRA itoe taarifa sahihi juu ya nani aliyefanya kazi hiyo, kama Kinana na Nape wamerekodiwa, nani ana uhakika kama Balozi wa Marekani hajarekodiwa, Balozi wa Uingereza hajarekodiwa?

"Viongozi wetu wa vyombo vikubwa hawajarekodiwa? Kama wamerekodiana wenyewe kwa wenyewe, sisi vipi, wengine vipi? Tuache huu utamaduni," Kubenea alisema.

Mbunge huyo alisema vitendo hivyo vikiendelea kufumbiwa macho, vitahatarisha kufungiwa kwa TCRA na Mamlaka ya Mawasiliano ya Kimataifa kutokana na kushindwa kutimiza wajibu wake.

"Nitakuwa mtu wa mwisho kuunga mkono suala hili linaloweza kuligawa taifa kwa sababu za tofauti za kisiasa. Minyukano ndani ya vyama ipo, kusemana kupo, kuteta kupo.

"Na hata mimi nakumbuka sauti niliyokuwa nikizungumza na rafiki yangu Antony Komu (Mbunge wa Moshi Vijijini), iliwahi kusambaa kwenye mtandao, lakini tuliyamaliza ndani ya chama kwa kukiri na kuomba radhi," Kubenea alisema.

Mazungumzo yaliyorekodiwa yenye sauti zinazodaiwa za kina Nape, Kinana na Makamba, yalianza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii baada ya Kinana na Makamba kwa pamoja kumwandikia barua Katibu wa Baraza la Ushauri la Viongozi Wakuu wastaafu wa CCM, Pius Msekwa, wakilalamika kudhalilishwa na mtu anayejiita mwanaharakati huru.

Nipashe jana ilimtafuta Msemaji wa TCRA, Semu Mwakyanjala, kuzungumzia changamoto ya udukuzi wa mazungumzo hayo ya simu, lakini akasisitiza kuwa suala hilo ni la kijinai, hivyo linapaswa kushughulikiwa na kutolewa ufafanuzi na vyombo vya dola.

"Uhalifu wowote au jinai yoyote ile ni Jeshi la Polisi ndilo limepewa mamlaka ya kisheria kusimamia suala hilo kwa kuchunguza na kukamata.

"Mtu akifanyiwa uhalifu anaenda polisi kuripoti na si TCRA na mtu akifanya uhalifu mtandaoni, polisi ndiyo wenye jukumu la kufuatilia," Mwakyanjala alisema.

Nipashe pia ilimtafuta Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz, kuzungumzia suala hilo, lakini akasema yuko kikaoni na kumwomba mwandishi amtafute baadaye.

Baadaye DCI Boaz alimpigia simu mwandishi na kumtaka aende ofisini kwake leo kwa ajili ya ufafanuzi wa suala hilo kwa maelezo kuwa jana hakuwa na uhakika kama kweli alikuwa anazungumza na mwandishi wa habari.

# Takukuru ilivyookoa bil. 4.5/- kwenye uchakachuaji

**Na Christina Haule,** MOROGORO

ZAIDI ya Sh. bilioni 4.5 zimeokolewa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), baada ya kunusurika kufujwa kwa njia tofauti kwenye miradi minne ya maendeleo iliyokusudiwa kuboresha huduma mbalimbali za kijamii mkoani hapa.

Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Morogoro, Janeth Machulya, alisema katika kipindi cha robo ya mwaka yaani Aprili hadi Juni Takukuru imetekeleza kazi yake ambapo fedha hizo shilingi 4,545,987,652.06 zilifujwa kwenye mradi wa Hospitali ya Wilaya Morogoro, ukarabati wa Shule ya Sekondari Morogoro, Shule ya Sekondari Mjimpya na mradi wa maji Dihinda wilayani Mvomero.

Kamanda huyo alisema ufujwaji wa fedha hizo umetokana na ukiukwaji mkubwa wa taratibu za manunuzi na mikataba, kufanyika malipo bila taratibu, fedha nyingi kutumika pasipo kazi kuonekana, kazi duni na makandarasi kutekeleza miradi kinyume cha taratibu au matakwa ya mkataba. Aidha, Machulya alifafanua kuwa Hospitali ya Wilaya Morogoro ilitengewa Sh. 1,500,000,000, Shule ya Sekondari Morogoro Sh. 1,042,554,532.80, Shule ya Sekondari Mjimpya Sh. 1,400,000,000 na mradi wa maji Dihinda ulikuwa wa Sh. 603,433,119.29.

Hata hivyo Machulya alisema Takukuru inaendelea na uchunguzi zaidi kuhusiana na ufujaji huo licha ya kwamba katika hatua za awali wapo viongozi kadhaa waliosimamishwa kazi kwa kumjibu wa kanuni na taratibu za sehemu zao za kazi.

Pia alisema, kufuatia uchunguzi uliofanywa kwenye sekta kadhaa katika kipindi hicho taarifa 128 zilipokelewa kwa njia mbalimbali ikiwamo simu taarifa 42 na 86 kupitia njia mbalimbali zikiwamo barua, watu kufika ofisini.

"Kwa taarifa zote hizi serikali za mitaa wanaongoza kwa kulalamikiwa, malalamiko 44 yaliwahusu, Mahakama 16, mabaraza ya migogoro kwenye kata 15, Polisi 13, ardhi 9, utawala 6, vyama vya ushirika sita, elimu 5, afya 5, fedha 4, maji 3, na Tanesco 2, " alisema Machulya.




Afande Julius Linje akichangia damu katika kituo cha uchangiaji Ukonga jijini Dar es Salaam. Anayempatia huduma hiyo ni Rosemary Bulemeo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# AAR, Damu Salama wachangia damu, kutoa huduma za afya bure

**Na Enock Charles**

KAMPUNI ya Bima ya AAR na Taasisi ya Damu Salama zimeshirikiana kuchangia damu katika eneo la Ukonga jijini Dar es Salaam.

Shughuli hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki ambapo taasisi hizo ni wadau muhimu wa sekta ya afya nchini pia zilitoa huduma ya kupima afya za wakaazi wa eneo hilo bure na kutoa huduma nyingine za kitabibu ikiwa ni pamoja na ushauri wa kitaalamu kuhusu afya.

Akizungumza na waandishi wa habari muda mfupi baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, Meneja wa Maendeleo ya Biashara wa Kampuni ya Bima ya AAR, Hamida Rashid, alisema kuwa hatua hiyo ni sehemu ya utamaduni wa taasisi hizo wa kujali afya ya jamii na kushiriki kwa vitendo kuboresha na kulinda maisha ya jamii.

"Tunaendeleza utamaduni wetu wa kujali ustawi wa jamii kwa sababu uwepo wetu unatokana na jamii inayotuzunguka. Hivyo, kama wadau muhimu wa sekta ya afya, tumeamua kushiriki kwa vitendo kuchangia damu ili kusaidia kuokoa maisha ya jamii yenye uhitaji," alisema Hamida. "Tunafahamu kuna uhitaji mkubwa wa damu salama nchini na ni jukumu letu kama kampuni ya Bima kushirikiana na wadau wenzetu, Damu Salama kushiriki kwa vitendo katika upatikanaji wa damu," aliongeza.

Aidha, Hamida alisema kuwa taasisi hizo zimetoa huduma nyingine za afya ikiwa ni pamoja na ushauri wa kitabibu kwa wakazi wa Mombasa-Ukonga kwani wanaamini kuwa jamii inapaswa kupata elimu ya kutosha ya jinsi ya kujikinga na magonjwa na kuimarisha afya zao ili kupunguza idadi ya watu wanaosumbuliwa na magonjwa yatokanayo na kutozingatia au kutofahamu masuala ya msingi ya kuimarisha afya zao.

Kwa upande wake, mtaalamu mwelekezi wa uchangiaji damu kutoka Damu Salama, Mariam Juma, alisema kuwa pamoja na kuchangia damu, taasisi hizo zimetumia fursa hiyo kutoa elimu kwa umma kuhusu namna bora ya kuimarisha afya zao, faida ya kuchangia damu na kuhuisha usalama wa damu ili kuongeza upatikanaji wa damu salama. Lister Gilbert, mkazi wa eneo la Mombasa, Ukonga ambaye ni mmoja kati ya walioshiriki zoezi la kuchangia damu, alizipongeza taasisi hizo kwa jinsi zilivyoendesha zoezi hilo kwa kutoa elimu iliyomwongezea sababu zaidi za kuchangia damu.

Mwishoni mwa Juni, 2019, Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS) ilieleza kuwa kwa mwaka jana Tanzania ilikuwa na upungufu wa damu kwa asilimia 42, ikieleza kuwa kupitia zoezi la uchangiaji damu nchini, kiasi cha chupa 307,835 kilipatikana ambacho ni sawa na asilimia 58 ya mahitaji. Kwa mujibu wa NBTS, ili kukidhi mahitaji ya kila mwaka, taasisi hiyo inapaswa kukusanya chupa 526,000.

# Sababu kupungua ujangili wa tembo Hifadhi ya Ruaha

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

KAMISHNA Mwandamizi wa Kanda ya Kusini, Dk. Christopher Timbuka, amesema vitendo vya ujangili wa tembo katika Hifadhi ya Ruaha vimedhibitiwa kutokana na mikakati mbalimbali kwa kushirikiana na wadau ikiwamo uanzishwa wa Jeshi Usu.

Alisema kubadili kwa mfumo wa utendaji kazi kutoka ule wa kiraia na kuwa Jeshi Usu kumeweza kupunguza tatizo sugu la ujangili wa wanyamapori hasa tembo.

Dk. Timbuka alisema hivi karibuni Wizara ya Maliasili na Utalii iliridhia maombi ya Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) kubadili mfumo wa utendaji kazi kutoka wa kiraia na kuwa Jeshi Usu ili kukabiliana na tatizo sugu la ujangili wa wanyamapori, misitu, na rasilimali nyingine za nchi.

Alisema kuwa muundo mpya unahusisha Kanda ya Kaskazini yenye hifadhi za Arusha, Tarangire, Ziwa Manyara, Kilimanjaro na Mkomazi, Kanda ya Mashariki inayojumuisha Hifadhi za Saadan, Mikumi na Udzungwa, Hifadhi za Ruaha na Kitulo na Katavi zitakuwa chini ya usimamizi wa Kanda ya Kusini.

Dk. Christopher aliwapongeze maofisa na askari waliovishwa vyeo vya kijeshi hivyo na kusema kuwa vyeo hiyo sio mapambo ila ni vya kiuhifadhi kwa ajili ya rasilimali za hifadhi za taifa.

Kanda ya Magharibi itasimamia Hifadhi za Taifa za Gombe, Mahale, kisiwa cha Saanane, Kisiwa cha Rubondo, Serengeti pamoja na Hifadhi mpya za Burigi, Kimisi, Biharamulo, Ibanda na Rumanyika.

Alifafanua kuwa lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwawezesha wahitimu kufanya kazi kwa mfumo wa Jeshi-Usu katika kuboresha utendaji kazi na majukumu ya Dk. Timbuka alifafanua kuwa kuwapo kwa mfumo wa jeshi hilo kumeboresha usimamizi na thabiti wa maliasili zilizopo hifadhini kwa kuwajengea maofisa na askari uwezo wa kimwili, kisaikolojia, kimaadili na uzalendo.

Katika hatua nyingine, Dk. Timbuka aliendesha zoezi la uvishwaji vyeo kwa maofisa wahifadhi na askari wasio wahifadhi limefanyika katika Uwanja wa Msembe, Hifadhi ya Ruaha (RUNAPA) na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, wilayani Iringa mkoani Iringa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, ametoa rai kwa maofisa na askari wa Jeshi Usu la Uhifadhi la Tanapa kwa kufanya kazi kwa weledi na nidhamu kwa kuzingatia kiapo cha utii walichokula ili kulinda rasilimali.

# Serikali yamkuna Waziri Mkuchika jimboni

**Na Hamisi Nasiri,** NEWALA

MBUNGE wa Newala Mjini, George Mkuchika, ambaye pia ni Waziri Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora), ameipongeza serikali kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye jimbo lake ikiwamo ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo iliyojengwa Kata ya Mkunya. Mkuchika alitoa pongeza hizo mwishoni mwa wiki mjini Newala alipokuwa akizungumza na wananchi wa kata hiyo ikiwa sehemu ya ziara yake ya kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wananchi wa jimbo hilo.

Alisema serikali imesikiliza kilio na kero mbalimbali za wananchi wa jimbo hilo kwa kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo imeanza kuleta manufaa kwa wananchi.

"Nikiwa mbunge mara kwa mara nimekuwa nikiiomba serikali kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye jimbo langu, nashukuru imesikia naona miradi mingi inatekelezwa kwa nguvu zote, naipongeza serikali kwa hili," alisema Mkuchika. Mkuchika alisema amefurahishwa na kitendo cha serikali kwa kutekeleza ujenzi wa jengo la mahakama ya mwanzo, na kwamba tayari limeshafikia hatua ya kukamilika na muda wowote kuanzia sasa litaanza kutoa huduma za kimahakama. Alisema wananchi wa Kata ya Mkunya moja ya kilio chao kikubwa ilikuwa ni kupatiwa mahakama ili kuwawezesha kusikilizwa kwa madai yao na tayari serikali imeshasikiliza kilio hicho, na kuamua kujenga mahakama hiyo na kwamba kazi ya serikali iliyobaki ni kuharakisha kupeleka wafanyakazi ikiwamo hakimu.

Alisema wananchi wa Jimbo la Newala Mjini, na hasa Kata ya Mkunya wamekuwa na kero kadhaa za kijamii, afya, maji, barabara na miundombinu mbalimbali, hivyo mara kwa mara wamekuwa wakimweleza mbunge huyo kuwatatulia, lakini sasa baadhi ya huduma wameshaanza kuzipata wakiwa kwenye kata yao.

# Marufuku mgodi North Mara kutumia bwawa la tope sumu

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

BARAZA la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC) limesitisha matumizi ya bwawa la kuhifadhia tope sumu katika Mgodi wa Acacia North Mara baada ya sampuli mbalimbali za vipimo kuonyesha kuwa bado kuna utiririshaji wa maji yenye kemikali sumu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea bwawa hilo lililopo eneo la Nyamongo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Mhandisi Dk. Samuel Gwamaka, amesema kampuni imeshindwa kudhibiti utiririshaji wa maji hayo yenye kemikali za sumu zinazototililika kuelekea katika makazi ya wananchi na kuathiri mazingira pia. "Kama NEMC tumesimamisha matumizi ya bwala la tope sumu mpaka pale watakapoweza kudhibiti utiririshaji wa maji yake au kujenga bwawa jingine jipya ambalo litaweza kudhibiti utiririshaji maji ya kemikali za sumu na kuathiri mazingira na afya za wananchi," alisema Dk. Gwamaka.

Akiwa ameambatana na maofisa waandamizi kutoka Tume ya Madini, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na pia Baraza, Dk. Gwamaka amesema NEMC haitamwonea aibu wala huruma mtu au kampuni yoyote inayofanya shughuli zake bila kufuata kanuni na taratibu za kimazingira.

"Mfano Bwawa la kuhifadhia tope sumu, Septemba 2018, Februari, Machi, Mei na Juni mwaka huu mwaka huu wataalamu walichukua sampuli katika bwawa hilo na zote zilibaini kuwapo na kemikali zenye sumu," alisisitiza.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serilikali, Boniventure Masambu, alisema sampuli zote zililizochukuliwa kwa nyakati tofauti na kufanyiwa uchunguzi zimeonyesha kuwapo kwa kemili na hivyo kutoa ushauri.

"Tumefurahi kuona ushauri wetu umefanyiwa kazi mara moja na mamlaka uhusika," Masambu alisema na kuongeza afya za wananchi na utunzaji wa mazingira ni muhimu kwa mustakabali wa taifa.

Naye Kaimu Meneja wa Acacia, Reuben Ngusaro, aliahidi kufanyia kazi maelekezo yaliyotolewa ilikuweza kukabiliana na athari zote za kimazingira zinazotoka na tope sumu. "Tutayafanyia kazi maagizo yote kwani tunathamini afya ya wananchi na mazingira. Yote tuliyoyakuta tutayarekebisha," alisema.



Mkurugenzi wa Masoko wa Benki ya TPB, Deo Kwiyukwa (kulia), akikabidhi msaada wa ndoo 50 za rangi kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga (SHIRECU), Richard Luende, kwa ajili ya upakaji rangi katika majengo ya Shule ya Sekondari Buluba Shinyanga Mjini. Halfa hiyo fupi ilifanyika katika shule hiyo mkoani Shinyanga mwishoni mwa wiki. **MPICHA PICHA WETU**

# Wafanyabiashara waliopewa leseni, vyeti TBS wafundwa

**Na Zuwena Shame**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limewataka wafanyabiashara waliotunukiwa vyeti na leseni za biashara kutumia fursa hiyo kwa kuongezea uzalishaji zaidi wa bidhaa sokoni na kuwa chachu ya mendeleo ya biashara zao na uchumi kwa ujumla.

Aidha, baada ya kutunukiwa vyeti na leseni za ubora, bidhaa za wafanyabiashara hao zitatambulika kitaifa na kimataifa kwa kuweka nembo ya TBS ambayo huashiria ubora na usalama wa bidhaa husika.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa TBS, Lazaro Msasalaga, wakati wa kuwatunuku vyeti na leseni 113 kwa wafanyabiashara nchini.

Msasalaga alisema itakuwa ni aibu kubwa iwapo mfanyabiashara ataacha kuzingatia matakwa ya ubora baada ya kutumia cheti na leseni na kujiingiza kwenye hatari ya kunyang'anywa leseni au cheti au hata bidhaa yake kuharibiwa na kutozwa faini ama kuondolewa sokoni. "Hii ni hasara kubwa ambayo manejimenti ya TBS isingependa kuona inatokea," alisema Msasalaga.


Alisema TBS ina jukumu kubwa la kusimamia na kuandaa viwango vya kitaifa ili kuhakikisha kwamba maslahi ya nchi yanazingatiwa kitaifa, kikanda na kimataifa.

Aliongeza kuwa pamoja na kuandaa viwango, TBS inasimamia utekelezaji wa viwango ili kulinda afya na usalama wa walaji, kuongezea pato la taifa sambamba na ukuaji uchumi wa viwanda.

Alisema kuwa hadi sasa wajasiriamali 300 nchini wameshapata leseni na kutumia alama ya ubora ya TBS na kuzitumia kwenye bidhaa zao, hivyo kuzifanya kupenya kwenye masoko mbalimbali yakiwamo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Haya ni mafanikio makubwa kwa taifa katika malengo yetu ya taifa ifikapo 2025 tuwe tumejenga uchumi wenye nguvu, imara na ushindani," aliongeza Msasalaga.

Aliwataka wafanyabiashara ambao vyeti vyao vimekwisha muda wake kwenda ofisi za karibu za shirika hilo ili wapewe barua ya kielelezo kwa ajili ya kutumia kipindi cha mpito hadi leseni na vyeti vyao vitakapokuwa tayari.



# Mbunge atuliza wananchi sakata la uchomwaji makazi

Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

MBUNGE wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, amewaomba wananchi zaidi ya 300 wa jamii ya Barabaig na Maasai wa vijiji vya Vilima Vitatu na Mijingu wilayani Babati kuwa watulivu na kuepuka kuleta vurugu katika kipindi hiki cha uchomwaji wa nyumba zao.

Akitoa ombi hilo jana wilayani humo, wakati akiongea na wafugaji hao katika semina ya siku mbili iliyoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Mtandao wa Wafugaji na Wawindaji wa asili (Pingo's Forum), kwa ajili ya kuelimisha umuhimu wa kutafuta haki zao kupitia vyombo husika, Millya alisema katika kipindi hiki walichonacho cha kukosa makazi ni vema wakawa watulivu na kumwachia Mungu na serikali.

Alisema anaamini wakazi 34 kati ya hao waliochomewa moto maboma yao Julai 7, 8 na 9, mwaka huu kwa madai ya kujenga katika mapito ya wanyama kuelekea Ziwa Manyara, wakitulia na kuiachia serikali lazima viongozi watatoa ufumbuzi wa tatizo hilo.

"Mimi nawaomba mtulie na mwachieni Mungu na Rais wetu sababu msikivu na anawapenda sana wafugaji na watu wote, hili suala atalishughulikia tu, msifanye fujo ya aina yoyote," alisema.

Millya aliomba viongozi wa ngazi zote kuanzia ya vitongoji hadi taifa kuchunguza tukio hilo kwa makini ili wananchi hao wapate haki yao ya kuishi kwa amani katika makazi yao kama wananchi wengine nchini wanavyoishi.

Alisema jamii hizo huishi vizuri na wanyama kutokana na kutokula nyama zao, hivyo wamekuwa marafiki wazuri wa mazingira.

Vile vile, alisema wanyama ni rasilimali muhimu nchini kwa kuwa ikitunzwa na kulindwa inasaidia kuchangia uchumi wa nchi na kubadilisha hali ya taifa kwa kujengwa vituo vya afya, barabara nzuri na kuboresha sekta mbalimbali. Naye Mwenyekiti wa Wafugaji Wilaya ya Babati, Lomnyaki Ngoiseye, alimwomba mbunge huyo kupeleka kilio chao katika kamati ya kutetea wafugaji cha kunyanyasika kila mara kwa kuchomewa makazi yao na kuwafanya wakose uhuru wa kuishi vema katika nchi yao.

Kwa upande wa waathirika wa tukio hilo, mfugaji mmoja na mwindaji ambao hawakutaka majina yao kutajwa, walisema tangu makazi yao yachomwe moto Julai 7, mwaka huu, wamelazimika kulala chini ya miti na kuhatarisha maisha yao kutokana na wanyama wakali kupita katika maeneo hayo na kupigwa na baridi kali.

Waliomba serikali isikie kilio chao na ikiwezekana viongozi watembelee kijiji chao ili wakajionee hali halisi na kuzungumza nao.

Wafugaji, wawindaji na wavuvi waliochomewa makazi yao walisema walikuwapo kabla ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961.



Mratibu na msimamizi wa mradi wa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovolti 400, kutoka Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), Mhandisi Peter Kigadye, akimfafanulia jambo Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Mhandisi Innocent Luoga, alipotembelea na kukagua ujenzi wa Lot T1 iliyopo Nangwa, wilayani Babati mkoani Manyara jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Waomba kupatiwa elimu vifungashio

Na Mary Mosha, BABATI

WAKULIMA wa Kijiji cha Magugu, Kata ya Magugu Wilaya ya Babati, mkoani Manyara wamekiri kutumia vifungashio vya viuatilifu na kuiangukia serikali kupitia Taasisi ya Ukaguzi na Uthibiti wa Viuatilifu nchini (TPRI) kuendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kupunguza madhara yatokanayo na vifungashio hivyo.

Amosi Sadani, alisema elimu iliyotolewa ni ndogo pia wamechelewa kuipata hali inayosababisha baadhi yao kupata magonjwa mbalimbali yakiwamo ya saratani, huku wengine wakiamini ni ushirikina kutokana na ongezeko la vifo vya wakulima na jamii zao.

"Tumekuwa tukiamini wakulima wenzetu wanatumia ushirikina, ili kupoteza maisha ya wengine baada ya kulima mashamba makubwa kumbe ni madhara ya kuwapo ongezeko la matumizi ya viuatilifu mashambani, huku vifungashio vikiwa havisafishwi ipasavyo kwa kuwa baadhi yetu wanasafisha kwa maji ya moto," alisema Sadani na kuongeza:

"Tumeteseka vya kutosha, tunajuta kuikosa elimu hii muda mrefu na tunaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuitoa nchi nzima kwa kuwa kuna baadhi ya wakulima nchini wanatumia vifungashio vya viuatilifu hasa vya plastiki wakitumia kwa kufungashia vitu mbalimbali ikiwamo mafuta," alisema Martha Mchimbi. Prisca Saidi, aliiomba serikali kupitia watafiti wanaotoa elimu, lakini pia kuangalia namna ya kupata viuatilifu ambavyo havina athari kwa wakulima ili kupunguza madhara kwa jamii inayowazunguka wakulima.

"Pamoja na kuwa tumepata elimu ya usafishaji wa vifungashio vya viuatilifu pia wauzaji na wasambazaji wa viuatilifu wapewe mafunzo ili kuwasaidia wakulima elimu mara wanapofika kwa ajili ya manunuzi ya viuatilifu," alisema Prisca.

Kwa upande wake Ofisa Kilimo wa Kata, Mary Temu, alikiri kupokea elimu iliyotolewa na TPRI na kusema kuwa udongo wa magugu haufai kuotesha kitu chochote bila kuuchanganya na viuatilifu hali ambayo inawalazimu wakulima kuvitumia zaidi.

Alisema kutokana na madhara yaliyoelezwa hapo, inaonyesha kuwa magugu ni miongoni mwa wananchi walioathirika kwa asilimia 85 kwa vifungashio vya viuatilifu. Vile vile Kaimu Mkuu wa Kitengo cha udhibiti wa viuatilifu na utunzaji wa mazingira kutoka TPRI, Mwema Felix, alisema serikali ya awamu ya tano, ipo kwa ajili ya kuwajali watu wa chini kabisa ambao ni wazalishaji na kwa sasa baada ya kufanya tafiti na kubaini kuwa wakulima wa Babati hawana elimu ya kutosha, walijikita katika kutoa elimu.

Alisema utoaji wa elimu huo tunatarajia kulete mabadiliko makubwa, kwa wakulima na jamii zao na tutaweza kulisaidia taifa katika kwenda kwenye uchumi wa kati.

## Vitendo vya ubakaji, ulawiti vyashika kasi

Na Jaliwason Jasson, MANYARA

VITENDO vya ubakaji na ulawiti kwa watoto wilayani Babati, mkoani Manyara, vinaendelea kushika kasi, ndani ya wiki mbili, watoto watatu wenye umri wa miaka (6) wamebakwa na kulawitiwa.

Hayo yalielezwa jana na Ofisa Ustawi wa Jamii mjini hapa, ambaye hakuwa tayari kuandikwa jina lake gazetini, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu unyama wanaofanyiwa watoto.

Alisema watoto wawili kati ya hao walifanyiwa unyama huo, wakati wanatoka shuleni wakielekea nyumbani kwao mtaa wa Miomboni.

"Huyo mtu aliyewalawiti na kuwabaka aliwapiga fimbo na huku akiwalazimisha kuwaingiza kwenye shamba la mbaazi na wao walituambia alipowafikisha shambani hapo akawafanyia ukatili na kuwatisha wasiende kusema wakisema anawaua," alisema ofisa huyo.

Alisema watoto hao walikuwa wanatoka shuleni na wanasoma shule moja iliyopo mjini hapa, darasa la awali.

Vile vile, alisema watoto hao hawakuweza kumtambua mtu aliyewalawiti, lakini walisema alikuwa kijana ambaye alikuwa amevaa sweta jekundu.

Alimtaja mtoto mwingine aliyefanyiwa unyama huo kuwa anasoma darasa la kwanza, ambaye alikutana na baba mmoja aliyemwita kumtuma na baadaye akamfuata na kumtendea unyama huo.

Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Augustino Senga, alithibitisha kutokea kwa matukio hayo na kusema wanawashikilia watu wawili wanaodhaniwa kuwa ndio walifanya ukatili huo.

Watuhumiwa hao aliwataja kuwa ni Patrick Paul (23), fundi ujenzi na mkazi wa Gallapo na Abdalla Bakari (18), mkazi wa Endakiso.

Alisema watoto hao waliliambia jeshi hilo kuwa watu waliowafanyia unyama huo waliwaona wamefuga rasta.

Senga alisema uchunguzi wa daktari ulibainisha kuwa ni kweli watoto hao waliingiliwa, hivyo ametoa wito kwa jamii kushirikiana kukemea uhalifu wa aina yoyote, huku akiwasisitiza viongozi wa dini na serikali kukemea vitendo viovu kwa nguvu zote.

"Lakini tunawaomba wananchi tushirikiane kuwafichua watu hawa wanaowafanyia ukatili watoto wetu, kwa kuwa wanaharibu kizazi kijacho na hatuwezi kuendelea kuwaficha," alisema.



Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Ushirika AMCOS Kijiji cha Komisha Salawe, Kata ya Mwenge, Shinyanga Vijijini, Kwiyolecha Nkilijiwa, akizungumza na waandishi wa habari jana, kwa niaba ya wenyeviti wa AMCOS mkoa huo, kuhusu masikitiko ya agizo la Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga la kuwazuia kununua zao la dengu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Aweso atengua kutendawili hujuma ya maji

**Na Godfrey Mushi,** SAME

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, ametegua kitendawili cha hujuma ya maji kilichomchefua Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, na kuamua kumsimamisha kazi, Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Same, Mussa Msangi kwamba kilisababishwa na kuziba kwa lango la chanzo cha maji na hivyo kufanya msukumo wa maji kuwa mdogo.

Kitendo cha kutotoka kwa maji baada ya kuzinduliwa kwa mradi huo uliojengwa na serikali kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7 kulimkwaza Waziri Mkuu, akieleza kutopendezwa na udanganyifu uliofanyika.

Aweso alifanikiwa kutekeleza agizo la Waziri Mkuu juzi mchana la kuhakikisha maji hayo yanatoka kwa msukumo mkubwa na kutoondoka Hedaru hadi hapo maji yatakapopatikana.

Mradi huo uliojengwa kwa fedha za serikali ulikuwa na uwezo wa kuhudumia zaidi ya wananchi 20,000. Naibu Waziri Aweso, alikwenda katika chanzo hicho akiwa ameongozana na timu maalum ya ufuatiliaji wa maelekezo hayo ya Waziri Mkuu akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule.

Baada ya kumsimamisha kazi, Waziri Mkuu alimkabidhi mhandisi huyo kwa Aweso na kumtaka waziri huyo asiondoke katika mji mdogo wa Hedaru hadi hapo maji yatakapopatikana lakini pia uchunguzi dhidi yake uanze mara moja.

Akiwa katika Mji wa Hedaru wiki iliyopita, Waziri Mkuu pia alivunja bodi tatu za watumia maji katika Wilaya ya Same, kutokana na kushindwa kuwajibika na miradi hiyo kugubikwa na hujuma mbalimbali ikiwamo matumizi ya fedha za umma.

"Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, (RPC-Hamisi Issah) upo hapa, nitafutie viongozi hao wa bodi za maji na walete kwangu, waniambie kwa nini wananidanganya, utaondoka nao hawa," aliagiza Waziri Mkuu akionekana kuchukizwa na kitendo hicho.

Alipomuuliza Mhandisi wa Maji (Msangi) kwa nini amemdanganya, Msangi alijitetea akisema, "Mheshimiwa, maji yapo lakini tatizo mradi huu unatumia Solar (umeme wa jua) na kunapokuwa na mawingu, maji yanasumbua."

# Kada CCM awapa somo viongozi wastaafu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), David Msuya, amewapa somo makatibu wakuu wastaafu wa chama hicho na baadhi ya viongozi waliowahi kupewa dhamana ya uongozi serikalini, kuacha majaribio ya kutaka kukivuruga. Msuya alitoa rai hiyo kwa viongozi hao wastaafu akiwa katika mji wa Moshi, wakati huu ambapo CCM na vyama vya upinzani vikijipanga kuelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji unaotarajiwa kufanyika baadaye Oktoba mwaka huu.

"Mimi rai yangu kwa viongozi hao wastaafu ni kwamba wanapaswa kukaa na kutulia, wakifurahia maisha yao baada ya kulitumikia taifa na chama tawala kwa muda mrefu na sio kuibua mijadala isiyokuwa na mashiko kila siku kwenye vyombo vya habari na hivyo kuwatia hofu wanachama wa CCM," alisema.

Ingawa hakuwataja kwa majina, lakini Makatibu wakuu wastaafu wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba kwa siku kadhaa sasa wamekuwa gumzo katika vyombo vya habari nchini, baada ya kusambaa kwa waraka unaodaiwa kuwa wa kwao, huku wao wenyewe wakieleza kusikitishwa na kauli za kuwachafua na kuwadhalilisha zinazotolewa dhidi yao.

Tayari makatibu hao wakuu, wamedai wameshaandika barua kwenda kwa Baraza la Ushauri la Wazee wa CCM, kuwasihi watumie busara katika kushughulikia jambo hilo linaloendelea kuhatarisha umoja, mshikamano na utulivu wa chama hicho. Aidha, Msuya alitoa rai kwa viongozi hao wastaafu wasijaribu kuivuruga CCM, wakati huu taifa linapokaribia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa ambapo chama hicho kinataka kupata viongozi makini wenye uwezo wa kukizungumzia chama kwa kufuata katiba ya CCM na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi.

Alisema viongozi watakaochaguliwa ni lazima wakayasemea mambo mazuri yanayofanywa na Rais John Magufuli ikiwamo ujenzi wa barabara za lami katika maeneo mengi nchini.

Pia imo miradi ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), ujenzi wa hospitali za wilaya, rufani, zahanati na vituo vya afya.

Alisema Rais Magufuli amepambana na kuja na miradi ya ujenzi wa barabara za juu, kufufua Shirika la Ndege nchini (ATCL), kuanzisha Hifadhi mpya ya Taifa ya Burigi/Chato ambayo itafungua fursa za utalii katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, upanuzi wa bandari na ujenzi wa viwanja vya ndege, mambo ambayo hayajawahi kufanyika katika kipindi kirefu.

# Mwenyekiti ZEC aridhishwa na maboresho ya daftari mpigakura

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MWENYEKITI wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Hamad Mahmood, ameridhishwa na huduma zinazotolewa kwa wananchi kwenye vituo vya kuandikishwa wapiga kura katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani hapa.

Mahmoud alieleza kuridhishwa kwake na maendeleo ya zoezi hilo jana, alipofanya ziara ya kikazi kuangalia maendeleo ya zoezi la kuboresha daftari la kudumu la wapigakura linaloendelea kwenye mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Zoezi hilo lilizinduliwa rasmi Julai 18, mwaka huu na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Akiwa wilayani Hai, alitembelea vituo mbalimbali vinavyoshughulikia maboresho ya daftari hilo na kupokea taarifa za utekelezaji wa kazi kwenye vituo husika ikiwa ni pamoja na kusikiliza changamoto zinazojitokeza kwenye zoezi hilo.

Aidha, Mahmood alikwenda katika vituo vya Kata ya Machame Kaskazini ambako alifurahishwa kuona namna zoezi linavyoendeshwa kwa uwazi hasa baada ya kukutana na mawakala wa vyama tofauti vya siasa, wakifuatiliza utekelezaji wa zoezi hilo.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka watendaji wanaoshiriki zoezi hilo kutekeleza kwa uaminifu majukumu waliyopewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ili kufanikisha zoezi hilo.

Pamoja na hayo, Mahmood aliwakumbusha watendaji hao kutumia kwa uangalifu vifaa vinavyotumika kwa zoezi hilo, kwa kuwa vimepatikana kwa fedha nyingi.

Wakati anazindua zoezi hilo, Majaliwa alisema mpiga kura yeyote atakayejiandikisha vituo zaidi ya kimoja na ikathibitika katika zoezi la uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura lililoanza jana katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, watakutana na mkono wa dola.

Kwa mujibu wa NEC, kwa upande wa Tanzania Bara, tume imeongeza vituo vya kuandikisha wapigakura kutoka 36,549 hadi 37,407, vituo 6,208 vimebadilishwa majina, vituo 817 vimehamishwa kutoka kijiji au mtaa mmoja kwenda mwingine na vituo 19 vimehamishwa kutoka kata moja kwenda kata nyingine," alisema.

Kwa upande wa Tanzania Zanzibar, tume imeongeza vituo vya kuandikisha wapigakura kutoka vituo 380 hadi vituo 407.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 23, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 15



**Hatua hii ya COSTECH, chachu ya ubunifu, sayansi na teknolojia**

Ukurasa 17



## JIELIMISHE

Fahamu ukweli wa dhana tano kuu kuhusu nyoka



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?

## Wenza asili ya Asia wapata watoto waliopandikizwa kimakosa



# Taasisi ya Ustawi wa Jamii, nuru ya ukuaji wa uchumi

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# Epuka mauaji wenye ualbino kwa imani za kishirikina



Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), David Misime. **PICHA: MTANDAO**

KILA mwaka tarehe Juni 13, kunakuwapo na Maadhimisho ya siku ya watu wenye Ualibino duniani na Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi zinazoadhimisha siku hii.

Mwaka huu Maadhimisho hayo yalifanyika huko jijini Dodoma na kuambatana na utoaji wa elimu pamoja na kujadili changamoto zinazowakabili watu wenye ualbino zikiwapo za kijamii, kiuchumi na kiusalama.

Kuhusiana na changamoto za kiusalama katika maeneo mbalimbali duniani kumekuwapo na changamoto hiyo na Tanzania ikiwapo.

Matatizo ya kiusalama kwa watu wenye ualbino yalianza kujitokeza matukio ya kujeruhiwa na kuuawa kuanzia mwaka 2006.

Matukio hayo kulingana na uchunguzi uliofanywa na Jeshi la Polisi ulibaini kuwa yalitokana na imani potofu kwa baadhi ya watu kuamini kuwa akiwa na nywele za mtu mwenye ualbino atakuwa tajiri na atapata mgodi wenye madini mengi au atapata samaki wengi kwenye uvuvi.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), David Misime katika mahojiano na mwandishi wa makala haya, alieleza juhudi za Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine na wananchi kwa ujumla zilivyosaidia kupunguza matukio hayo kwa kuwakamata watuhumiwa waliotenda matukio ya aina hiyo na kutoa elimu endelevu kwa jamii ili kuondokana na kujihusisha na imani hizo potofu.

Pamoja na kuhakikisha kuwa wanaotenda makosa hayo wanakamatwa, tumeona pia utoaji elimu ni njia kubwa ya kuzuia matukio kama hayo.

Tunawafanya wananchi waelewe kuwa watu wenye ualibino ni binadamu kama wengine na kwamba kiungo cha mtu mwenye ualbino hakiwezi kukufanya kuwa tajiri, kwani kama ingelikuwa hivyo ungelikutana na familia zenye watu wenye ualbino waliokuwa matajiri kinyume chake ni watu wenye maisha ya kawaida kama walivyo watu wengine.

"Tunawafanya watu waelewe kuwa utajiri unatokana na kufanya kazi kwa bidii, weledi na ubunifu na si vinginevyo. Pia watu wanatakiwa watambue kuwa wakiendeleza imani hizo potofu wataishia kuwa maskini kwa kutengana na familia zao na kupelekea kunyongwa hadi kufa kama waliofanya matukio kama hayo" SACP Misime alisema.

Huko mkoani Mwanza walikamatwa na walifikishwa mahakamani na wameshahukumiwa na kunyongwa hadi kufa. Huko Geita watuhumiwa Saba wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa na huko Shinyanga watatu nao hivyo hivyo.

Mbeya nako watuhumiwa wanne wa matukio ya kujeruhi na huko Kagera mtuhumiwa mmoja alihukumiwa kifungo cha miaka 20 jela.

Kama unavyoona jumla ya watu 21 wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa na kesi zingine bado ziko mahakamani hii inaonyesha wazi kuwa hata kama hujui kusoma wala huoni kuwa imani hizo potofu matokeo yake sio utajiri bali ni kunyongwa hadi kufa.

Jeshi la Polisi limeweka mikakati mbalimbali ya kuendelea kupiga vita vitendo vya mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi ikiwemo kuendelea kukusanya taarifa za kiintelejensia zitakazosaidia kuwabaini wanaofanya vitendo hivyo, Kutoa elimu kwa jamii kwa kushirikiana na wadau wengine ili waachane na imani za kishirikina zilizojengeka kuwa unapotumia viungo vya albino vinaweza kusaidia katika biashara, shughuli za uchimbaji madini, uvuvi na katika uchaguzi.

Pia, Jeshi la Polisi mikoa yote inaendelea na Operesheni za kuwakamata waganga wa jadi wanaopiga ramli chonganishi na kuwafundisha albino mbinu mbalimbali za kuchukua tahadhari na kutoa taarifa mapema pindi wanapowatilia mashaka watu wanaotaka kuwadhuru.

Wito wa Jeshi la Polisi kwa jamii ni kuepukana na imani potofu, watu wathamini ubinadamu, utu wafanye kazi kwa bidii kwani ndio njia pekee ya kukufikisha kwenye maendeleo na kuendelea kuishi ukiwa huru.

Tuendelee kupeana elimu ya kuachana na imani potofu ambazo zinaaibisha nchi yetu ambazo hazina ukweli ndani yake na elimu hiyo ianze kuanzia ngazi ya familia, mtaa, kijiji hadi tarafa.

Mtu mwenye ualbino ni binadamu kama alivyo binadamu mwingine, hivyo tuheshimu utu wao kama ulivyo wa wengine, tusifanye mambo yatakayoleta laana katika familia zetu.

Jeshi la Polisi kupitia kitengo cha Ushirikishwaji wa jamii, kwa jamii ambayo bado haina uelewa katika masuala ya maumbile ya watu hususani wenye ualbino sambamba na kuwaelimisha wenye kuamini ushirikina ambao husababisha kuwaondolea uhai binadamu wengine.

Aidha, Jeshi la Polisi limeendelea kuwaongezea ulinzi watu wenye ualbino na pia limewataka wanasiasa kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuelimisha jamii kuhusiana na jambo hilo kwasababu wanaishi karibu na jamii.

Pia wanasiasa wanatakiwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kuwapatia elimu waganga wa jadi kuacha imani za kishirikina.

***Imetolewa na:-***
***Kitengo cha Uhusiano,***
***Makao makuu ya Jeshi la Polisi,***
***Dar es Salaam,***
***habariphq@gmail.com***



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Maneno yawapayo watu shida

KWA mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha (Zanzibar), lugha ya Kiswahili imepanuka sana na matumizi yake yameenea kwa kasi duniani kuliko watu wengi walivyotarajia. Imevuka kiwango cha kuwa lugha ya taifa na kuwa na hadhi ya kimataifa.

Sasa Kiswahili kimevuka mipaka ya Afrika Mashariki na kusambaa katika mabara yote ulimwenguni. Tayari kimekuwa miongoni mwa lugha zinazotumika katika mikutano ya kimataifa na mawasiliano ya intaneti (mtandao wa mawasiliano kimataifa wa kikompyuta).

Kutokana na mabadiliko na maendeleo hayo, pameibuka matumizi ambayo si fasaha, na mara nyingine si sahihi, katika mfumo wa sarufi, matamshi na hata maana ya maneno ya lugha hiyo. Kwa mfano neno 'kwa' hutumiwa mno na wazungumzaji kama ilivyo vyombo vyetu vya habari. Neno hili lina maana nne: Linaunganisha sentensi mbili; neno linalotumika kuhusisha tendo na kifaa kinachotumika kutendea.

Neno linaloeleza namna tendo lilivyofanyika k.m. ("Amesoma kwa shida sana;" anaishi kwa mashaka (shida zinazompata mtu katika maisha); neno linaloeleza pahali tendo lilipofanyika: "Amepelekwa kwa daktari; ingawa ni mbali lakini amekwenda kwa miguu."

Neno linaloonesha kwenda, kutoka au kukaa mahali panapomilikiwa na mtu mwingine: "Atakwenda kwa baba yake." Namna, jinsi ya kutenda jambo: "Tembea kwa maringo." Neno linalobainisha uwiano baina ya mambo mbalimbali: "Wamefungana mabao mawili kwa mawili." Neno linaloonesha sehemu za hesabu kitarakimu kwa mfano: "Nne kwa tano (4/5)."

Neno linalotumika kuunganisha vitu viwili katika kulinganisha: "Walishindana nyumba kwa gari;" neno linalounganisha kitu kimoja na kingine katika utendaji. Pamoja na ufafanuzi huu, bado neno 'kwa' hutumiwa tofauti na maudhui (mambo yanayoelezwa katika hadithi, riwaya, hotuba, tamthilia au masimulizi yoyote yale) yake.

Hukereka (sumbuliwa na jambo; chukizwa) kila nisikiapo redioni, kwenye runinga au kusoma magazetini jinsi wanadamu wanavyolinganishwa na mtambo/mitambo! Mfano: "Bony atupia Ivory Coast ikitesti mitambo." Neno 'tupia' nilikwisha eleza jinsi linavyotumika kwa hiyo niwieni radhi kwa kutolitanzua tena.

'Testi' si Kiswahili ingawa hutumiwa sana na magazeti yetu ya michezo. Maana yake ni jaribu, tahini; pima. Aidha 'mtambo' ni kifaa chenye kutoa nguvu za kuendesha vitu vinavyofanya kazi mbalimbali; kamba inayotengenezwa kwa chane za miyaa na hutumiwa kuvutia mtego wa samaki.

Vilevile 'tupia' nililitolea maana yake kwenye matoleo yaliyopita. Neno hilo latokana na 'tupa' lenye maana ya peleka au vugumiza kitu kisichohitajika kwenye kikapu au shimo la taka; acha bila kutunza; rusha kitu kutoka ulipo kwenda mbali. Pia ni kifaa kigumu cha chuma cha kukerezea au kunolea vitu vingine, mfano kisu, panga, jembe n.k.

"Yanga mpya balaa" ni kichwa kilichofuatiwa na habari ifuatayo: "Licha ya maneno ya kejeli kutokana kwa watani zao, Yanga wametamba kujua wanachokifanya ya kuhusiana na usajili wanaoendelea nao, hasa wa wachezaji wa kigeni."

'Balaa' ni jambo, kitu au mtu anayefikiriwa kuleta maafa, mkosi au hasara; kisirani, nuksi. Pia ni jambo lenye kuleta hali ya kutoelewana; kizaazaa, mtafaruku, beluwa. Je, ni kweli kuwa Yanga mpya ni 'hasara, kisirani au nuksi?'

Aidha sentensi ya mwandishi imeandikwa shaghalabaghala (shelabela; upogoupogo; bila mpango). Ingeandikwa: "Licha ya maneno ya watani wao, Yanga wanasema wanajua wanachofanya ya kuhusu usajili, hasa wachezaji wa kigeni."

"Okwi: Sina bifu na Simba." Wasiwasi wangu ni waandishi wa leo kushabikia sana maneno ya mitaani ambayo Waingereza huyaita 'slang.' Imenilazimu kutumia neno la Kiingereza ili kuwazindua waandishi wanaopenda sana matumizi ya kigeni ingawa yapo ya Kiswahili! Mwandishi angeandika: "Okwi hana kinyongo na Simba kwa kutoshirikishwa kwenye tuzo za MO Simba Award msimu huu.

Hata hivyo habari hiyo yenye aya (paragrafu) tano, mwandishi haelezi mtu aliyesema au wanaosema Okwi ana kinyongo kwa kutoshirikishwa kwenye tuzo za MO Simba Award. Malalamiko hufuatiwa na kinyongo. Mwandishi haelezi jinsi Okwi anavyolalamika hata kuwa na kinyongo alichokiita 'bifu.'

Maana ya 'beef' ni nyama ya ng'ombe lakini pia kwa maana nyingine (kwa Waingereza wenyewe), ni maneno ya mitaani yakimaanisha kuwa na dukuduku, lalamika. Kwa mfano maana ya 'beef up' ni imarisha.

**Methali: Maji ya pondo hayataki tanga. marobarnabas@yahoo.com. 0784 334 096**

ELIMU
NA MWALIMU REUBENI LUMBAGALA

# Hatua ya COSTECH, chachu ya ubunifu, sayansi na teknolojia

WABUNIFU ni wadau muhimu katika ukuzaji wa sayansi teknolojia na maendeleo kwa ujumla.

Kutokana na umuhimu wa wabunifu, kuwawezesha ni jambo la kutiliwa mkazo mkubwa ili kazi zao ziweze kuleta manufaa kwa nchi na sehemu zingine zinazohitaji kazi zao za kisayansi na teknolojia.

Dira ya nchi yetu ni kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Dira hii itaweza kufikiwa mapema ikiwa kazi za wabunifu zitatambulika, kuthaminiwa na kuendelezwa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ambayo ni mdau muhimu wa maendeleo ya nchi katika nyanja zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Wabunifu wakiwekewa utaratibu na mazingira mazuri ya kuwawezesha, nchi itapiga hatua kubwa katika nyanja ya sayansi na teknolojia ambayo ni muhimu katika suala zima la kuchagiza uchumi wa viwanda hatimaye uchumi wa kati kwa maendeleo endelevu nchini.

Naungana na Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa hatua yake ya kuwaunga mkono wabunifu 60 baada ya kutoa Sh. milioni 700 ili ziwasaidie kuendeleza tafiti na bunifu zao kwa minajili ya kuleta tija na manufaa kwa Taifa letu.

Neema hiyo ilitangazwa Julai 10 mwaka huu na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha katika Kongamano Maalum la Ubunifu lililoandaliwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), likishirikiana na COSTECH katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam (DITF).

Katika kongamano hilo, Naibu Waziri Ole Nasha anasema: "Mwaka jana tuliandaa mashindano maalum ya ubunifu na walipatikana washindi wa kitaifa 60... kwa kutambua umuhimu wa kazi zao, pamoja na kutoa fedha pia tumeanza mchakato wa kutoa mwongozo maalum wenye utaratibu wa kuendesha vituo vya teknolojia na ubunifu."

Sh. milioni 700 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kuwasaidia wabunifu ni kiashiria kuwa serikali yetu imedhamiria pasi na shaka kuhusu nia ya kukuza sayansi na tekonolojia ili kufikia uchumi wa viwanda.

Kutokana na ukweli kuwa wabunifu wapo wengi na serikali imeonyesha kuwajali na kuwaunga mkono katika kazi zao, kasi ya uvumbuzi na uandaaji wa kazi zilizo bora utaongezeka na hapo ndipo ukuaji wa sayansi na teknolojia nchini utakapokuwa ni suala dhahiri na si nadharia tu.



Mmoja wa wanasayansi (kulia), akikata chuma kwa ajili ya kujitengenezea kifungua chupa (opener). **PICHA: MTANDAO**

> Jambo la msingi kabisa ni kwa wabunifu kuzitumia vizuri fedha wanazopata kutoka serikalini na wadau wengine katika kukuza kazi zao.

Aidha, mpango wa serikali wa kuandaa mwongozo maalum wenye utaratibu wa kuendesha vituo vya teknolojia na ubunifu ni jambo litakalokuza kwa kiwango kikubwa maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Ni lazima mwongozo uwepo ili vituo hivyo viendeshe shughuli zao kwa mujibu wa maono na malengo ya serikali, ili sekta ya umma na sekta binafsi ziwe na sauti moja katika kukuza sayansi, teknolojia, ubunifu na maendeleo.

Pia, kitendo cha serikali kuiagiza COSTECH kukaa pamoja na Wakala wa Usajili wa Biashara na Kampuni (BRELA) ili kukomesha wizi wa kazi za wabunifu ni jambo litakalokuza sayansi na teknolojia kwa kiwango kikubwa.

Wapo watu wasio waaminifu ambao wanaweza kutumia shida za wabunifu kuwaibia kazi zao na hatimaye kufaidi jasho lao huku wenyewe wakiendelea kuishi maisha ya shida.

Hivyo basi, wito huu ni muhimu kuzingatiwa zaidi na wabunifu ambao ni waathirika wa kuibiwa kazi zao.

Utaratibu maalum wa kulinda kazi za wabunifu, ni vyema ukawekwa mapema ili wabunifu waanze kula matunda ya kazi zao haraka iwezekanavyo.

Jambo la msingi kabisa ni kwa wabunifu kuzitumia vizuri fedha wanazopata kutoka serikalini na wadau wengine katika kukuza kazi zao.

Kupata fedha za kuendeleza kazi za wabunifu ni jambo moja lakini kuzitumia fedha hizo katika lengo mahsusi ni jambo la msingi zaidi, kwani kwa kwenda kinyume na malengo ya fedha hizo ni kurudisha nyuma maendeleo ya mbunifu mwenyewe na ya nchi pia.

Kama ambavyo serikali kwa kushirikiana na wadau wengine walivyo na nia ya kuwasaidia wabunifu katika kazi zao, vilevile wabunifu nao waone umuhimu wa kujituma zaidi katika bunifu zao na wale watakaobahatika kupata ufadhili wa kuendeleza kazi zao, watumie fursa hiyo vizuri ili uendelezaji wa kazi za wabunifu liwe suala endelevu.

Wadau wengine wajitokeze kuiunga mkono serikali katika kutoa ufadhili wa kazi za wabunifu ili idadi ya wanaopata ufadhili iongezeke.

Ushirika wa sekta ya umma na binafsi ukiwa imara, utakuza sayansi, teknolojia na maendeleo kwa kasi kubwa zaidi.

Wabunifu, uwanja ni wenu, andaeni kazi nzuri ili kupata ufadhili na pia kushiriki moja kwa moja katika ukuaji wa uchumi na maendeleo. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoa wa Dodoma.

***Maoni: (+255) 764 666349.***

UGUNDUZI

**NA MANENO SELANYIKA**

# Taasisi ya Ustawi wa Jamii, nuru ya ukuaji wa uchumi



Baadhi ya wahitimu wa kozi na ngazi mbalimbali kutoka Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW). **PICHA: MANENO SELANYIKA**

MCHANGO wa taasisi mbalimbali za umma unahitajika katika kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano zinazolenga kuboresha maisha ya wananchi sanjari na ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Taasisi za elimu ya juu ikiwamo Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW) zina mchango muhimu katika ujenzi wa Tanzania mpya, inayolenga kufikia uchumi wa kati hadi ifikapo mwaka 2025.

Miradi mikubwa inayotekelezwa kwa sasa na serikali itakapokamilika, yumkini itaifikisha nchi kwenye kiwango hicho cha uchumi kinacholengwa na taifa letu.

Miradi hiyo ni pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), ujenzi wa miundombinu, mradi wa uzalishaji umeme wa Stiegler's Gorge na uboreshaji wa huduma za jamii mathalani huduma za afya na elimu lengo likiwa ni kuboresha ustawi wa jamii yetu.

ISW ni chuo ambacho kimekuwa kikitoa wahitimu walioiva kitaaluma katika kozi za ustawi wa jamii na hivyo taasisi kujijengea heshima si kwa Tanzania tu bali ulimwenguni kote.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Joyce Nyoni, anasema Chuo kinafundisha kozi za Ustawi wa jamii, menejimenti ya rasilimali watu, Sheria, Uamuzi na Usuluhishi, ambazo ni muhimu katika ujenzi wa uchumi imara.

> ...Wahitimu huandaliwa ili waweze kutengeneza programu zenye tija kwa makundi mbalimbali yakiwamo makundi maalum ili yaweze kuwa na mchango katika maendeleo.



Jengo la Utawala la ISW.



Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii nchini (ISW), Dk. Joyce Nyoni.

"Kwa mfano kozi ya Ustawi wa Jamii inaandaa vijana wetu kuweza kufanya kazi kwa karibu zaidi na jamii... wahitimu huandaliwa ili waweze kutengeneza programu zenye tija kwa makundi mbalimbali yakiwamo makundi maalum ili yaweze kuwa na mchango katika maendeleo," anasema na kuongeza:

"Wahitimu wetu pia wanaandaliwa ili watoe huduma za utengamao na mabadiliko ya tabia (rehabilitation and behavioural changes) ili kudumisha amani, utulivu na kujenga ustahimilivu katika jamii ambao ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi."

Dk. Joyce anafafanua kuwa kozi hiyo ni kozi mama na mtambuka kuanzia ngazi ya Astashahada mpaka Shahada ya Uzamili ambayo imetoa maofisa ustawi wa jamii waliobobea kwenye masuala mbali mbali ya kijamii.

Kwamba maofisa wanaoweza kuishauri jamii kukabiliana na maovu kama ukatili wa kijinsia, utunzaji wa wazee, watu wanaoishi kwenye mazingira magumu na watoto waishio kwenye mazingira hatarishi.

"Wahitimu hawa wanajumuisha idadi ya wataalamu wa ustawi wa jamii ambao wanatoa huduma kwa jamii yetu, katika halmashauri, wilaya, mikoa na mashirika mbali mbali hapa nchini," anabainisha.

**SHERIA ZA KAZI**

Kwa upande wa Mafunzo ya sheria za kazi ambayo ni kozi za Stashahada ya Uzamili ya Sheria, Uamuzi na Usuluhishi Dk. Joyce anasema yanalenga kuandaa wataalamu wenye uwezo wa kutatua migogoro mahali pa kazi, sheria ambazo ni muhimu katika ujenzi wa uchumi imara.

Anabainisha kwamba migogoro ni kikwazo cha ustawi iwe mahala pa kazi au katika jamii husika, hivyo Chuo kinafundisha wataalam wa usuluhishi, baadhi yao wakifanya kazi katika Mahakama ya Kazi na Usuluhishi, vyama vya wafanyakazi na pia katika ofisi mbalimbali kama washauri wa masuala ya mahusiano kazini.

"Wataalam wa kozi hizi wanachangia tija mahala pa kazi iwe kwenye viwanda au kampuni kwani pasipokuwepo na migogoro ya kikazi, ufanisi huwa ni maradufu," anasema na kuongeza:

"Hawa watu ni muhimu sana mahala pa kazi ...bila hawa hakuna tija kazini na hawa ni wataalam wa kutatua migogoro mahala pa kazi... natoa wito kwa kampuni na taasisi mbalimbali nchini, kuwatumia maofisa hawa."

**KOZI ZA BIASHARA**

Dk. Joyce anabainisha kwamba kozi za biashara pia zinatolewa na taasisi yake, zinawawezesha wahitimu kujiajiri na kutengeneza ajira kwa wengine.

Anasema katika zama hizi za uchumi huria wanawajenga wanafunzi kitaaluma kiasi kwamba pindi wanapohitimu na kutaka kujiajiri hawahitaji mtaji mkubwa kwani tayari wanaweza kutoa huduma ambayo thamani yake ni kubwa na kuwawezesha kupata fedha nyingi katika soko.

"Hivyo kama taasisi, tuna wajibu wa kushiriki uchumi wa viwanda na moja ya ushiriki wetu ni kuwajenga vijana wetu wawe washiriki katika ujenzi wa uchumi huo kwa vitendo," anasema

Anabainisha kuwa wahitimu wa chuo chake wana uwezo wa kushindana katika soko la ajira kokote Afrika Mashariki na hali hiyo inatokana na ubora wa mafunzo wanayopata.

"Hapa tunazingatia sana mafunzo kwa vitendo ili kuwajengea wahitimu uwezo wa kufanya kazi kwa kujiamini na ndiyo maana kila Alhamisi wanafunzi wetu huenda kwenye maeneo ya jamii na ofisi mbali mbali kufanya mazoezi (concurent field work)," anasema na kuongeza:

"Vile vile wanafunzi wetu hupata mafunzo ya muda mrefu wakati wa likizo zao (block field work) na kujifunza kwa vitendo."

**WAZIRI**

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu wakati akizindua bodi ya Magavana ya Taasisi mapema mwaka huu alisema bado kuna uhitaji wa Maofisa Ustawi wa Jamii nchini na hivyo akakishauri chuo kufanya kazi zaidi ya kuandaa wataalam hao.

Alibainisha kwamba wataalam wa kozi ya ustawi wa jamii ni muhimu katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda.

**MALENGO**

Dk. Joyce anayataja malengo ya taasisi kuwa ni kuendelea kubadili maisha ya jamii na watu wake kwa kufanya tafiti, kutoa elimu na ushauri na weledi kwa ubora wa hali ya juu itakayochochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Anawashauri viongozi, Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuandaa mazingira yatakayowawezesha wataalam wa ustawi wa jamii kutoa ushauri nasaha katika maeneo wanayoishi wananchi.

"Tunataka kufundisha watu wengi zaidi wajue masuala ya ustawi wa jamii na wanaoweza kutusaidia kwa hilo ni viongozi wakuu wa mikoa na wilaya," anasema.

Anabainisha kwamba wataalam watakaowafundisha kitaalam wanaitwa 'Para Social Workers" ambao watasaidia kutoa mafunzo ya ushauri nasaha kwa jamii kwani, wanawafikia wananchi hadi kwenye ngazi ya mitaa na vijiji.

"Ushauri nasaha si upande wa masuala ya Ukimwi tu, kuna mambo mengi hapo, kuna masuala ya ushauri kwa vijana, ushauri kwa wanandoa na mengine kama hayo," anasema.

Anabainisha kwamba chuo kina mpango wa kupeleka huduma zake maeneo mbalimbali ya nchi na kwa kuanzia wana mpango wa kufungua matawi kwa Kanda.

Dk. Joyce anasema taasisi yake pia anaandaa mitaala mipya itakayokuja na kozi ambazo mbali na mambo mengine zitaangalia masuala ya watoto kwa mapana zaidi.

Anasema Chuo kimekuwa kikiboresha miundombinu kutegemea upatikanaji wa fedha na hadi sasa, kimeboresha miundombinu yake kwa kiwango kikubwa.

"Tunaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia kwa kuongeza vyumba vya madarasa, mabweni na kumbi za mihadhara... muhimu zaidi tunatamani tuwe na mabweni ya kutosha kwa wasichana," anasema.

> Tunaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia kwa kuongeza vyumba vya madarasa, mabweni na kumbi za mihadhara...

**MWANZO WAKE**

Dk. Joyce anasema chuo hicho (ISW), kilianzishwa mwaka 1973 kwa sheria namba za 26 na kufanyiwa mapitio mwaka 2006, kwa lengo la kuandaa wataalamu wa kuimarisha utoaji huduma za jamii chini ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto.

Anabainisha kuwa taasisi yake inashirikiana na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ili kuongeza ufanisi.

Anataja baadhi ya taasisi wanazoshirikiana nazo kuwa ni Chuo Kikuu cha Bergen, Chuo Kikuu cha Oslo vyote vya nchini Norway.

"Tumekuwa tukishirikiana na kubadilishana ujuzi, uzoefu na taasisi hizo," anasema.

Dk.Joyce anasema moja ya majukumu makuu ya taasisi za elimu ni kufanya utafiti sanjari na kutoa mafunzo.

***Mwandishi anapatikana kupitia namba 0716386409, 0786461073***

JIELIMISHE

## Fahamu ukweli wa dhana 5 kuu kuhusu nyoka

KWA kawaida nyoka hutazamwa kwa hatari kubwa, werevu na mara nyingine hata kuhusishwa na imani potofu na uchawi katika baadhi ya jamii za Kiafrika.

Kwa kawaida nyoka anakuwa juu ya orodha ya mambo ambayo mtu huyaogopa maishani mwake.

Maelfu ya watu duniani hufariki kutokana na sumu kali ya nyoka baada ya kuumwa kila mwaka kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Ukosefu wa matibabu na hata matibabu mabaya hufanya vifo hivyo kutokingika.

Kuumwa na nyoka huenda kusionekane kuwa janga baya la kiafya.

Lakini katika maeneo mengine duniani ni hatari ya kila siku na huenda husababisha maafa ama hata kubadilisha maisha ya mtu.

Pengine ndio sababu ya kuwapo dhana tofauti, baadhi zikiwa potofu kuhusu wanyama hawa.

Kuna mambo ambayo yanahitajika kuwafahamu zaidi wanyama hawa.



**HAWATAMBAI KWENYE MAWE NA KAMBA**

Wanaweza kutambaa juu na hata chini ya mawe, kwenye miti na majengo. Nyoka hupenda kujificha ardhini.

Ni rahisi kwao kujificha chini ya vichaka, na vigumu kutambaa chini ya mawe madogo kwenye bustani.

Ni vyema kuzikata nyasi ziwe ndogo na uondoshe masalio yoyote ya nyasi zilizokatwa au majani makavu yaliyoanguka na kujikusanya.

Kadhalika ni vyema uondoshe sehemu za mti zilizoanguka juu ya paa au zinazoning'inia kutoka nyumba yako.

**UKIONA MTOTO WA NYOKA,**
FAMILIA NZIMA IPO HAPO

Iwapo nyoka huzaa watoto au kutaga mayai, kawaida anapojifungua huwaondoa watoto na kuwaacha kivyao.

Iwapo utamuona nyoka mkubwa karibu na mdogo basi huenda ni sadfa tu.

Wao hutawanyika punde wanapojifungua.

**NYOKA HUTELEZA**

Kawaida, watu ambao hawajawahi kumgusa nyoka hudhani kwamba wanyama hao huteleza ukiwagusa. Ngozi ya nyoka huonekana kuwa kavu, lakini kwa kuigusa ni nyororo.

**NYOKA HUOGOPA BINADAMU**

Nyoka wanaogopa binadamu zaidi ya binadamu wanavyowaogopa. Kwa kawaida huwa wana haya au aibu sana na iwapo wangekuwa na nafasi wanaweza kutoroka wasionekane.

Ni iwapo tu amekwama au ametishiwa, kama ilivyo kwa kiumbe chochote, nyoka hushambulia kujilinda.

Lakini mara nyingi baadhi huona afadhali kutoroka kuliko kushambulia.

**KUTAGA MAYAI**

Licha ya kwamba reptilia wengi hutaga mayai, si nyoka wote wanaotaga. Baadhi ya nyoka kama aina ile ijulikanayo Oriental Vine, huzaa nyoka wadogo.

**MENGINE KUHUSU NYOKA**

Je unafahamu kwamba kuna zaidi ya aina 3000 za nyoka duniani?

Sasa kati yao, 375 wana sumu.

Nchini Australia, kuna aina 140 za nyoka na 100 huwa na sumu. Nyoka mwenye sumu kali duniani ni wa Australia - Inland Taipan.

Nyoka huwa na urefu wa kati ya sentimita 10 mpaka mita 7 aina ya chatu.

Nyoka huishi katika mazingira tofauti ikiwemo vichakani, jangwani na hata ndani ya maji.

Hutumia ulimi wao kumnusa adui kabla ya kumshambulia. **BBC**

UTAFITI

# Mtindo wa maisha unaweza kuzuia matatizo ya akili



Mazoezi ya mwili ni moja ya njia za kupunguza hatari ya kupata maradhi ya kiakili **PICHA: MTANDAO.**

KARIBU kila mmoja anaweza kupunguza ugonjwa wa matatizo yanayotokana na kuathirika kwa akili (dementia), hata kama ni ya kurithi katika familia, kulingana na utafiti wa maisha ya kiafya.

Utafiti wa watu karibu 200,000 unaonyesha hatari ya kupata matatizo ya kiakili inashuka kwa kiwango cha robo tatu. Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Exeter wanasema matokeo ya utafiti wao yalikuwa ni ya kusisimua, kutia msukumo na yalionyesha kuwa watu hawawezi kuhangaishwa na hofu ya kupata maradhi ya kuathirika kwa akili (dementia).

Matokeo yalifichuliwa katika Kongamano la Kimataifa la Jumuiya ya Magonjwa Yanayodumaza Akili yanayofahamika kwa lugha ya kitaalamu kama -alzheimer's

## YALIYOZINGATIWA

Watafiti waliwapa alama watu juu ya mtindo wa maisha kwa kuzingatia mazoezi ya mwili, lishe, pombe na uvutaji sigara.

Na miongoni mwao mfano wa mtu aliyepata alama nzuri ni yule ambaye alikuwa na sifa zifuatazo:

Kwamba havuti sigara kwa sasa na anayeendesha baiskeli kwa kasi ya kawaida kwa muda wa saa mbili na nusu kwa wiki. Kwamba ambaye hula mlo kamili ambao unajumuisha aina tatu za matunda na mboga kwa siku, na ni nadra kula nyama za kusindikwa.

Kwamba hunywa glasi moja ya bia kwa siku, asiyevuta sigara mara kwa mara na hafanyi mazoezi ya mara kwa mara.

Kwamba hula chakula chenye matunda chini ya mara tatu na mboga kwa wiki, na hujumuisha mara mbili au zaidi nyama za kusindikwa na nyekundu kwenye mlo wake kwa wiki.

Aidha, hunywa walau glasi tatu za bia kwa siku. Sue Taylor, mwenye umri wa miaka 62, kutoka eneo la Exeter, ameshuhudia athari za magonjwa ya akili katika familia yake kwani mama yake na bibi yake walikuwa na maradhi hayo.

Anahudhuria darasa la mazoezi ya mwili kwenye bustani mara tatu kwa wiki hata katika majira ya baridi na hutembea kwa muda wa dakika 45 kabla ya kwenda kazini.

"Inahitaji juhudi kubwa, unapaswa kufikiria kuhusu mazoezi haya na kuhakikisha yanaingia akilini na maishani mwako," anasema.

Hata hivyo, Taylor anasema faida zake ni muhimu, hususan kwa wajukuu wake.

"Ninataka tu kutunza akili yangu katika hali nzuri kwa muda mrefu iwezekanavyo...sitaki wajukuu wamkose bibi kimwili na kiakili,"anasema.

## MAISHA BORA YA KIAFYA YANALETA TOFAUTI GANI?

Utafiti ulifuatilia maisha ya watu 196,383 wenye umri kuanzia miaka 64 kwa muda wa miaka minane.

Ulitathmini vipimo vya vinasaba (DNA) vya watu kupima hatari za maumbile yao ya urithi za kupata hatari ya ugonjwa.

Utafiti huo ulionyesha kuwa kuna visa 18 vya maradhi ya dementia kati ya watu 1,000, ikiwa watazaliwa na jeni za ugonjwa na baadaye kuishi mtindo wa maisha ya kutozingatia afya.

Lakini kiwango hicho kilishuka hadi kufikia visa 11 kati ya watu 1,000 wakati wa utafiti, ikiwa watu hao wenye hatari ya kupatwa na ugonjwa huo wangeishi mtindo wa maisha unaozingatia afya.

Huenda idadi ikaonekana kuwa ni ndogo, lakini hiyo ni kwasababu watu wenye umri wa miaka chini ya 70, huwa wanakuwa na uwezekano mdogo wa kupata maradhi ya dementia yanayoathiri akili. Watafiti wanasema kuwa kupunguza viwango vya dementia kwa kiwango cha theluthi moja duniani, kunaweza kuwa na athari nzuri miongoni mwa watu wenye umri wa uzee ambao kwa kawaida huathiriwa na ugonjwa huo.

"Kiwango hicho kinaweza kuwa ni maelfu ya watu," anasema Dk. David Llewellyn.

Pia aina hii ya utafiti haiwezi kuidhinisha moja kwa moja sababu za mtindo wa maisha unaosababisha hatari tofauti za dementia. Ni sehemu chache katika data zilizobainika. Lakini matokeo, yaliyochapishwa katika jarida la shirika la kitabibu la Marekani (Journal of the American Medical Association) yamefanana na yale ya utafiti na ushauri wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

## JE UNAWEZA KUEPUKA DEMENTIA KABISA?

La kusikitisha ni kwamba, unaweza kuishi maisha ya mtakatifu, lakini bado ukapata ugonjwa huu. Mtindo wa maisha hubadili tu tabia mbaya.

Hata hivyo, hakuna dawa za kubadili sababu ya ugonjwa huu. Kupunguza uwezekano ya kuupata ndicho kila mtu anachoweza kukifanya.

Hata hivyo, matokeo huenda yasiwe sawa kwa kila mtu kwa watu wote miongoni mwa watu wenye umri wa miaka juu ya 40 na juu ya 50 ambapo ndipo mtu anaweza kuupata, wanasema watafiti.

## UJUMBE MUHIMU

Hata kama una wasiwasi juu ya dementia, labda una historia ya ugonjwa huu katika familia yako, utafiti huu unasema haijalishi kuwa utaupata, Dk. David Llewellyn ameiambia BBC.

"Bado una uwezekano wa kupunguza hatari ya dementia kama utaweza kuishi maisha ya kiafya na hilo kusema kweli linatia moyo." Anaongeza.

Mtafiti mwenzake Dk. Elzbieta Kuzma anasema mara ya kwanza kwa mtu kukuonyesha kuwa anaweza kukabiliana na hatari ya urithi wa dementia, matokeo yake husisimua.'

## WATAALAMU WANASEMA NINI ?

Fiona Carragher, kutoka shirika la kukabiliana na magonjwa ya ubongo na akili -Alzheimer's Society, anasema:

"Kwa hali iliyopo sasa ya kwamba mtu mmoja hupata dementia kila baada ya dakika tatu nchini Uingereza, kufahamu jinsi ya kupunguza hatari za dementia ni jambo muhimu sana."

"Kwa hiyo kula mboga, badala ya kunywa mchanganyiko wa vileo, kunywa mchanganyiko wa juisi ya matunda na kuwa na vifaa vya mazoezi ili kufanya mazoezi ya mwili ni muhimu zaidi!" anaongeza.


Dk. Carol Routledge kutoka kituo cha utafiti wa magonjwa ya akili nchini Uingereza- Alzheimer's Research UK, anasema matokeo ya utafiti ni muhimu.

"Huu ni ushahidi mwingine zaidi kwamba kuna mambo ambayo sote tunaweza kuyafanya kupunguza hatari ya kupata ugonjwa, huku asilimia 34 pekee ya watu wazima wakidhani kuwa hili linawezekana," anaongeza:

"Japo hatuwezi kubadili Jeni tulizorithi, utafiti unaonyesha kuwa kubadili mtindo wetu wa maisha bado kunaweza kusaidia kuleta mabadiliko ya mambo mabaya kwa ajili ya manufaa yetu." **BBC**

JE, WAJUA?

# Wenza wapata watoto wao waliopandikizwa kimakosa



Juu ni godoro lililochakaa. Chini; Godoro jipya. **PICHA: MTANDAO.**

WENZA wenye asili ya Asia ambao walijaribu kupata watoto kwa njia ya kupandikiza (IVF), wamedai kuwa kumetokea mkanganyiko katika hospitali ya jijini California nchini Marekani, mkanganyiko uliofanywa wapate watoto wasio wao.

Mashtaka yaliyofunguliwa na wenza hao katika jiji la New York, yanasema wawili hao walipata mshtuko baada ya kuzaa watoto wawili wa kiume ambao hawakuwa na chembe yeyote ya Asili ya Asia kama ilivyo kwa wazazi hao.

Vyombo vya habari nchini Marekani, vimeripoti.

Vipimo vya vinasaba (DNA) vinathibitisha kuwa watoto hao hawakuwa na uhusiano wowote na wapenzi hao.

Hospitali hiyo haijasema chochote kuhusu shutuma hizo.

Wapenzi hao ambao wamepewa majina ya AP na YZ wanasema kwa muda mrefu walikuwa wakitafuta watoto, kisha wakatumia kiasi cha pauni 80,000 kama gharama za hospitali na kupandikiza.

Inaripotiwa kuwa baada ya kujifungua Machi 30 mwaka huu, wapenzi hao walishtuka kuona watoto ambao waliambiwa walipandikizwa kwa kutumia jeni (genes) zao, hawakuwa waliowatazamia.

Kulikuwa na dalili awali kuwa vitu havikuwa sawa baada ya kufanyiwa uchunguzi wakati wa ujauzito na kuambiwa kuwa walitegemea watoto wa kiume, ingawa madaktari waliwaambia hawakupandikiza viinitete vya kiume wakati wa matibabu yao.

Madaktari wameripotiwa wakiwaambia wapenzi hao kuwa uchunguzi huo umetoa majibu yasiyo sahihi, kabla ya kwenda kujifungua watoto wawili wa kiume.

Mbali na kuwa watoto hawakufanana na wazazi hao, watoto wenyewe pia hawakufanana.

Kwenye tovuti ya kliniki hiyo ya uzazi, iitwayo CHA imesema inatoa huduma hizo kwa umakini wa hali ya juu na huduma zilizo bora kabisa. **BBC**

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Nachingwea yapania ufaulu wa asilimia 90 darasa la saba

• Yaanzisha kambi za taaluma shule ya msingi



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango, akisalimiana na wanafunzi walioko kambini. **PICHA: SABATO KASIKA**

KAMBI za kitaaluma zimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya elimu kwa kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri kwenye mitihani yao, kwa vile wanapata muda wa kutosha kujifunza na kujisomea.

Wanafunzi ambao wamekuwa wakiwekwa katika kambi hizo maalum kwenye baadhi ya mikoa hapa nchini ni wale wa shule za msingi na sekondari, lengo likiwa ni kuhakikisha ufaulu unaongezeka.

Kwa kuzingatia hilo, kambi hizo za kitaaluma zimekuwa zikiandaliwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa elimu wakiwamo wazazi na walezi, ambao huchangia vyakula na fedha.

Mchango wao huo unawafanya wawe wadau muhimu kwenye maendeleo ya elimu kwa vile vyakula wanavyochangia na fedha wanazotoa vinatumiwa na watoto wao kambini wanapokuwa wananolewa kitaaluma.

Nachingwea ni wilaya ambayo kwa mara ya kwanza imeweka wanafunzi wa shule za msingi katika kambi za taaluma ili wajiandae kwa ajili ya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi kwa mwaka huu wa 2019.

Jumla ya wanafunzi 4,133 wa darasa la saba kutoka shule za msingi 106 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, wameingia kambini tangu Julai 9 na watakuwa huko hadi Septemba 10 mwaka huu.

Kambi hizo ambazo ni 34 zimewekwa maeneo mbalimbali ya kata za Nachingwea, ambapo Mkuu wa wilaya hiyo, Rukia Muwango, ametoa Sh. milioni moja kama mchango wake kwa ajili ya kufanikisha kambi hizo.

"Tunataka watoto wetu wasipoteze muda kwa mambo yasiyowahusu, ndio maana tumewaweka katika kambi ili wapate muda wa kutosha kujiandaa na mtihani wa mwisho wa darasa la saba," anasema.

Muwango pia anatoa wito kwa walimu kufundisha kwa kufuata ratiba waliojiwekea na wawe walezi wazuri wa watoto ili kambi hizo ziweze kuwa na matunda mazuri hapo baadaye.

"Pamoja na mimi kuchangia, ninawaomba wadau wengine wa elimu kujitolea vilevile kwa hali na mali, kwani bado tuna upungufu wa vyakula na mahitaji mengine muhimu," anasema.

### MARATAJIO BAADA YA KAMBI

Makwasa Bulenga ni Ofisa Elimu Msingi, Wilaya ya Nachingwea, ambaye anasema wanatarajia ufaulu wa asilimia 90 katika mtihani wa mwaka huu kwa maandalizi wanayoyafanya.

"Hayo ndio makisio yetu, kwani matokeo ya mwaka jana, jumla ya wanafunzi 3,611, wavulana wakiwa 1,667 na wasichana 1,944 walifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi... waliofaulu walikuwa ni 2,669, wavulana wakiwa 1,260 na wasichana 1,409... matokeo hayo yalikuwa ni ufaulu wa asilimia 73.91," anasema Bulenga.

Anabainisha kwamba, kabla ya kuweka kambi za kitaaluma mwaka huu, Nachingwea imekuwa ikishika namba tatu kimkoa kati ya wilaya sita za mkoa wa Lindi.

"Nina uhakika kambi hii itatunyanyua nafasi za juu...ni mara ya kwanza kuweka kambi kwani tulikwama kuanza miaka ya nyuma kutokana na changamoto mbalimbali zikiwamo za baadhi ya wananchi kutoona umuhimu wa kambi hizo na hivyo kujiweka pembeni," anasema.

Bulenga anasema wazazi wameelimishwa na sasa mwitikio wao katika uchangiaji wa kambi za kitaaluma unaridhisha, kwa vile hadi sasa zaidi ya asilimia 80 wamekamilisha michango yao.

"Mtazamo wa wazazi kuhusu kambi hizi ni chanya, kwani wengi wao wamechangia vyakula, kuanzia mahindi, maharage au mbaazi na sukari kwa ajili ya watoto wao watakaokuwa kambini kwa muda wa miezi miwili," anasema.

### CHANGAMOTO ZA ELIMU

Kiongozi huyu wa elimu anasema, kuna changamoto kadhaa zinazoendana na mazingira ya uendeshaji wa vituo hivyo, baadhi yake ikiwa ni uhaba wa walimu shuleni, hali inayosababisha wanafunzi kutopata maarifa yanayohitajika kwa ukamilifu.

"Tumeanzisha kambi ili walimu wa shule mbalimbali, wale ambao ni mahiri kufundisha wanafunzi waweze kutoa mchango wao kwenye kambi hizo kwa ajili ya kuwaandaa vizuri wanafunzi wetu," anasema.

Anaongeza kuwa upungufu wa miundombinu ikiwamo ya madarasa umekuwa ukisababisha wengi wa wanafunzi kusongamana darasani na hivyo kuwafanya wakose usikivu na ufuatiliaji wa vipindi.

Changamoto nyingine anayoitaja Bulenga ni ile ya baadhi ya wazazi na walezi kuwashawishi watoto wao kufanya vibaya katika mtihani wa mwisho kwa kisingizio cha kutoweza kuwagharimia elimu ya sekondari.

Anafafanua kuwa hatua ya kuweka kambi hizo inawafanya wazazi na walezi wenye mawazo hayo kutopata nafasi ya kuwashawishi watoto wao kwa lengo la kutaka wafanye vibaya kwenye mtihani.

"Kwa utaratibu tuliouweka ni kwamba, tumewaweka kambini wanafunzi wote wakiwamo wale ambao bado wazazi wao hawajachangia chochote, huku tukiendelea kuhamasisha michango zaidi," anasema.

> Tunataka watoto wetu wasipoteze muda kwa mambo yasiyowahusu, ndio maana tumewaweka katika kambi ili wapate muda wa kutosha kujiandaa na mtihani wa mwisho wa darasa la saba.

### WABUNIFU WA KAMBI ZA TAALUMA

Mkoa wa Simiyu ni moja ya mikoa iliyobuni kambi hizi kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa elimu na kufanikiwa kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa sekondari mkoani humo hadi kushika nafasi ya 10 kitaifa.

Hiyo ilikuwa katika matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita mwaka 2018, kutoka nafasi ya 26 mwaka 2017.

Wadau waliofanikisha matokeo hayo ni viongozi na watendaji wa serikali ngazi ya mkoa na wilaya, wakuu wa shule na walimu wa shule za sekondari za kidato cha tano na sita.

Pia wadhibiti ubora, maofisa elimu wilaya na kata, wenyeviti wa bodi za shule, viongozi wa dini na viongozi wa chama cha walimu.

Kufanikiwa kwa kambi za taaluma kumesababisha wilaya na mikoa mbalimbali nchini kuiga utaratibu huo ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Mojawapo ni wilaya zilizoiga mpango huo mzuri ni Nachingwea ambayo kwa mara ya kwanza imeweka wanafunzi wa shule za msingi ambao sasa wako kambini wakinolewa kwa ajili ya kufanya Mtihani wa Taifa wa kuhitimu darasa la saba.



WADAU SABATO KASIKA

# Sauti za wadau

KWA mara ya kwanza, Sekondari za Kata 52 zimeingia katika shule 100 bora kwenye matokeo ya kidato cha sita ya mwaka huu.



**AKAROLY GODFREY (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SEKONDARI za kata bado zina changamoto nyingi, ambazo kila mmoja wetu anazijua na nyingine ziko ndani ya uwezo wetu sote kama jamii na wadau wa elimu kwa ujumla, lakini ndani ya changamoto, bado kuna baadhi ya shule zimeingia katika shule 100 bora kwenye matokeo ya kidato cha sita mwaka huu.

Hii inaonyesha kuwa sasa jamii imeanza kutambua wajibu wa kujali elimu, lakini vinginevyo zingeendelea kufanya vibaya. Pia matokeo hayo yawe chachu ya kuzidi kuboresha shule hizo badala ya kuridhika na kudhani kwamba sasa mambo yanakwenda vizuri.


Ikumbukwe kuwa umbali mrefu kati ya shule za sekondari za kata na makazi ya wanafunzi umechangia kwa kiasi kikubwa kuwafanya wanafunzi wawe na matokeo mabaya kila mwaka.

Hapa inahitajika kujengwa mabweni ya kutosha iwe ni kwa ushirikiano wa serikali na wazazi.

Kwa upande wa wanafunzi, wanatakiwa kujitahidi kujisomea bila kujali mazingira waliyomo, bali watambue kuwa wanachotafuta ni elimu, hivyo wawe na moyo wa kupenda shule ingawa zina uhaba wa vitu mbalimbali au uhaba wa walimu.

Wao wanatakiwa kuwa na juhudi za ziada za kutafuta elimu badala ya kusubiri kufundishwa darasani tu.

Wakiwa na moyo huo, sekondari za kata zitaendelea kufanya vizuri na hatimaye kupendwa na watu wengi.



**VICTORIA JOHN (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**


MATOKEO ya kidato cha sita ya mwaka huu yamezipa heshima sekondari za kata ambazo tangu zianzishwe zimekuwa zikidharauliwa sana, kutokana na jinsi, ambavyo zimekuwa zikifanya vibaya na hata baadhi ya wanafunzi kudaiwa kuingia sekondari bila kujua kusoma na kuandika.

Kwa hali kama hiyo ni vigumu kupenda shule kama hizo. Kwa matokeo hayo sasa kuna haja ya kuendelea kuziboresha ili ziendelee kuwa na matokeo mazuri zaidi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Tangu kuanzishwa kwa shule hizo, wahitimu wengi wamekuwa wakiambulia ufaulu hafifu.

Hili suala la ufaulu hafifu athari zake ni kubwa ikiwamo wahitimu kukosa fursa katika sekta rasmi, huku wengine wakikosa kabisa sifa ya kupokelewa katika taasisi za juu za elimu na mafunzo. Kwa hiyo matokeo yanapoanza kuwa mazuri ni muhimu sasa kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto ambazo zimekuwa zikiwasumbua wanafunzi.

Imekuwa ni kawaida wanafunzi kutembea umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni kwa miguu, lakini kutokana na hali ya uchumi ya wazazi na walezi ya kutokuwa na kipato cha kutosha, hushindwa kumudu gharama ikiwamo ya nauli za bodaboda na matokeo yake wanafunzi wa kike hujikuta kwenye mtego wa mahusiano ya kimapenzi na madereva wa bodaboda, mwisho wake ni kupata mimba na kukatisha masomo.

Ninatamani kila sekondari ya kata iwe na mabweni ili wanafunzi waondokane na changamoto zinazoweza kukatisha ndoto zao.



**HAMZA NIZAR (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NINAAMINI kwamba wengi wetu tumesoma katika shule za kata na zimesaidia sana kutuweka sawa kielimu kama wahitimu wa sekondari.

Zilianza zikiwa na matatizo mengi, lakini angalau zimetufikisha hapa tulipo kwa kupata elimu ya sekondari ambayo sasa inatusaidia kuendesha maisha.

Pengine wengine tungehitimu elimu ya msingi na kubaki nyumbani. Ninaheshimu sana uamuzi wa serikali wa kuanzisha shule hizi, imesaidia vijana wengi, ambao sasa wamekuwa wakijishughulisha kwa kufanya biashara mbalimbali.

Kuanzishwa kwa shule za kata kumesaidia kuibua hata vipaji vya vijana ambavyo wasingeweza kuvionyesha iwapo wangeishia elimu ya msingi. Serikali ilikuwa na maana nzuri sana kuzianzisha, lakini tatizo lilikuwa ni mpango kazi wa kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya wanafunzi na walimu.

Lakini sasa mwelekeo ni mzuri hasa kufuatia baadhi ya shule kufanya vizuri na kuleta ushindani kwenye elimu. Kilichofanywa na shule 52 za kata kwenye matokeo ya kidato cha sita mwaka huu kiwazindue wazazi ambao wamekuwa wakidharau sekondari za kata au kutotambua umuhimu wa kuwapo kwa shule hizi.

Ninaamini kwamba elimu bora ya watoto wa Kitanzania ndio lengo la kila mzazi anayethamini elimu.



**SIMON NDALLU MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM**

SASA ni wazi ile dhana kwamba shule zote za kata ziko katika mazingira magumu na hazifanyi vyema katika maendeleo ya elimu siyo sahihi.

Kwani ingawa shule nyingi za kata hazifanyi vyema na zinakabiliwa na changamoto nyingi, zipo baadhi ya shule za sekondari za kata zenye maendeleo mazuri kitaaluma hata kuzidi zile kongwe za serikali zikiwamo pia za binafsi.

Mojawapo ya shule za kata ni zile ambazo zimefanya vizuri katika matokeo ya kidato cha sita ya mwaka huu na kuingia katika 100 bora na sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo amewahakikishia wazazi na walezi kwamba siyo wakati wa kuwasumbua watoto wao kwa kuwahamisha shule za serikali na kuwapeleka binafsi, kwasababu kila kitu kinakwenda vizuri.

Anawahakikishia kuwa sekondari za kata zimeanza kufanya vizuri baada ya changamoto za muda mrefu ambazo zilichangia kuzifanya kama hazifai kutatuliwa kwa kiwango kikubwa.

Ninakubaliana naye kwamba zilikuwa katika kipindi cha mpito, sasa zinaelekea katika mazingira ambayo kila Mtanzania atazipenda, kwani serikali imefanya uwekezaji mkubwa hadi kufikia baadhi yake kuwa na matokeo mazuri ya mtihani wa kidato cha sita. Serikali inasema shule zake zimefanya vizuri ikilinganishwa na ufaulu wa kipindi cha nyuma ambacho zilikuwa ni kama mzigo usiobebeka, lakini ninadhani sasa zimeanza kubadilika na kutoa wahitimu walioiva kielimu.



**NURU KITAMBO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SIYO siri kwamba sekondari za kata zina changamoto lukuki, nyingine zina mazingira magumu ambayo wanafunzi wakifika na kuona hukimbia. Baadhi zina upungufu wa walimu, nyumba za walimu na upungufu mwingineo.

Hata hivyo, bado zimejitahidi kwani kati ya shule 100 bora, 52 ni za kata. Hizo zote ni juhudi za serikali na wadau wa elimu, zimefanikisha sekondari za kata kuanza kuwa na matokeo mazuri na inawezekana huo ukawa ndio mwanzo wa kuzifanya zizidi kung'aa na kupata umaarufu mkubwa nchini.

Sasa ni wajibu wa wanafunzi kuongeza bidii katika masomo hata kama bado kuna mazingira, ambayo yanachangia shule hizo zisiwe na ufaulu mzuri.

Lakini jambo moja wajue kuwa bado wana nafasi ya kuongeza bidii katika masomo, ili mwisho wa siku waweze kufaulu.

Shule za kata zina umuhimu hasa kutokana na ukweli kwamba hata kama bado zina changamoto, wanafunzi wanahitaji kupata elimu.

Hivi kweli kama shule hizi zisingekuwepo watoto wangekwenda wapi? Hivyo hata kama zipo zile ambazo hazifanyi vizuri, ni bora kuliko watoto kuhitimu elimu ya msingi na kukaa nyumbani.

Kwa kawaida mwanzo huwa ni mgumu kama ilivyotokea kwenye shule hizi, lakini sasa baadhi zimeanza kufanya vizuri.



## RC apongeza wazee kwa ushirikiano naye

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewashukuru wazee mkoani hapa kwa ushirikiano wanaoutoa kwa serikali katika kuhakikisha mkoa unaendelea kuwa na amani na mshikamano na hatimaye kuwaletea wananchi maendeleo.

Chalamila alitoa shukurani hizo juzi alipokutana na kufanya kikao na wazee zikiwa zimebaki siku chache kutimiza mwaka mmoja tangu alipoteuliwa na Rais kushika wadhifa huo.

Alisema katika kipindi chote cha utendaji kazi wake, amekuwa akiungwa mkono na wazee hao wenyeji kwa kupewa ushauri na kushirikiana naye katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

"Nimefurahi sana kukutana nanyi wazee wangu. Kila wakati nimekuwa nikitafuta fursa ya kukutana nanyi ili kuwashukuru kwa moyo wenu na bidii katika kuunga mkono shughuli zote za kufanya maendeleo. Mmekuwa watu muhimu sana kwangu kwa sababu mnajua mwelekeo wa taifa letu," alisema Chalamila.

Pia Chalamila alisema kupitia ushirikiano huo, mkoa wa Mbeya umekuwa na mabadiliko mengi kwa muda mfupi ikiwamo ongezeko la ukusanyaji wa mapato, kupunguza uhalifu, ukuaji wa elimu na utendaji wa watumishi wa sekta mbalimbali kuboreka.

Alisema pia uchumi wa mkoa huo umekuwa ukikua kwa kasi kutokana na ushirikiano wa wananchi wakiongozwa na wazee hao ambao wamekuwa wakiwahamasisha.

Alisema tangu walipotekeleza agizo la Rais Magufuli la kufungua soko la madini, mkoa huo umeuza zaidi ya kilo 250 za madini na serikali imepata Sh. milioni 64 ikiwa ushuru wa bidhaa hiyo.

Aidha, aliomba ushirikiano huo ili kufikia azma yake ya kuendeleza utu, nidhamu na uadilifu katika utendaji wa watumishi mbalimbali wa sekta zote na kufikia lengo la kukuza uchumi na maendeleo kwa kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano.

Mwenyekiti wa wazee hao, Isakwisa Mwambulukutu, alisema umoja huo unampongeza Rais John Magufuli kwa utendaji wake kwa madai kuwa anafanya kazi kubwa ambayo haikutarajiwa.

Vilevile alimpongeza Chalamila kwa kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za maendeleo huku akisisitiza kuwa wataendelea kushirikiana naye ili maendeleo ya mkoa huo yaendelee kuwa juu.

# Jukwaa laundwa kupaisha alizeti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa alizeti mkoani Mbeya wameunda jukwaa maalumu la kushughulikia changamoto zinazolikabili zao hilo ili kuongeza uzalishaji na kuliwezesha taifa kupunguza kiwango cha uagizaji wa mafuta ya kupikia kutoka nje.

Jukwaa hilo liliundwa mwishoni mwa wiki kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) kupitia mradi wake wa uboreshaji wa mifumo ya masoko katika maziwa na alizeti (Tam).

Ofisa Mshauri wa Sera katika mradi huo nchini, Renatus Mbamilo, alisema jukwaa hilo linawahusisha wadau mbalimbali wakiwamo wakulima wa alizeti, wazalishaji wa mbegu, wafanyabiashara wa zao hilo na mafuta pamoja na wasindikaji wa mafuta ya alizeti.

Mbamilo alisema jukwaa hilo litazinduliwa mwishoni mwa mwezi huu jijini Mbeya na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, pamoja na kuwasimika rasmi viongozi wa muda waliochaguliwa.

Alisema lengo la kuanzisha jukwaa hilo ni kuboresha uzalishaji wa alizeti kwa kuwafanya wadau kuwa na sauti moja ili kuhakikisha zao hilo linazalishwa kwa ubora na kibiashara tofauti na ambavyo linazalishwa kwa mazoea. "Tumeamua kuanzisha majukwaa haya kwa sababu tumebaini kuwa yana tija kubwa, yanawaleta wadau pamoja, yanawasaidia kujifunza vitu mbalimbali pamoja na kuzibaini kwa pamoja changamoto zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi," alisema Mbamilo.

Alisema mbali na jukwaa hilo, pia yako majukwaa mengine ambayo yameshaundwa likiwamo jukwaa la wadau wa maziwa katika Mkoa wa Kilimanjaro ambalo alisema linafanya vizuri katika kuendeleza sekta ndogo ya maziwa.

Naye Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Mbeya anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji, Said Madito, alisema katika mkoa wa Mbeya, alizeti ni miongoni mwa mazao ya kipaumbele kutokana na umuhimu wake.

Alisema wilaya zinazozalisha kwa wingi zao hilo ni Chunya na Mbeya ambayo inazalisha kiwango kidogo na kwamba viwanda vya kusindika mafuta ya zao hilo vinapatikana zaidi jijini Mbeya.

Alisema mafuta yatokanayo na alizeti yana ubora kuliko mafuta mengine na kwamba yanahitajika sana duniani licha ya uzalishaji wake kuwa mdogo kuliko mahitaji.

Alisema zaidi ya asilimia 66 ya mafuta ya kupikia yanayotumika nchini yanaagizwa kutoka nje ya nchi na kwamba jukwaa la wadau linaweza kusaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kuongeza kiwango cha mafuta ili kupunguza kiwango cha uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje.

Madito alisea asilimia 16 mpaka 18 ya mafuta yote yanayotumika duniani yanatokana na alizeti na kwamba mafuta hayo yana soko kuliko aina zingine.

"Tunataka jukwaa hili liwe chachu ya uboreshaji wa zao hili katika Mkoa wetu, hata teknolojia za usindikaji tunataka ziboreshwe kama ilivyo kwa mikoa ya Singida na Dodoma ambayo ndiyo inayoongoza," alisema Madito.

Kwa upande wake, Ofisa Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, alisema biashara ya alizeti katika Mkoa wa Mbeya ni kubwa na kwamba uzalishaji uko chini kuliko mahitaji ya soko.

Aliwataka wakulima watumie fursa ya soko hilo kuongeza uzalishaji ili kujiinua kiuchumi kwa kuzalisha zaidi pamoja na kuepuka kuuza zao hilo likiwa ghafi.



Wanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya St Anne Marie Academy ya Mbezi kwa Msuguri, wakimpongeza mwenzao, Maria Shuma, aliyepata daraja la 1.7 kwenye mtihani wa majaribio (Mock) uliofanyika hivi karibuni na shule hiyo kufanikiwa kuwa ya sita kwa Mkoa wa Dar es Salaam kati ya shule 302. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka sheria ya ununuzi ifumuliwe

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Elius Mwakalinga, ameshauri Wakala wa Taifa wa Barabara (Tanroad) kupitia upya Sheria ya Ununuzi (PPA) kwa kile alichoeleza kuwa baadhi ya vipengele vyake havina tija.

Mwakalinga alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wilayani Rungwe, alipokuwa anazungumza na kampuni na vikundi vya makandarasi wanaofanya kazi za ukarabati na usafi wa barabara. Alisema baadhi ya vipengele vya sheria hiyo vinawabana makandarasi hasa wazawa.

Alitoa ushauri huo kutokana na malalamiko ya baadhi ya makandarasi ambao walidai kuwa Tanroads inawanyima kazi za barabara kwa kisingizio cha sheria ya ununuzi.

"Ili kuondoa malalamiko haya kwenye mikataba yetu kuna matatizo itabidi tukae wizara, bodi ya barabara na Tanroads kuangalia upya sheria hii kwani inawapa makandarasi wa kigeni nafasi kubwa ya kupata kazi kuliko wazawa," alisema Mwakalinga.

Mwakalinga aliwashauri makandarasi wazawa kuwa wabunifu na kuungana na makandarasi wakubwa na kubuni miradi mingine badala ya kuendelea kulalamika kunyimwa kazi na Tanroads.

Mkurugenzi wa Barabara nchini, Mhandisi Rogatus Malavila, alisema serikali kupitia mkakati wa kukuza na kuinua matumizi ya teknolojia stahiki na nguvu kazi, inatekeleza sera na mipango mikakati mbalimbali ambayo inalenga kuwa na matumizi bora ya teknolojia.


Alisema teknolojia hiyo itakuwa inatumika kwenye ukarabati wa barabara, madaraja na majengo ambapo alidai itasaidia kupatikana kwa ajira kwa makandarasi hao.

Baadhi ya makandarasi wa matumizi ya teknolojia stahiki na nguvu kazi walilalamikia Tanroads na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijni (Tarura) kuwa taasisi hizo zina urasimu katika kuwapatia kazi na badala yake wanawapatia makandarasi wakubwa.

Meneja wa kampuni ya visima kutoka mkoa wa Morogoro, Villa Majitaka, alisema serikali inawatambua makandarasi hao, lakini kila wakienda kuomba kazi za kutekeleza baadhi ya miradi, zinanyimwa.

"Sisi tunatambuliwa na serikali na tunalipa kodi lakini kila tukiomba kazi tunanyimwa na badala yake wanapewa makandarasi wakubwa pekee. Hali hii inatupa wakati mgumu na tunashindwa hata kulipia kampuni zetu kwa kukosa fedha," alisema Majitaka.

Aliongeza kuwa makandarasi wa teknolojia stahiki na nguvu kazi jukumu lao ni kukarabati madaraja, majengo na barabara lakini kwa sasa kazi hizo wanapewa makandarasi wakubwa ambao wanatakiwa kutekeleza miradi mikubwa.





# Vijana waomba fursa uchaguzi ujao

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeombwa kutoa fursa kwa vijana kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu ujao 2020, kama ambavyo Rais John Magufuli, ameamua kuwaamini katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), wilayani Bahi, Hassan Kadoke, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema vijana wamejipanga katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kumpa kura zote Rais Magufuli kutokana na kazi iliyotukuka anayoifanya kwa Watanzania wote bila kujali itikadi za chama.

Kadoke alisema wao kama vijana kwa sasa wanatembea kifua mbele kutokana na kazi kubwa inayofanywa na Rais Magufuli pamoja na wasaidizi wake.

Alisema viongozi hao wamekuwa wakijenga heshima kwa nchi na chama kwa kuhakikisha wanasimamia falsafa na misingi ya CCM kwa kuimarisha mshikamano kwa Watanzania.

Mwenyekiti huyo alisema Wilaya ya Bahi tangu ianze imekuwa haina kituo cha afya hivyo serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi huo.

"Tuseme nini tena ujenzi wa hospitali ya wilaya unaendelea ujenzi wa vituo vya afya vinne unaendelea, huu ni mtaji mkubwa kwetu wakati tukielekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, tuna imani CCM itashinda kwa kishindo," alisema.

Aliyekuwa mgombea ubunge kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) 2015, Mathias Lyamunda, ambaye kwa sasa amejiunga na CCM, alisema amerudi kwa mapenzi yake kwa Rais Magufuli.

Alisema mpaka anarudi CCM alifanya uchunguzi wa kina kwa zaidi ya miaka mitatu hivyo kuridhishwa na utendaji kazi wa Rais Magufuli.

"Nachosema Magufuli ndicho anachotenda unabaki upinzani unafanya nini mimi sijashawishiwa na mtu yeyote kumbuka mimi ni kijana, lakini naiona nuru ya CCM, yale niliyokuwa nikiyaomba wakati wa kampeni mwaka 2015 mengi Rais ametayekeleza kwa vitendo," alisema Lyamunda.

Vile vile, Lyamunda aliwataka vijana kuchangamkia fursa kwa kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

"Sioni ushindi kwa wapinzani kwetu Bahi nina imani katika vijiji 59 na vitongoji 200 kote huko tutashinda tena kwa kishindo katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu," alisema.

# Waonywa kujisaidia vichakani

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

WAKAZI wa vijiji vya wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma wameonywa tabia ya kujisaidia vichakani na kutakiwa kujenga vyoo vyenye ubora ili kuepukana na magojwa ya mlipuko.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Askofu wa Kanisa la Pentecoste Holiness Association Mission Tanzania (PHAM) (T), Julias Bundala, alipokuwa akizungumza na waumini wa madhehebu mbalimbali katika Kijiji cha Mlali, wilayani hapa.

Bundala alisema, ujenzi wa vyoo vya kisasa utasaidia kuepuka magonjwa ya milipuko kama watavitumia katika maeneo yao.

"Kwa kweli hapa lazima nisema karibu wakazi wengi katika vijiji vya wilaya hii vyoo vyao havina hadhi na havistahili kutumiwa kwa kuwa vinaweza vikahatarisha maambukizi ya magonjwa, lakini pia wengine wanajisaidia porini," alisema.

Alisema kuwa ni wakati sasa wa wakazi hao kubadilika katika matumizi hayo yaliyopitwa na wakati na kuiunga mkono serikali ambayo imekuwa ikisisitiza kuwapo kwa afya bora kwenye jamii.

"Ninawaomba jengeni vyoo imara badala ya kuvijenga vyoo ambavyo kuta zake zinaishia nusu mtu akiingia mwili mzima uko wazi kwa kweli kwa upande wa waumini wangu sipendi kuona vyoo hivyo," alisema.

Aliwataka wachungaji wa kanisa hilo kuhakikisha wanakuwa na vitambulisho, Katiba na vyeti vya usajili kwa kuwa watakuwa wamejiweka wazi kwa wakati huu serikali ilivyoanza kuhakiki madhehebu ya dini.

Alisema hivi karibuni serikali imetangaza azima yake ya kufanya uhakiki wa madhehebu ya dini, hivyo ni muhimu kila mchungaji akazingatia hilo.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo kuepuka na imani ambazo zimekuwa zikinyoshewa vidole ambazo zimekuwa zikipotosha jamii.



Wanafunzi wa ushonaji kituo cha Mama Arno, Mji Mdogo wa Kibaigwa mkoani Dodoma, wakifanya mafunzo kwa vitendo kituoni hapo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wajasiriamali nchini wapewa somo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAJASIRIAMALI nchini wametakiwa kushiriki mafunzo yanayotolewa na Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), ili kuwasaidia kuongeza ujuzi kwenye bidhaa wanazotengeneza ziweze kuleta ushindani katika soko la kimataifa.

Hayo yalisemwa na Meneja wa SIDO Mkoa wa Dodoma, Sempeho Manongi, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu wajasiriamali wadogo wanaotengeneza bidhaa kwa lengo la kuziuza katika maeneo tofauti.

Alisema pamoja na kuwa wana ujuzi, lakini wanapaswa kuendelea kupata mafunzo mengine toka SIDO kwa sababu yatawajengea uwezo mkubwa wa kuweza kushindana na wafanyabiashara kutoka nchi jirani.

"Nawaomba wajasiriamali wajitokeze katika mafunzo, tunahita kuona wengi wanashiriki katika maonyesho ya kimataifa ili kutangaza bidhaa zao pamoja na taifa kwa ujumla," alisema Sempeho.

Alifafanua kuwa hivi sasa taifa linaingia katika uchumi wa viwanda kwa hiyo wajasiriamali wanapaswa kutumia fursa ya mafunzo yanayotolewa na SIDO ambayo yatawasaidia kuingia katika maonyesho ya kimataifa.

Alisema kuwa hakuna sababu ya wao kubweteka wanachotakiwa ni kutumia fursa za mafunzo mbalimbali yanayotolewa ili waweze kufanya mabadiliko katika biashara wanazofanya.

Alisisitiza wajasiriamali kuwa na nembo ya TMDA ambayo itawasaidia kupanua soko la nje na ndani ya nchi kulingana na bidhaa wanazofanya kwa sababu itawasaidia kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya biashara.

Manongi alisema nembo ya TMDA itawasaidia kupata masoko makubwa katika bidhaa wanazotengeneza na kuuza kutokana na kwamba bidhaa zao zitakuwa na viwango vyenye ubora.


"Nawaomba mjitahidi kuwa na nembo za TMDA mkifanikiwa kuwa na nembo hizo itawasaidia bidhaa zenu kujulikana kutokana na kwamba mtakuwa mnashiriki katika maonyesho mbalimbali ya kimataifa ya kibiashara," alisema Manongi.

Alisema serikali ya awamu ya tano inasisitiza viwanda, hivyo ni vema wajasiriamali wakawa na nembo hiyo ili kujitanua kibiashara na kufika mbali kwa kile wanachokifanya.

Alieleza wao kama SIDO lengo lao ni kuona kila mjasiriamali anakuwa na nembo katika bidhaa zake ambazo zitawasaidia kuendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano inayosisitiza uchumi wa viwanda.

Vile vile, alisema wajasiriamali wanapaswa kutobetweka na kile wanachokifanya hivi sasa na badala yake wajiongeze katika mafunzo ili waweze kusonga mbele katika biashara wanazofanya.

## HABARI ZANZIBAR





Meli ya MV Mapinduzi namba mbili ikiwa imefunga nanga katika Bandari ya Malindi, baada ya kusitisha safari yake ya kwenda Pemba, kutokana na injinia ya meli hiyo, Haji Abdullah Khatib, kudaiwa kujinyonga wakati boti hiyo ikiwa safarini. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sekta ya elimu yaboresha fani ya Sayansi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema Serikali ya Zanzibar imeanza kuonyesha kwa vitendo utekelezaji wa msingi ya uimarishaji wa miundombinu katika sekta ya elimu kwenye fani ya Sayansi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia yaliyopo ulimwenguni.

Alisema utekelezaji huo umezingatia mwelekeo wake katika ujenzi wa majengo 24 ya maabara ya Sayansi (School Hurb), katika visiwa vya Unguja na Pemba yatakayojikita na masomo ya Kemia, Fizikia na Biologia.

Balozi Iddi alisema hayo kisiwani Pemba wakati akikagua miradi ya maendeleo pamoja na ufuatiliaji wa mashamba na heka tatu ambazo bado haliko kwenye miliki ya serikali.

Alisema wakati umefika kwa wanafunzi wa shule za sekondari Unguja na Pemba kuchangamkia fursa hiyo ambayo katika siku za baadae itaziba pengo la upungufu wa wataalamu wa fani ya sayansi nchini.

Balozi Iddi alisema ameridhika na kiwango kizuri cha ujenzi kilichofikiwa na wahandisi wa majengo hayo kampuni ya kizalendo ya Salim Contructor na kuzitaka kampuni nyingine zitakazopewa jukumu la ujenzi wa majengo ya serikali na taasisi za umma kuzingatia ubora wa kiwango kinachokubalika.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa maabara ya sayansi ya Shule ya Kilindi, Ofisa Mdhamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Mohamed Nassor, alisema maabara hiyo ni miongoni mwa majengo 24 yanayoendelea kujengwa katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar. Mohamed alisema Maabara ya Sayansi (School Hurb) yameanzishwa kama vituo vya kutoa huduma katika masomo ya sayansi likiwamo pia somo mama la Kiingereza kwa wanafunzi hasa walioko vijijini ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakikosa fursa hizo. Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba, Hemed Suleiman Abdulla, alisema wananchi wa mkoa huo wanafurahia maendeleo makubwa yanayopatikana chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein.

Alisema huduma za majisafi na salama, umeme, barabara za lami pamoja na miundombinu ya miradi ya kiuchumi imekuwa ikileta matumaini ya kuongezeka kwa kipato cha wananchi hao jambo ambalo limestawisha maisha yao ya kila siku.

Hemed alisema wananchi wana kila sababu ya kujivunia maendeleo hayo makubwa yanayoonekana kila pembe katika dhana nzima ya utekelezaji wa vitendo wa ahadi zilizotolewa na Serikali ikiwamo kuwasili kwa vifaa vya kutengenezea miundombinu ya mawasiliano Kisiwani Pemba.

# Tamwa yatoa ushauri kwa serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa) upande wa Zanzibar, kimeishauri Serikali kuboresha miundombinu ya utendaji wa jeshi la polisi ili liweze kufanya kazi zake kwa weledi na ufanisi na kuhakikisha haki inatendeka kwa wakati mwafaka.

Kauli hiyo imetolewa na Meneja utetezi wa chama hicho, Hawra Shamte, wakati akitoa taarifa ya utafiti kuhusiana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto kwa vyombo vya habari. Alisema hatua hiyo itasaidia kesi za ukatili kwa wanawake na watoto kusimamiwa ipasavyo. "Jumla ya kesi tano za mauaji ya wanawake zipo katika vituo vya polisi na watuhumiwa bado hawajapatikana," alisema.

Alisema kuwa kesi hizo ni zile ambazo matukio yake yalifanyika kuanzia mwaka 2016 hadi 2019, katika maeneo tofauti ya Zanzibar, huku kesi tano zikiwa zipo polisi, moja kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na tatu zimefutwa.

Alisema, Zanzibar kuna sheria nzuri za makosa ya jinai, tatizo lipo katika utekelezaji wa sheria hizo, hivyo ni wajibu wa watekelezaji wa sheria kuhakikisha kuwa zinafanyiwa kazi.

Alizitaja kesi ambazo zipo mahakamani ni ya kuuawa kwa Samira Sultan Abdalla, ilitokea Juni 2017, huko Kiembesamaki, ambaye mifupa yake ilikutwa katika shimo la karo na kesi ipo Mahakama ya Vuga kwa ajili ya kutolewa ushahidi.

Kesi nyingine ni ya Wasila Mussa, aliyeuawa Julai 18, 2018 huko Tunguu, uchunguzi wa awali umekamilika na kesi imeanza kusikilizwa.

Vile vile, alisema kesi ya tatu ambayo ipo mahakamani ni ya mtoto wa miezi tisa, Arman Mohammed Hassan, aliekutwa ameshafariki dunia huko Fuoni akiwa anaelea katika ndoo ya maji, kesi hiyo ilitokea Oktoba 2017, ipo katika Mahakama ya Vuga, inasubiri ushahidi.

Naye Mkurugenzi wa chama hicho, Dk. Mzuri Issa, alisema utafiti huo uliofanywa na Tamwa umelenga kumkomboa mwanamke na mtoto dhidi ya vitendo hivyo na kuhakikisha vinaondoka nchini.

# Elimu uhifadhi mazingira yahitaji nguvu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, Abeid Juma Ali, amesema jitihada zinahitaji kuongezwa katika utoaji elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa jamii.

Sheha wa Shehia ya Mwakaje, Asha Ali Mohammed, aliyasema hayo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, baada ya zoezi la upandaji miti pamoja na utoaji wa elimu ya mazingira lililoandaliwa na mradi wa maendeleo kwa jamii (RAA) kutoka Ujerumani, lililofanyika Shule ya Mtopepo wilaya ya magharibi 'A' Unguja.

Alisema kuna tatizo la uharibifu wa mazingira hasa maeneo ya bahari na kusababisha kuharibu viumbe vya bahari ikiwamo samaki na matumbawe hali inayosababisha kuua samaki kwa upande wa bahari.

Alisema kuna utupaji ovyo wa taka na chupa, hivyo aliwasishi wananchi na wafanyabiashara kuzihifadhi vizuri ili kuhakikisha haziathiri mazingira.

Aliwaomba kila mmoja kutumia nafasi yake kuhakikisha anasafisha maeneo yake anayoishi ili kuepuka athari za mabadikilo ya tabianchi.

Alisema iwapo jamii, walimu na wanafunzi watakuwa waadilifu katika kuhamasika kufanya usafi kutaepusha maradhi mbalimbali yanayoweza kutokea ikiwamo ya mripuko.

Aliwaomba walimu, wanafunzi wa skuli ya Mtopepo kuwa na ushirikiano wa karibu na wanafunzi wa Ujerumani ikiwamo kubadilishana fursa.

Naye Diwani wa wadi ya Munduli, Juma Fikirini Khamis, alisema serikali imeanzisha vikundi vya mabaraza ya vijana ili kukusanya taka na kuzihifadhi mahala salama.

Mwenyekiti wa mradi wa maendeleo kwa jamii (RAA) kutoka Ujerumani, Birigit Mitawi, alisema lengo la mradi huo ni kutoa elimu ya uhifadhi ya mazingira ili kuhakikisha Zanzibar inaendelea kuwa salama.

Aliwashauri wananchi na jamii kwa ujumla kutumia vyakula vya matunda muda mwingi ili kutunza mazingira.

Akizungumzia matumizi ya palastiki, aliwaomba wananchi kutumia mikoba ya asili ya ukili ambazo yanapunguza athari za mazingira.

Kwa upande wao wanafunzi kutoka Ujerumani walisema Zanzibar inaweza kunusurika na mabadiliko ya tabianchi iwapo wananchi watakuwa wanapunguza matumizi ya vitu vya plastiki.

## Mawakili wa kujitegemea waaswa maadili

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

KAMANDA wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kigoma, Raphael Mbwambo, amewatahadharisha mawakili wa kujitegemea kuzingatia maadili ya taaluma zao.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini jana, alisema: "Tunawatadharisha mawakili wa kujitegemea kuzingatia maadili ya taaluma zao na kuepuka kwa namna yoyote ile kushirikiana na watumishi wasio waadilifu kwa lengo la kutaka kipato kinyume cha sheria, vinginevyo Takukuru haitasita kuwachukulia hatua za kisheria."

Aidha, aliwakumbusha wakurugenzi wa halmashauri zote za Mkoa wa Kigoma kuhakikisha watumishi wote na wao wenyewe wanapolipwa fedha za posho ya masurufu ya safari au matumizi mengine, wanafanya marejesho pamoja na kufanya uhakiki wa uhalali wa matumizi ya fedha hizo kwa mujibu wa sheria.

Aidha, alisema kukiuka kanuni na taratibu za fedha za umma, Takukuru haitasita kuchukua hatua dhidi yao pale itakapothibitika kuwa wamezembea kwa namna yoyote ile katika usimamizi wa fedha za umma au nao wameshiriki katika uvujaji huo. Pia Mbwambo aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kushirikiana na Takukuru katika kuchunguza na kuhakiki uadilifu wa wanachama wenye nia ya kuwa wagombea katika uchaguzi katika ngazi mbalimbali.

Alisema hatua hiyo itasaidia kubaini wanachama wasiyo waadilifu na kuwaengua mapema katika mchakato wa uchaguzi, wanachama wa vyama vya siasa na wananchi wote wanahimizwa kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa, wakati wa uchaguzi kwa kukemea na kukataa kushawishiwa kwa vitendo vya rushwa kabla na wakati wa uchaguzi. Aidha, alisema wanachama wanahimizwa kutoa taarifa dhidi ya watu watakao onekana kutaka kushawishi kwa njia yoyote ile kwa nia ya kujenga mazingira ya kuchaguliwa kwa kuwapa zawadi au kitu chochote, na kamwe wasikubali kutumiwa kuwapigia debe watu wenye nia ya kugombea kwa misingi ya kutoa rushwa. Alisema zaidi: "Ni vema wananchi watambue kuwa rushwa katika uchaguzi ina madhara makubwa katika maendeleo ya jamii kwa ujumla."

Alisema katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu, Takukuru imepokea jumla ya taarifa 47 ya vitendo vya rushwa na zinaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali.

# Watumishi waonywa dhidi ya siasa

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

SERIKALI wilayani Kalambo mkoani Rukwa, imewataka watumishi wa umma wilayani humo kujikita katika kuwatumikia wananchi na si kujiingiza kwenye siasa kwa sababu wananchi wanahitaji kutatuliwa changamoto zao na wakati wa siasa bado.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala msaidizi wa wilaya hiyo, Wilhem Kijazi, wakati wa kikao kazi kwa ajili ya kuwakumbusha watumishi wa umma majukumu yao mbalimbali.

Alisema kuwa muda si mrefu utafanyika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ili kuwapata viongozi wa serikali za mitaa na vijiji hivyo watumishi wa umma watambue kuwa wanajukumu kubwa la kuwatumikia wananchi na wala si kuanza kujihusisha na siasa.

Katibu tawala huyo msaidizi alisema kuwa bado kuna changamoto kubwa ambazo zinawakabili wananchi, hivyo wazishughulikie badala ya kuanza kufikilia siasa kwani wakati wake bado.

"Nichukue nafasi hii kuwakumbusha watumishi wa umma kuwa wana wajibu wa kuwatumikia wananchi ili kuziondoa changamoto walizonazo na si kuanza kufikilia siasa kwani muda bado, wao waendelee kupiga kazi," alisema.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Nicholaus Mlango, aliwakumbusha watumishi hao kuhakikisha kuwa wanajaza fomu za OPRAS ili kujipima utendaji kazi wao na kuona kuwa wanayopata wanastahili kutokana na kujaza fomu hizo.

Alisema kuwa serikali ipo makini nao na inajitahidi kutatua changamoto zao, na kinachotakiwa ni kuongeza kasi katika utendaji kazi sambamba na ubunifu ili nchi ipige hatua kwa kasi zaidi.

Kaimu mkurugenzi huyo aliwataka watumishi hao kuheshimu sheria na kuwawaadilifu katika utumishi wao kwani tofauti na hivyo, watapoteza sifa ya kuwa watumishi wa serikali kwa sababu serikali inahitaji watumishi wenye maadili.



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, akihutubia katika uzinduzi pamoja na makabidhiano ya madarasa mawili na ofisi ya walimu ya Shule ya Msingi Lusangi yaliyojengwa kwa msaada wa Kampuni ya Bima ya Sanlam kwa gharama ya Sh. milioni 49, shuleni hapo, Tarafa ya Pahi, Wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU.**

# Kibano kwa wananchi kuvamia hifadhi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewapiga marufuku wananchi kuvamia hifadhi ya Samina iliyopo Halmashauri ya Mji wa Geita na kuendesha shughuli za kuchungia mifugo na kulima.

Alisema Rais John Magufuli hivi karibuni alitoa muda kwa wakulima wote nchini waliokuwa wamevamia kwenye maeneo ya hifadhi na kuendesha shughuli za kilimo kuvuna mazao yao kisha kuondoka.

Kanyasu alitoa kauli hiyo wakati akiwahutubia wananchi kwenye mkutano wa hadhara katika Kata ya Mtakuja Halmashauri ya Mji wa Geita baada ya wakulima kuwalalamikia wafugaji kuwalisha mazao yao waliolima kwenye hifadhi ya Samina wakimtaka Naibu Waziri huyo kutatua mgogoro huo kabla haujaleta maafa.

Naibu Waziri huyo mbali na kuwapiga marufuku wananchi hususan wafugaji kuvamia hifadhi hiyo, aliwaagiza maofisa kilimo, maofisa watendaji wa kata kusimamia na kufuta sheria kwa wafugaji wanaochungia mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kuharibu mazao yao, huku akisema wanaoingia kwenye hifadhi hiyo bila utaratibu wote ni wavamizi.

Naibu Waziri huyo akijibu kero za wananchi wa kata hiyo, alisema Mji wa Geita unakua kwa kasi kubwa kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu na kusababisha uhitaji mkubwa wa matumizi ya majisafi na salaama. Alibainisha kuwa awali upatikanaji wa majisafi na salama ulikuwa ni asilimia 15, lakini sasa umefikia asilimia 55, ambapo aliwahakikishia wananchi kuwa serikali imetenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria, na iwapo utakamilika kero ya maji itakuwa historia Mjini Geita.

Kuhusu huduma ya afya, alisema serikali inatarajia kukiboresha kituo cha afya cha Kata ya Nyankumbu ambacho kinatoa huduma ya hospitali ya wilaya baada ya hospitali ya wilaya kupandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita, huku akisema kuwa mitaa yote katika Jimbo la Geita Mjini itapata umeme.

Diwani wa Kata ya Mtakuja, Constantine Molandi, akamuomba Naibu Waziri huyo kutatua kero ya ukosefu wa huduma ya maji, ukosefu wa umeme na kuboresha miundombinu ya barabara za mitaa barabara ya kutoka Mtaa wa Mbabani kwenda Nyantorotoro.

## HABARI KIMATAIFA

# Waziri wa fedha akamatwa kwa ufisadi

**NAIROBI,** Kenya

WAZIRI wa Fedha wa Kenya, Henry Rotich, amejisalimisha kwa maafisa wa upelelezi jana, muda mfupi baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka Kenya kuagiza akamatwe.

Kwa mujibu wa mtandao wa Nairobi News, Rotich alipelekwa kwa gari hadi makao makuu ya idara ya upelelezi ambako alihojiwa kuhusu malipo yaliyotolewa kwa ujenzi wa mabwawa mawili nchini.

Rotich anatuhumiwa kukiuka muongozo wa utoaji wa kandarasi iliopewa kampuni ya Italia, CMC de Ravenna yenye thamani ya zaidi ya dola milioni 450 kwa ujenzi wa mabwawa.

Hapo awali, Mkurugenzi wa Mashtaka Kenya aliagiza kukamatwa kwa Rotich na ashtakiwe kuhusu ufisadi.

Mkurugenzi huyo wa mashtaka, amekuwa akizungumza katika vyombo vya habari kuhusu uamuzi wa kumshtaki Waziri wa Fedha na maafisa wengine wa serikali kuhusu kandarasi zilizotolewa kwa kampuni ya Italia kujenga mabwawa mawili.

**Kila kesi inatuma ujumbe mzito kwa walio mafisadi... au kwa wanaovutiwa kuingia katika ufisadi... kwamba watashitakiwa...**

Noordin Haji ameeleza kwamba watashtakiwa kwa kupanga kufanya udanganyifu, kushindwa kutii muongozo unaotumika katika upatikanaji wa kandarasi miongoni mwa mambo mengine. Mashtaka hayo yanahusiana na ujenzi wa mabwawa mawili nchini uliogharimu fedha nyingi.

Imeelezwa kuwa machi mwaka huu, Waziri Rotich alikana kupitia tangazo kwenye gazeti kuhusika kufanya makosa. Hata hivyo kampuni hiyo ya Italia CMC de Ravenna pia imekana tuhuma hizo.

"Katiba yetu inasisitiza baadhi ya maadili yetu yakiwamo uadilifu... kuyatimiza husussani kwa walio uongozini... Kutimiza maadili haya ni muhimu kwa uhai wetu...Rushwa inatishia msingi wa taifa letu - ufisadi unatugawanya na kuangamiza utu" alisema na kuongeza.

"Kila kesi inatuma ujumbe mzito kwa walio mafisadi... au kwa wanaovutiwa kuingia katika ufisadi... kwamba watashitakiwa..."

Haji alieleza kuwa kashfa kuhusu ujenzi wa mabwawa hayo umewagharimu wananchi wa Kenya ambao walitoa mabilioni ya fedha kupitia makato ya kodi.

Maofisa wengine walioagizwa kukamatwa na kushitakiwa ni pamoja na Katibu Mkuu katika Wizara ya Fedha, Kamau Thugge, Dk. Susan Jemutai Koech kutoka Wizara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkurugenzi Msimamizi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Kerio Valley (KVDA), David Kimosop.

Taarifa kuhusu gharama ya ujenzi wa mabwawa hayo zilizua mijadala katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii Kenya, kuanzia Machi mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na KVDA ilieleza kuwa ililipa kampuni hiyo ya Italia Sh. bilioni 21 za Kenya.

Ilisema mkandarasi huyo, CMC Di Ravenna, alilipwa kwa mafungu mawili kujenga mabwawa hayo ya Arror na Kimwarer katika jimbo la Elgeyo Marakwet Kaskazini mwa Kenya.

Wananchi Kenya waliingiwa na huzuni baada ya kupata taarifa kuwa mabilioni ya fedha yaliopangwa kufadhili mradi wa bwawa la maji katika eneo la Bonde la ufa magharibi mwa Kenya zimechukuliwa na wajanja.

Wakenya walijitosa katika mitandao ya kijamii kuelezea hasira na kuchoshwa kwa kile wanachotaja kuwa ni vitisho vya bure kwa viongozi wafisadi katika serikali.

Akizungumzia kuhusu uchunguzi kuhusu namna kandarasi za ujenzi wa mabwawa hayo zilivyotolewa, Noordin amesema: "Imebainika kwamba namna mpango ulivyoidhinishwa, ulivyopatikana na malipo yalivyotolewa kwa mradi wa mabwawa hayo, umegubikwa kwa ukiukaji mkubwa wa sheria." **BBC**

## Helikopta kutumika kuwaokoa samaki

**OTTAWA,** Canada

IDADI ya samaki aina ya salmon nchini Canda wanatarajiwa kuokolewa kwa ndege baada ya kukwama mtoni kutokana na maporomoko ya ardhi.

Juni mwaka huu maofisa, waligundua kuwa miamba iliyoshushwa na maporomoko imeziba kipande cha mto Fraser katika Jimbo la British Columbia, na kuwazuia maelfu ya samaki hao kuelekea juu ya mto ambao hutaga mayai.

Vikosi vya uokozi vimepiga kambi katika eneo hilo kupanga mkakati wa namna ya kuwaokoa samaki hao kwa kuwasafirisha mpaka upande wa pili wa mto kwa kutumia helikopta.

Haijulikani ni samaki wangapi ambao wamenasa, lakini inaaminika kuwa ni 700 tu ambao wameweza kuvuka kikwazo hicho bila ya msaada wowote.

Makabila mengi ya asili nchini Canada wanategemea samaki hao kama chakula na bidhaa muhimu kwenye sherehe zao za jadi.

Waziri wa Uvuvi wa Canada, Jonathan Wilkinson, alisema serikali imekuwa ikifanya kazi usiku na mchana kuwasaidia samaki hao.

Hata hivyo, bado haijatangazwa tarehe rasmi ambapo uokozi huo wa kutumia ndege utafanyika. Vikosi vya uokozi kwa sasa vinatengeneza bwawa la kuwazuia samaki hao.

Baada ya kuwekwa kwenye bwawa hilo, watawekwa mataki ya lita 780-2,700 na kunyanyuliwa na helikopta kutoka eneo hilo la maporomoko.

Matanki hayo yatapuliziwa hewa ya oxygen ili kuwasaidia samaki watulie na kufika salama.

Wakati bwawa hilo likitengenezwa, maofisa sasa wanafunga vifaa maalum baadhi ya samaki hao ili kufuatilia myenendo yao baada ya kuokolewa. **BBC**



Wanajeshi wa Kenya wakiwa katika operesheni ya kuwasaka wanajeshi wa kikundi cha kigaidi cha Al-Shabaab nchini Somalia. **PICHA: AP**

## Kenya yawasaka Al-Shabab

**NAIROBI,** Kenya

VYOMBO vya usalama nchini Kenya vinafanya operesheni kwenye eneo la Kaskazini Mashariki mwa nchi hiyo ambako inapakana na nchi ya Somalia.

Operesheni hiyo inalenga kuwasaka wapiganaji wa Al-Shabab wanaojipenyeza kuingia nchini humo.

Tangu juzi vikosi vya wanajeshi kutoka Kenya vimekuwa vikifanya doria kwenye maeneo ya rasi ya Kamboni, Kiunga na Ishakani, huku baadhi ya raia kwenye maeneo hayo wakisema ni kama kuna katazo la kutotembea usiku licha ya kuwa haijatangazwa.

Kwa mujibu wa idara ya ujasusi nchini Kenya, wapiganaji wa Al-Shabab wanadaiwa kuingia nchini Kenya ili kutekeleza mashambulizi.

Kwa mujibu wa wakazi wa eneo hilo milio ya risasi na milipuko ya mabomu ilisikika siku ya Jumamosi, hata hivyo chanzo bado hakijafahamika.

Kwa mujibu wa mashahidi, Jeshi la Ulinzi la Kenya, Kenya Defense Forces (KDF) limewataka wakazi wa maeneo hayo kutokwenda mbali na makazi yao.

Operesheni hiyo imefanyika kufuatia mfululizo wa mashambulizi yaliyotokea wiki mbili zilizopita.

Mnamo Julai 15, mwaka huu mapigano kati ya wapiganaji wa Al-Shabab na vikosi vya ulinzi vya Kenya yalisababisha wapiganaji watatu wa kundi hilo kuuawa na askari wawili wa Kenya kujeruhiwa.

Uhasama kati ya Al-Shabab na majeshi ya Kenya umekuwa ukitokea mara kwa mara katika eneo hilo, hasa tangu jeshi la Kenya kutumwa kusaidia nchini Somalia mnamo mwaka 2011. **RFI**

## Ufaransa, Burundi warudiana

**BUNJUMBURA,** Burundi

WAKATI Burundi ikiwa chini ya vikwazo vya Umoja wa Ulaya (EU) tangu mwaka 2015, serikali ya Ufaransa imetangaza kurejesha ushirikiano wake na nchi hiyo katika sekta ya ulinzi.

Ufaransa imeamua kuchukuwa hatua hiyo kwa kutoa upya msaada wake wa moja kwa moja kwa Burundi tangu mwanzoni mwa mwaka 2019, kwa matumaini ya kuimarisha uchumi ambao unaelezwa kufikia kiwango cha chini kabisa.

Ushirikiano huo ni katika lengo la kuinua uchumi na uelewano wa kisiasa katika nchi hiyo ambayo inaelezwa kuwa inaendelea kuvunja haki za binadamu kwa mujibu wa mashirika ya kimataifa ya haki za binadamu.

Hatua ya Ufaransa kutoa msaada kwa Burundi imetokana na ziara iliyofanywa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Burundi, Ezekiel Nibigira, mjini Paris Oktoba mwaka jana. **RFI**

# Mwinyi adai Makamba kamkwaza

Na Mwandishi Wetu

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Pili, Alhaji Ali Hassan Mwinyi, ameelezea kutofurahishwa kwake na kitendo kilichofanywa na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, January Makamba, kutumia picha yake katika mitandao ya kijamii muda mfupi baada uteuzi wake kutenguliwa na Rais John Magufuli.

Akizungumza nyumbani kwake jijini Dar es Salaam jana, Mwinyi alisema picha iliyotumiwa na January Makamba katika mitandao ya kijamii ikimwonyesha yeye ameketi naye wakicheka muda mfupi baada ya kufukuzwa uwaziri imemkwaza kutokana na kutumiwa katika mazingira na wakati usiostahili.

Mwinyi alisema picha hiyo ilipigwa zamani wakati Makamba alimpomtembea kwa ajili ya kupata uzoefu wake kwa kuwa naye aliwahi kuwa Waziri wa Muungano na Mazingira na pia alikwenda kumwomba aandike dibaji katika kitabu chake.

Kuhusu waraka ulioandikwa na Makatibu Wakuu wastaafu wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuf Makamba kwenda kwa Baraza la Viongozi Wastaafu, Mwinyi alisema "huo ni utoto".

Mwinyi alipongeza majibu yalitolewa na Katibu wa Baraza hilo, Pius Msekwa kwenda kwa wawili hao na kusema walioandika waraka huo wameshindwa kufuata katiba na taratibu za chama na kwamba "viongozi wastaafu hawawezi kupoteza muda wao kwa masuala ya kitoto".

Mwinyi aliwataka Watanzania kumuunga mkono Rais John Pombe Magufuli kwa juhudi kubwa anazozifanya kuleta maendeleo kwa muda mfupi.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Massanja Kadogosa (kulia), akishikana mikono na Meneja Mauzo Taifa wa Kampuni ya Tanga Cement (TCPLC), Leslie Massawe, wakati wa hafla ya ufunguzi wa safari za treni za mizigo katika reli ya Dar- Tanga- Kilimanjaro uliofanyika mjini Moshi, mwishoni mwa wiki. Wengine kutoka kushoto ni Meneja Uhusiano na Mawasiliano ya Nje wa Tanga Cement, Mtanga Noor, Meneja Kiwanda cha Tanga Cement, Mhandisi Ben Lema, Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya Tanga Cement, Diana Malambugi na Meneja Biashara wa Kampuni hiyo, Peet Brits. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa akata mzizi wa fitina

INATOKA UK.3

watumiaji wa eneo hilo kwa maana ya wanyama na binadamu.

"Nataka nije niwasilikize, tuelimishane na migogoro mingine ni ya kutokuelewa. Kuna sheria, kanuni na taratibu zetu. Tutazungumza umuhimu wa hapa (Ngorongoro), umuhimu wenu na umuhimu wa rasilimali ili wote tuwe na uelewa wa pamoja," alisema.

Aidha, alisema hairuhusiwi mtu yeyote kupotosha au kuongoza kundi lolote kuhusu jambo lolote, na wanapaswa kusubiri kikao chake na wananchi hao.

Akizungumzia eneo hilo, alisema sifa ya Tanzania duniani ni kuwa ni chimbuko la dunia imechangiwa kwa kugundulika kwa masalia ya binadamu wa kale, na kwamba hakuna binadamu atakayejisifu kuwa asili yake ni kwake bia kuitaja Tanzania.

"Tunapoadhimisha umri wa miaka milioni 2.8 toka kugundulika kwa mwaka 1959, liligunduliwa na wataalamu wa ikolojia. Uelewa mkubwa kwa wanasayansi na wana historia kuhusu mchango wa Afrika na Tanzania duniani," alisema.

Aliongeza kuwa: "Masalia ya Zinjathropus na zana za mawe walizotumia ni uthibitisho kwamba Tanzania ndiyo chimbuko la binadamu, imehifadhi kumbukumbu hizo kwa miaka milioni mbili iliyopita."

Alisema eneo la Olduvai linaonyesha nyayo za zamadamu milioni 300.6 iliyopita alianza kusimama na kutembea na kwamba zina manufaa ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kwa Watanzania.

Aidha, aliwataka wataalamu kuendelea na utafiti wa namna ya kuzihifadhi nyayo hizo kwa uwazi ili zitembelewe na watu wengi zaidi kwa kuwa ndiyo chanzo cha kujitambua, kujua uhusiano wa dunia na mazingira.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Dk. Luis na Dk. Mary Leakey waliishi kwenye kambi hiyo wakifanya utafiti kuanzia mwaka 1930 hadi 1984 na walifanya kazi zote na kugundua mambo muhimu ambayo yanaonekana, kukumbukwa na kupewa heshima kubwa.

"Ni vyema nyumba walizotumia wataalamu hao na vifaa vingine yakiwamo magari vikaendelea kuhifadhiwa. Nakiri kuvutiwa na mnara wenye sanamu ya Zinjathropus, unavutia watalii wengi. Ushauri wangu paboreshe pasiachwe wazi, pajengewe seng'enge na kuwe na kibanda cha msimamizi akitoa maelezo, ni eneo lenye upepo mkali na vumbi," alisema.

Aidha, Waziri Mkuu alitaka ajira kutolewa zaidi kwa wenyeji ili kuendelea kuwahusisha kwenye uhifadhi, huku akieleza mapato ya eneo la Olduvai kuwa yameongezeka kutoka Sh. milioni moja hadi Sh. bilioni 2.5 kwa mwaka.

Kadhalika, aliagiza kuboreshwa Bonde la Olduvai kwa kulifanya la kuvutia zaidi bila kupoteza sura yake kwa kujenga banda la kivuli kwa wageni wanaotembelea, huku eneo lenye udongo ukionyesha matabaka ya miaka milioni 1.8 utengenezwe vizuri kwa kuvutia zaidi.

Waziri Mkuu alisema pia ni vyema kwenye maeneo hayo kukawa na maelezo ya lugha ya Kiswahili, huku akiwataka Watanzania kuwajibika kutunza maeneo yote yaliyohifadhiwa kwa manufaa endelevu.

Aidha, alisema serikali imeondoa vikwanzo vya magari ya watalii kusimamishwa njiani kwa ajili ya ukaguzi kwa kujenga vituo maalum vya ukaguzi kwa kuwa awali walisimamishwa na askari wa usalama barabarani zaidi ya mara 20 kutoka KIA hadi Manyara.

"Tumeshaelekeza gari lolote la utalii litasimamishwa kwa utaratibu maalum ambako mawakala wote wanajua, kwa kufanya hivyo kutapunguza usumbufu barabarani," alisema.

Awali, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala, aliwatoa wasiwasi wananchi wa Ngorongoro juu ya uhusiano na ushirikiana kati ya wizara na wao, na kwamba umefanyika utafiti mkubwa wa kisayansi juu ya hatima ya uhifadhi na maisha ya watu.

"Kumekuwa na migongano kutokana na sababu zilizo wazi, wakati hifadhi inatangazwa wananchi walikuwa 8,000 kwa sasa kuna watu zaidi ya 95,000 eneo ni lile lile, mazingira ya mifugo, mahitaji yameongezeka na utamaduni wa wananchi wa asili unabadilika," alisema.

Alisema zamani chakula kilitokana na utamaduni wa kuwa na mifugo lakini kwa zaidi ya asilimia 25 hawana mifugo yoyote, wanakula vyakula vingine.

Waziri Kingwangala alisema migogoro iliyopo inafahamika ndiyo maana serikali iliona kuna haja ya kutumia mbinu za kisayansi zaidi kutafuta suluhisho na kwamba majibu ya kisayansi yatatoa majibu sahihi.

***Salome Kitomari (Dar) na Cynthia Mwilolezi (Ngorongoro)***

# Reli Tanga- Moshi

INATOKA UK.5

miaka michache, Tanga itakuwa zaidi ya ilivyokuwa enzi zake za katani, kitu kilichofanya Tanga uwe mji maarufu nchini Tanzania na Afrika Mashariki.

Kampuni ya Tanga Cement ni kati ya wateja wakubwa wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) na mwaka 2016 ilisaini mkataba wa iliyokuwa TRL (Kampuni ya Reli) kuwezesha usafirishaji wa saruji kutoka Tanga Cement kuwaendea wateja wa kampuni hiyo waliopo mikoa ya Mwanza na Kigoma

Mkataba huo wa makubaliano ulitiwa saini ili kuwezesha usafirishaji wa zaidi ya tani 35,000 za saruji kwa mwezi.

Kampuni ya Tanga cement ilitengewa vichwa vitano vya treni na kichwa cha treni cha kupangia mabehewa ili kuwezesha usafirishaji watani 20,000 kwa mwezi kutoka Ponge hadi kigoma, na tani 15,000 kwenda Mwanza.

" Hii ilikuwa ni hatua muhimu ya mafanikio katika kupatia ufumbuzi usafirishaji wa saruji. Tumejenga uhusiano mzuri sana na TRC ambapo tunakutana mara kwa mara kuhakikisha kuwa kila jambo linakwenda sawa hasa kuhusiana na utekelezaji wa mkataba huo, wa makubaliano na tunatoa mapendekezo yanapohitajika na kushauri marekebisho ya hapa na pale, aliongeza Swart.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Majaliwa alisema kuwa wachambuzi wa kimataifa wanakadiria kuwa kutumia reli badala ya barabara kunapunguza gharama za usafirishaji kwa kiwango cha asilimia 30-40.

Kwa mujibu wa wadau wa sekta ya usafirishaji, kusafirisha tani moja ya saruji kutoka Tanga hadi Moshi kwa barabara kunagharimu Sh. 40,000, wakati reli inakadiriwa kugharimu Sh. 28,000. Tanga Cement yenyewe inatarajia kusafirisha jumla ya tani 1,600 kwa wiki na 80,000 kwa mwaka kutoka kiwandani Tanga hadi Moshi.

# Ajali ya Hiace yaua

INATOKA UK.3

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Richaed Abwao, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, na kusema kuwa Hiace iliyokuwa akitoka Kakola kuelekea mjini Kahama uligongana uso kwa uso na Land Cruiser.

Hata hivyo, Abwao alisema waliofariki dunia majina yao hayajatambuliwa na kuongeza kuwa miili imehifadhiwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama ikisubiri ndugu.

Kuhusu chanzo cha ajali, Kamanda Abwao alisema ni mwendokasi wa magari yote mawili na kuwataka madereva wa vyombo vya moto kuwa makini wanapokuwa barabarani ili kuepusha ajali ambazo sio za lazima, ambazo zimekuwa zikitokea kwa uzembe wa madereva.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Dk. George Masasy, alithibitisha kupokea miili sita juzi usiku, huku miili mitatu ikiwa ni watoto wadogo na mingine mitatu ya watu wazima.

Aidha, Dk. Masasy, alisema alipokea majeruhi 24, lakini wawili waliruhusiwa usiku ule ule na 22 waliobaki hali zao zinaendelea vizuri.

Hata hivyo, alisema watatu wakitarajiwa kuhamishiwa katika Hospitali ya Rufani ya Bugando mkoani Mwanza kutokana na hali zao kuwa mbaya.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


**NIPASHE NI JIBU LAKO**


**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**


### CHETI KIMEPOTEA



**YUSUPH J. MWENDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.158/0663** kilichotolewa na TOSAMAGANGA SEKONDARI mwaka 1996. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/4675/2019**

### VYETI VIMEPOTEA



115335602

**LEONCE FELIX SWAI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1343-0178** kilichotolewa na ANNE MARIE SEKONDARI mwaka 2008. Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.0800-0675** kilichotolewa na LOYOLA SEKONDARI mwaka 2011. Form four Living Certificate iliyotolewa na ANNE MARIE SEKONDARI mwaka 2008. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/148508/2019.**

### KUPOTEA KWA CHETI CHA URAIA



115335402

**Cheti No. CT 0000661 ya ndugu LEONILA DEGUZMAN SERUHERE** iliyotolewa Dar es salaam mwaka 2005. Ilipotea tarehe 12.10.2018 Kawe. Tukio hili limeripotiwa kituo cha polisi Kawe na kupewa Kumb. **KW/RB/4586/2019.** Yeyote atakayeiona aipeleke kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye au awasiliane na ndugu Leonila kwa simu **No. 0753 685576.**

### CHETI KIMEPOTEA



115335301

**MWANAKOMBO MOHAMED** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0907/0023** kilichotolewa na ZINGIBARI SEKONDARI mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/TAN/RB/101942/2019.**

### CHETI KIMEPOTEA



115335102

**VAILETH B. CHAULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S3733-0028** kilichotolewa na MAHENJE HIGH SCHOOL mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MB/RB/1829/2019.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO KAWE**


**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo: KAWE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 129/2019**

**Ombi la JOTI SEVERINI KADUNGALA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu FIKIRI SEVERINI KADUNGALA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe ……………………….. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo ya **FIKIRI SEVERINI KADUNGALA.**

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 6/8/2019.



115335002


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KOSCIELNY, RENNES WAKUBALIANA



**LONDON,** England

BEKI Laurent Koscielny ameripotiwa kwamba amefikia makubaliano binafsi ya kujiunga na klabu ya Rennes ya Ufaransa.

Arsenal ilitangaza mapema mwezi huu kwamba mchezaji huyo wa zamani wa Ufaransa alikataa kusafiri na kikosi kwenda nchini Marekani, sababu kubwa ya kukataa ni baada ya klabu hiyo kushinda kumwongezea mkataba mpya.

Mchezaji huyo ambaye amebakiwa na mwaka mmoja kwenye mkataba wake, anafanya kila linalowezekana ili arudi kwenda kucheza nyumbani kwao Ufaransa na amekuwa na majadiliano na Rennes, kwa mujibu wa RMCsport.

Gazeti hilo la Ufaransa limedai kwamba, pande hizo mbili zimefikia makubaliano na sasa kilichobaki ni kuishawishi Arsenal ili ikamilisha uhamisho wake.

Ilibainisha Jumanne wiki hii kwamba, kocha wa Arsenal, Unai Emery alizungumza mara tatu na Koscielny ili kumshawishi kujiunga na timu hiyo kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya.

Baada ya washikabunduki hao kushinda mabao 3-0 dhidi ya Colorado Rapids, Emery alisema kwamba alijaribu kuzungumza na beki huyo mwenye umri wa miaka 33, lakini alishindwa kumshawishi.

"Alianza kufanya mazoezi na sisi na nilizungumza naye mara tatu kuhusu hali yake ya mkataba mpya," alisema Emery akiwaambia waandishi wa habari.

# Juventus yapanga kumuuza Higuain

**TURIN,** Italia

JUVENTUS inapanga kumuuza Gonzalo Higuain kipindi hiki cha majira ya joto licha ya kuonyesha kiwango kizuri kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Tottenham.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ambaye alivaa kitambaa cha unahodha alipoingia kipindi cha pili, alifunga wakati wakichezea kichapo cha mabao 3-2 na alionekana kuwa kwenye kiwango cha kuvutia.

Hata hivyo, gazeti la Gazzetta dello Sport limedai kwamba mchezaji huyo hayupo kwenye mipango ya Juventus msimu huu na ataondoka kabla ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili mwezi ujao.

Higuain, ambaye alitumia msimu uliopita akicheza kwa mkopo kule C Milan na baadaye Chelsea, amejulishwa na maofisa wa klabu hiyo kwamba hayupo kwenye mipango ya baadaye ya klabu hiyo.

Klabu ya AS Roma kwa sasa ndiyo inayotajwa kuwa inamwania raia huyo wa Argentina, na imeripotiwa kwamba, klabu hizo zimefikia makubaliano ya ada ya usajili ya pauni 5.4.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, inapanga kumuuza mshambuliaji wake, Edin Dzeko kwenda Inter Milan wiki hii kwa ada ya pauni milioni 13.5 na Higuain ndio anaonekana kuwa mbadala wake.





# *Bosi wa Bayern asema Sane ataondoka City*

**MUNICH,** Ujerumani

PEP Guardiola hivi karibuni alisema anatarajia Leroy Sane kubakia katika Klabu ya Manchester City kipindi hiki cha majira ya joto, hata hivyo, Mwenyekiti wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge ana mtazamo tofauti kabisa.

Bayern imekuwa ikimwania mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, lakini matamshi ya Guardiola ya hivi karibuni yameonekana kama yakiwaonya.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, Mwenyekiti huyo wa klabu hiyo ya Ujerumani amesema: "Sitaki kuzungumza chochote kwa sasa. Lakini kama kuna jambo la kutangaza tutafanya hivyo. Lakini sio muda mrefu kutoka sasa.

"Sijui kama Pep anajua kila kitu kinachoendelea ndani ya klabu yake," aliongeza kusema Rummenigge. "Hajui chochote. Ngoja tusubiri."

Sane emabakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake wa sasa, lakini City wameshindwa kumshawishi kusaini mkataba mpya hadi sasa.

"Klabu hiyo ilimpa ofa mwaka jana," alisema Guardiola.

"Tunataka watu wawe na furaha hapa. Tutamsaidia kwa kadili ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba anaijua thamani yake.

"Malengo ni kuhakikisha anabakia na sisi hapa. Nimezungumza na klabu mara 10, kwamba nataka watu wawe na furaha hapa, kama hawataki tunaweza kuwaachia waondoke."

HABARI MICHEZO

# Bale atakiwa Shanghai Shenhua

**SHANGAI,** China

GARETH Bale anakaribia kumaliza kipindi chake cha uchezaji katika Klabu ya Real Madrid na sasa anawaniwa na klabu tajiri ya nchini China.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 raia wa Wales amekuwa kwenye wakati mgumu pale katika dimba la Bernabeu na Jumapili kocha wake, Zinedine Zidane alibainisha kwamba mchezaji huyo anaondoka.

Wakala wake, Jonathan Barnett alimshutumu Zidane kwa kuonyesha zarau kwa Mfaransa huyo kwa kumlazimisha aondoke.

Gazeti la Daily Mail limeripoti kwamba, Bale kwa sasa ana uwezekano mkubwa wa kutua kwenye Ligi Kuu ya nchini China.


Na imebainishwa kwamba, klabu hiyo ipo tayari kumlipa mchezaji huyo mshahara wa pauni milioni 350,000 kwa mwezi na kumfanya kuwa mchezaji atakayelipwa fedha nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu ya China maarufu kama Super League.

Imeripotiwa kwamba, Klabu hiyo ipo tayari kulipa kiasi hicho cha mshahara kwa sababu hawatalipa ada ya uhamisho.

Bale, ambaye mkataba wake wa sasa na Real Madrid ulikuwa unamalizika mwaka 2022, hatakiwi tena na Manchester United au Tottenham.



# MATA ANA IMANI POGBA ATABAKI MAN UNITED



**MARINA BAY,** Singapore

JUAN Mata ana matumaini makubwa na kiungo, Paul Pogba atabakia Manchester United na kulisaidia jiji hilo kuwa la rangi nyekundu tena.

Miaka mitatu baada ya kurudi pale Old Trafford kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 89, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 ametamka hadharani nia yake ya kuondoka klabuni hapo ili kwenda kutafuta changamoto mpya.

Uvumi zaidi ulikolezwa na wakala wake, Mino Raiola ambaye mara kwa mara amekuwa akisema kuwa mteja wake anataka kuondoka klabuni hapo na anawaniwa na klabu za Real Madrid na Juventus.

Lakini Pogba ameonekana kama vile amezipa kisogo taarifa za uhamisho wakati huu akiwa na United kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya na ameonekana kuwa na molari nzuri. Lakini mchezaji mwenzake Mata, akimzungumzia mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na timu ya taifa ya Ufaransa, amesema ana imani kubwa kuwa atabakia kwa mashetani hao wekundu.

"Wote tunamjua Paul na ni kiungo wa kuvutia na ni mtu mzuri pia, mwenye mawazo chanya, na mwenye ushawishi kwa kila mtu," amesema Mata.

"Nafikiri ana furaha, anawafanya watu wote wakusanyike pamoja na nina imani naye kubwa zaidi.

# *Milner hajui hatima yake Liver*

**BOSTON,** Marekani

JAMES Milner amebainisha kwamba hajui majaliwa yake ndani ya klabu ya Liverpool kwa sababu mazungumzo kwa ajili ya mkataba mpya bado hajafanyika.

Nahodha huyo msaidizi wa klabu hiyo ameingia kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake akiwa amebakiwa na miezi 12 ambao alisusaini mwaka 2015 wakati alipowasili hapo akitokea Manchester City.

Hadi sasa hakuna ishara yoyote ya mazungumzo kuhusu mkataba wake mpya na kwamba hali hiyo inazidi kumweka kwenye sintofahamu, ingawa yeye mwenyewe anataka kubakia klabuni hapo.

Wakati wawakilishi wa Milner walijaribu kuanzisha mazungumzo ya mkataba mpya msimu uliopita, lakini Liverpool hadi sasa haijaonyesha nia yoyote ya kutaka kufanya mazungumzo ya mkataba mpya.

Milner alikuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kurudi katika klabu yake ya zamani ya Leeds kipindi hicho cha majira ya joto.

Lakini baada ya klabu yake hiyo ambayo ndiyo ya kwanza kuichezea soka la kulipwa kushinda kupanda Ligi Kuu, mpango huo ulishindikana.

Lakini sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 amebainisha wazi hofu yake, kwani haoni jitihada zozote za kuanza kwa mazungumzo ya kusaini mkataba mpya.

Milner amesema: "Mwaka jana tulizungumza na klabu na tuliwauliza kama wanataka kufanya jambo lolote na walisema hapana.

"Hadi sasa hatujasikia chochote, hivyo sijui hatima yangu, maana kwa sasa nina miezi 12 tu iliyobaki katika mkataba wangu."



# DONDOO MAGAZETI




# PSG YASISITIZA HAKUNA OFA KWA NEYMAR

## ●●● Yabainisha bado ni mchezaji wao halali hata kama...

**PARIS,** Ufaransa

MKURUGENZI wa Klabu ya Paris Saint-Germain, Leonardo amesisitiza kwamba hakuna kilichobadilika kuhusu usajili wa mchezaji wao anayetaka kuondoka, Neymar.

Nyota huyo wa kimatifa wa Brazil amekuwa akihusishwa na mpango wa kusajiliwa kwa kiasi kikubwa cha fedha kurudi Barcelona, ikiwa ni miaka miwili tu baada ya kuondoka kwa Klabu hiyo ya Katalunya kujiunga na waajiri wake wa sasa kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia pauni milioni 198.

Ripoti zilibainisha kwamba, Barcelona wametuma ofa kwa klabu hiyo ya jijini Paris kwa ajili ya kumsajili Neymar, lakini Leonardo amesisitiza kuwa hakuna ofa iliyotolewa kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27.

**Leonardo ameiambia Sky Sports: "Hakuna tofauti yoyote, hakuna chochote hadi sasa. Hakuna ofa kamili iliyotolewa kwa ajili ya Neymar. Ana mkataba na sisi na ni mchezaji wetu.**

"Narudia, hakuna ofa yoyote kamili. Hali imekuwa hivyo hivyo kwa kipindi cha siku 10."

Naye kocha wa PSG, Thomas Tuchel aliongeza: "Ni suala kati ya Klabu na Neymar."Alifanya mazoezi na timu kwa mara ya kwanza jana, mwanzo alikuwa akifanya peke yake, na tunakwenda nae kwenye ziara nchini China.

"Hivyo kwa sasa naweza kusema ni mchezaji wetu na tutaendelea kumtumia, kwani hakuna kilichojitokeza hadi sasa kuhusu hatima yake klabuni hapa."

Klabu ya Barcelona wiki iliyopita iliripotiwa kwamba, imetoa ofa kwa Barcelona kwa ajili ya kumsajili Neymar ambayo itawahusisha pia wachezaji wawili ili kubadilishana naye.

## ZISIKUPITE

### BALE ATAKIWA CHINA

KLABU ya nchini China ya Beijing Guoan imeripotiwa imepanga kumsajili winga wa Real Madrid, Gareth Bale. Klabu hiyo, ina mpango wa kumfanya winga huyo mwenye miaka 30 kuwa mchezaji anayelipwa zaidi katika ligi kuu ya China. ***(Telegraph)***

### YAKUBALI MASHARTI YA HARRY

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwa imekubali masharti ya kumsajili beki wa Leicester na timu ya taifa ya England, Harry Maguire. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 atawasili katika uwanja wa Old Trafford kwa dau la pauni milioni 80. ***(Daily Mail)***

### AMALIZANA NA ARSENAL

BEKI wa Klabu ya Arsenal, Laurent Kolscielny, amemalizana na timu hiyo baada ya kuigomea kwenda kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi nchini Marekani na sasa atajiunga na miamba wa Ufaransa, Rennes. ***(RMC Sport)***

### MILNER HAJUI HATIMA YAKE

KIUNGO wa kati wa Klabu ya Liverpool na timu ya taifa ya England mwenye umri wa miaka 33, James Milner, amesema hajui hatma yake katika timu hiyo, kwani hadi sasa hakuna ishara yoyote ya mazungumzo kwa ajili ya kusaini mkataba mpya na yeye bado anataka kuendelea kubakia hapo Anfield. ***(Sky Sports)***

### BAYERN YAJITOSA KWA ZAHA

MIAMBA wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bayern Munich, wamejitosa kwenye mbio za kuwania kumsajili winga wa kimataifa wa Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 26, baada ya kushindwa kupata saini ya Leroy Sane wa Manchester City na Gareth Bale kutoka Real Madrid. ***(Bild)***

### CRYSTAL PALACE WAKATALIWA

OMBI la Klabu ya Crystal Palace la kutaka kumsajili beki wa kimataifa wa England, Reece James kwa pauni milioni 20, limekataliwa na klabu yake ya Chelsea. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 alihudumu msimu uliopita akiichezea Wigan.***(Daily Star)***

### SHAPARENKO AGOMBEA EPL

TIMU za Arsenal, Chelsea, Manchester United na West Ham zote za Ligi Kuu ya England, zimejitosa kwenye mbio moja ya kuwania kumsajili nyota wa klabu ya Dynamo Kiev, Mykola Shaparenko. ***(Daily Mail)***

### WAKATAA OFA KWA ASENSIO

KLABU ya Real Madrid imekataa ofa sita za kumuuza kiungo wa kati wa Hispania, Marco Asensio, ambaye anahusishwa na uhamisho wa kuelekea katika timu ya Liverpool. ***(Daily Mail)***

### IWOBI AITISHA ARSENAL

WINGA wa kimataifa wa Nigeria na klabu ya Arsenal, Alex Iwobi, ameonya kwamba ataihama Arsenal iwapo mchezaji anayedaiwa kuwa na thamani ya pauni milioni 80, Wilfried Zaha atajiunga na Arsenal. ***(Daily Star)***

### MAN CITY KUMSAJILI ALMADA

MANCHESTER City inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Thiago Almada, ambaye kwa sasa anaichezea Velez Sarsfield ya nyumbani kwao. Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England wameripotiwa kutaka kumsajili mchezaji huyo kwa pauni milioni 16. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## AS Kigali yaitisha KMC

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa timu ya KMC umesema mchezo wao wa kwanza wa Kombe la Shirikisho Afrika watakaoucheza ugenini dhidi ya AS Kigali ya Rwanda kati ya Agosti 9, 10 na 11 utakuwa ni mgumu kwao.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Jackson Mayanga alisema timu ya AS Kigali ni miongoni mwa timu nzuri ukanda wa Afrika Mashariki.

"Nitaendelea na programu zangu kama kawaida kwa ajili ya msimu ujao pamoja na mchezo wa kombe la shirikisho lengo ni kupata matokeo mazuri na timu yangu," alisema Mayanga.

Mayanga alisema timu yake inaendelea na mazoezi ya nguvu ikiwa pamoja na kusaka mechi mbalimbali za kirafiki, kabla mashindano hayo hayajaanza.

"Mchezo wetu wa kwanza wa Kombe la Shirikisho utakuwa mgumu, lakini naahidi kuwapa wachezaji wangu mbinu ambazo zitawalinda na maadui," alisema Mayanga.

Kwa upande wa msemaji wa timu hiyo, Anuari Binde aliwataka mashabiki wake waendelee kuwapa ushirikiano ili warudi na matokeo mazuri.

"Tunaomba mashabiki wetu wazidi kutupa ushirikiano turudi na ushindi nyumbani," alisema Anuari.

Alisema watatoa taarifa ya michezo yote ya kirafiki watakayoicheza, ambayo wanatarajia kucheza nje na ndai ya Mkoa wa Dar es Salaam.

"Tutatoa taarifa zote kuhusu maendeleo yetu endapo kama tutakwenda kucheza nje ya Dar es Salaam tutawafahamisha," alisema msemaji huyo.

# STARS YAANZA KAMBI KUIWINDA KENYA

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) jana imeanza mazoezi kwenye Uwanja wa Boko Veterani uliopo Bunju jijini Dar es Salaam tayari kwa kujiandaa na mchezo wao wa kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Taifa Stars itaikaribisha Harambee Stars Julai 28, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa na mchezo wao wa marudio utachezwa Agosti 2 mwaka huu jijini Nairobi nchini Kenya.

> **Akizungumza na Nipashe jana kocha msaidizi wa Taifa Stars, Juma Mgunda alisema wachezaji wote wameripoti kambini na jana jioni walianza rasmi mazoezi.**

"Wachezaji wote wameripoti kambini leo jioni rasmi (jana) tutaanza kufanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na Harambee Stars," alisema Mgunda.

Alisema wachezaji wote wameripoti wakiwa na afya nzuri, na kudai kila mchezaji ameahidi ushindi.

Kocha huyo aliwataka Watanzania kuwapa ushirikiano ili waweze kufanya vizuri katika mchezo huo na kuweza kuiwakilisha vema nchi yetu.

"Tunaomba Watanzania watupe ushirikiano ili tuweze kufanya vizuri tupeperushe bendera ya Tanzania," alisema.



Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda (kulia), akitoa tamko la kuridhia kuunganishwa kwa Tamasha la Urithi Festival kwa mwaka kufanyika pamoja na Tamasha la Utamaduni la Jumuiya ya Afrika (JAMAFEST) mbele ya Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Susan Mlawi (kushoto), wakati wa kikao kilichofanyika jijini Arusha jana, kujadili namna ya matamasha hayo yanavyoweza kuunganishwa kwa sababu yote yana dhana moja ya kutangaza utalii wa kiutamaduni na tarehe za maadhimisho ziko sawa mwezi Septemba 21- 28 jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAELEZO**




Wachezaji wa timu KCCA ya Uganda wakishangilia ushindi. **PICHA: MTANDAO**

## KCCA yajiwekea historia

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya KCCA ya Uganda ilifanikiwa kutwaa taji la Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati, Kombe la Kagame baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Azam ya Dar es Salaam Uwanja wa Nyamirambo mjini Kigali juzi.

Bao lililoipa ushindi huo timu hiyo ya Mamlaka ya Jiji la Kampala lilifungwa na Mustafa Kiiza dakika ya 62 aliyemtungua kipa Mghana wa Azam FC, Razack Abalora kwa shuti la mguu wa kushoto.

Kwa ushindi huo, KCCA wamezawadiwa dola za Kimarekani 30,000, huku washindi wa pili, Azam wakipewa dola 20,000 na washindi wa tatu, Green Eagles ya Zambia dola 10,000.

Ushindi huo unamaanisha KCCA wanatwaa taji lao la pili tu la kombe la Kagame kihistoria baada ya awali kulitwaa mwaka 1978 ilipoifunga Simba ya Tanzania pia katika fainali.

Aidha, kwa ushindi huo KCCA wameendeleza ubabe wao kwa Azam FC baada ya kuilaza 1-0 pia Julai 9 katika mchezo wa Kundi B na kumaliza kileleni wakifuatiwa na timu hiyo ya Tanzania.

Azam walikuwa wakilishikilia taji hilo tangu mwaka 2015 baada ya kulitwaa mara mbili mfululizo nyumbani, Dar es Salaam 2015 wakiifunga Gor Mahia ya Kenya 2-0 na 2018 walipoichapa Simba 2-1, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Taifa.

Azam imeshindwa kuwa timu nyingine ya Tanzania, baada ya Yanga kutwaa Kombe la Kagame nje ya ardhi ya nyumbani. Yanga ilibeba taji hilo mara mbili nje ya nyumbani, mwaka 1993 na 1999 mjini Kampala, Uganda.

Azam waliiingia fainali baada ya ushindi wa penalti 5-4 Ijumaa kufuatia sare ya 0-0 ndani ya dakika 120 dhidi ya AS Manyema Union ya DRC hapo hapo Uwanja wa Nyamirambo, wakati KCCA iliifunga Green Eagles ya Zambia 4-3 katika mchezo uliodumu kwa dakika 120 baada ya sare ya 2-2 ndani ya dakika 90.

Mapema jioni ya leo Green Eagles ilifanikiwa kumaliza nafasi ya tatu baada ya kuichapa Manyema Union 2-0, mabao ya Edward Mwamba dakika ya 28 na Amity Shamende dakika ya 69 Uwanja wa Nyamirambo pia.

# Michezo

Jumanne Julai 23, 2019

Nipashe




PSG yasisitiza hakuna ofa kwa Neymar

UKURASA 30



Mshambuliaji wa Tottenham Hotspurs, Harry Kane (kulia), akiifungia bao la tatu timu yake dhidi ya Juventus wakati wa mchezo wa kirafiki baina ya timu hizo uliopigwa nchini Singapore juzi Jumapili. Spurs iliibuka na ushindi wa mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga: Hatuwahofii Townships Rollers

## ●●● Yasema inawamudu, inajipanga...

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa timu ya Yanga umesema kwamba, kikosi chake kipo kamili 'gado' kuivaa timu ya Townships Rollers ya nchini Botswana kwenye mchezo wao wa raundi ya kwanza ya mchujo wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Shirikisho la Soka la Afrika, Caf, juzi lilitangaza ratiba hiyo ambapo wawakilishi wa Tanzania Bara kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga zitaanza raundi ya kwanza ya mchujo kuwania kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo.**

Pia kwa timu za Azam na KMC nazo zitaanza kwenye hatua hiyo ya mchujo ili kufuzu kucheza hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Mechi za kwanza zitachezwa kati ya Agosti 9 na 11 na Yanga itaanzia nyumbani jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu kutoka mkoani Morogoro ambako Yanga imeweka kambi yake, Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Salehe alisema kuwa timu inaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mchezo huo.

"Wachezaji huku wanaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mchezo wetu na timu hiyo ya Botswana, tunaamini kwamba mchezo huu utakuwa na ushindani mkubwa, lakini tunajiandaa vizuri kuwakabili," alisema Hafidh.

Aidha, aliongeza kuwa, licha ya kocha wao mkuu, Mwinyi Zahera kutokuwapo na timu hiyo, hakuna kilichoharibika na amebainisha programu ya mazoezi inaendelea kama kawaida.

"Programu za mwalimu wetu zinaendelea kama kawaida na muda wowote kocha Mwinyi Zahera ataungana na timu yake," alisema Mratibu huyo.

Alisema wachezaji wote wana morali ya hali ya juu na wameahidi kufanya vizuri katika mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa. Alisema amewasiliana na Zahera kuhusu kutoka kwa ratiba ya mashindano hayo na amesema anawaamini wachezaji wake na hakuna kitakachoharibika.

Endapo Yanga itashinda raundi hiyo, itakutana na mshindi kati ya Green Mamba ya Eswatini na Zesco ya Zambia. Na mchezi za raundi ya pili zitachezwa kati ya Septemba 13, 14 na 15 na marudiano kati ya Septemba 27, 28 na 29.

# Simba SC sasa yawabadilishia kibao do Songo

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA wa Simba, Patrick Aussems, amesema kuwa baada ya kutoka kwa ratiba ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa wanalazimika kufanya mabadiliko kwenye programu ya maandalizi yao.

Ratiba ya michuano hiyo iliyotolewa na Shirikisho la Soka la Afrika, Caf, inaonyesha kuwa Simba itacheza mchezo wake wa awali kati ya Agosti 9, 10, 11 dhidi ya UD do Songo ya Msumbiji.

Akizungumza kupitia mtandao wa kijamii wa Instagram wa Simba kutoka nchini Afrika Kusini jana, Aussems alisema watalazimika kubadili programu ya mazoezi yao ili kwenda sawa na ratiba hiyo.

"Mchezo huu ni muhimu tunatakiwa kubadili kidogo programu yetu sababu tunatakiwa kuwa tayari kwa hiyo michezo miwili. "Hatukutarajia hilo ni kama mshangao kwetu, lakini haina namna, tunahitaji kubadili ratiba yetu ili kuwa tayari kwa michuano mikubwa," alisema.

Simba imeweka kambi nchini Afrika Kusini kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya unaotarajiwa kuanza Agosti 23.

Ratiba hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika itailazimisha Simba pia kupanga tarehe nyingine ya tamasha lao la kila mwaka la kutambulisha kikosi kipya maarufu kama Simba Day, ambalo hufanyika Agosti 8, kwa sababu siku hiyo watakuwa nchini Msumbiji kwa ajili ya mechi dhidi ya UD do Songo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002